# Nipashe

Alhamisi Agosti 29, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580009

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Dereva adaiwa kulipindua lori, akutwa na pombe kali

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Mtaalamu alivyochambua TGNP vs ngono kwa watoto

Mfumuko wa volkano wagunduliwa

Kutoelewa afya ya udongo kunavyompa dhiki mkulima

MASIKINI 'MAPAFU YA DUNIA'...

Moto usiokwisha ndani ya msitu unaozalisha robo oksijeni duniani

UKURASA 13

# Maandamano kudai ndege yatawanywa

• **Wahusika** watinga ubalozi Afrika Kusini, watatu mbaroni, polisi waweka msimamo... *Endelea ukurasa 2*






Askari Polisi wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), wakiwa wameimarisha ulinzi nje ya Ubalozi wa Afrika ya Kusini hapa nchini, katika Barabara ya Shaaban Robert, jijini Dar es Salaam jana, baada ya mamia ya wananchi wakiwa na mabango kuandamana hadi ubalozini hapo, wakishinikiza kuachiwa kwa ndege ya serikali inayoshikiliwa, jijini Johannesburg nchini humo, kwa amri ya Mahakama. **PICHA: JOHN BADI**

## Bashiru: Mil.50/- kila kijiji tayari

UKURASA 4



## Ripoti waliotelekeza watoto hadharani

UKURASA 2

**MICHEZO** LIPULI YAANZA TAMBO LIGI KUU UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri Mkuu wa Mauritius, Pravind Kumar, kwenye ukumbi wa maonyesho wa Pacifico Yokohama nchini Japan, jana. Wote wawili wanahudhuria Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo kwa Maendeleo ya Afrika TICAD 7. Kushoto ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi. **PICHA: OWM**

# Maandamano kudai ndege yatawanywa

**Na Romana Mallya**

HUKU kukiwa na zuio la Jeshi la Polisi kufanya maandamano, jana mamia ya watu walijitokeza kuandamana kwenye Ubalozi wa Afrika ya Kusini nchini kushinikiza kuachiwa kwa ndege ya serikali aina ya Air Bus A220-300 inayoshikiliwa Afrika Kusini kwa amri ya mahakama.

Waandamanaji hao walifika ubalozini huko wakiwa wameshika mabango wakiimba "tunataka ndege yetu".

Ndege hiyo inashikiliwa Afrika Kusini kwa siku tano sasa kutokana na deni ambalo Tanzania inadaiwa na raia wa nchi hiyo, Hermanus Steyn.

Wakiwa nje ya majengo ya ubalozi huo jijini Dar es Salaam jana, baadhi yao walianza kupiga 'push up' huku wengine wakiimba "Mzee Mandela, South wamemsaliti".

Wakati wakiendelea kuimba, magari ya Jeshi la Polisi yakiwa yamesheheni askari wenye silaha, yalifika eneo hilo na askari wake walishuka na kujipanga kisha kutoa amri kwa waandamanaji kutawanyika kwa amani. Amri hiyo ilitolewa mara tatu.

Baada ya tangazo hilo la polisi kutolewa mara tatu, waandamanaji walitawanyika kila mmoja akikimbia njia yake, lakini baadhi yao walikamatwa.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, ambaye alikuwapo eneo la tukio, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wanawashikilia watu watatu kwa ajili ya mahojiano kutokana na maandamano hayo.

"Tulipata taarifa kuwa vijana na watu wengine ambao wamejipanga pamoja, wametokea walikotokea, wakaandamana kuja Ofisi ya Ubalozi wa Afrika Kusini nchini, lengo walikuwa wanafuatilia madai ya kuonyesha hisia za Watanzania baada ya ndege kukamatwa Afrika Kusini.

"Sisi, Jeshi la Polisi kama ilivyo ada haturuhusu maandamano na haturuhusu mtu kufanya vile anavyofikiria yeye, baada ya kupata taarifa, nilimwamuru Mkuu wa Kikosi cha Kutulia Ghasia na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala kuchukua hatua ya kuzuia maandamano haya na kuwakamata walioratibu na kuyaongoza.

"Kupitia serikali, tunafahamu waziri mwenye dhamana alikuwa tayari ameshakwenda Afrika Kusini kufuatilia suala hilo la ndege ambalo linaendelea kushughulikiwa.

"Kwa hiyo, Watanzania wawe watulivu na wasubiri hatua zinazochukuliwa na serikali. Hili walilolionyesha kwa kuandamana halina baraka kwetu na lazima tuchukue hatua," alisema.

Kamanda Mambosasa aliwataka Watanzania waendelee kuheshimu sheria hata kama kuna jambo limefanyika haliwapendezi.

"Tukiacha haya yakaendelea, yanaweza kutufikisha mahali ambako siyo pazuri, lakini pia yanaweza kuharibu taswira ya nchi. Wamefanikiwa kuwakamata viongozi watatu ambao walionekana waliratibu maandamano hayo ili hatua nyingine za kisheria ziendelee," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, akitoa ufafanuzi kuhusu kukamatwa kwa ndege hiyo, alisema kesi iliyofunguliwa na Steyn nchini humo haihusiani kabisa na suala la ubia kati ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na lile la Afrika Kusini.

"Kwenye hii kesi kuna mkanganyiko kidogo, wengi wanaihusisha na madeni ya zamani kwenye Shirika la Ndege kati ya Air Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika Kusini," Dk. Abbas alisema.

"Hii ni kesi tofauti kabisa, ni kesi kati ya serikali (Tanzania) na huyu bwana, ambaye ni raia wa Afrika Kusini, haihusiani na masuala ya ndege, ni kesi iliyoanzia nyuma miaka ya 80, huyu bwana kuna mali zake zilitaifishwa hapa Tanzania."

# Ripoti waliotelekeza watoto yaiva

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema ripoti kuhusu watoto waliotelekezwa na wazazi wao wa kiume imeshakamilika na wakati wowote wataiwasilisha kunakohusika.

Vilevile, amesema wameandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Mirathi ili vifungu vyenye upungufu vifanyiwe marekebisho na Wizara ya Katiba na Sheria.

Amesema lengo la mabadiliko hayo ni kuwasaidia wajane ambao kwa muda mrefu wamenyanyasika na kudhulumiwa mali za wenza wao kutokana na upungufu katika sheria hiyo.

Makonda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ripoti ya mkutano wake na wajane uliofanyika Aprili mwaka huu ukihusisha wajane 5,181 waliowasilisha changamoto zao.

Alisema ripoti kuhusu watoto itawasilishwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kuweka mifumo itakayosaidia kuondokana na changamoto hizo.

"Tumeona tutengeneze mifumo imara itakayosaidia wanyonge kupata haki zao wakati wowote na siyo suala la Makonda au Rais John Magufuli kuwapo madarakani ndo kuwapo na utatuzi, mifumo itasaidia miaka yote," Makonda alisema.

Aprili 9, mwaka jana, Makonda aliwaita ofisini kwake watoto waliotelekezwa na

INAENDELEA UK. 8

# Mahakama ya Mafisadi yaelezwa waziri alivyodhamini Dola 500,000

**Na Beatrice Shayo**

MAHAKAMA Kuu Kitengo cha Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi maarufu Mahakama ya Mafisadi imeelezwa namna waziri wa zamani wa serikali ya awamu ya tatu, Edgar Maokola Majogo, alivyomdhamini Alhaj Kilahama kukopa Dola za Marekani 500,000 kwa Kampuni ya Superior Financing Solution.

Kampuni hiyo inamilikiwa na mfanyabiashara aliyetajwa na Rais John Magufuli kuiibia serikali Sh. milioni saba kila dakika na washtakiwa wenzake walitajwa kuwa ni Alloycious Gonzaga na Isaack Kasanga.

Shahidi wa kwanza katika kesi hiyo, Dimon Mwakababu, ambaye pia ni Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, alidai hayo jana mbele ya Jaji Lilian Mashaka, wakati akichambua fomu za mikopo za kampuni hiyo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Christopher Msigwa, Mwakababu alidai Novemba 19, 2014, Kilahama aliomba mkopo wa Dola za Marekani 500,000 kwenye kampuni hiyo.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Ulevi wa dereva wasababisha ajali

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

GARI lenye tela likiwa limesheheni makaa ya mawe likitokea katika mgodi wa Ngaka Luanda, Mbinga mkoani Ruvuma, limepinduka karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, huku dereva akidaiwa kukutwa na pombe kali aina ya K-Vant na wakati huo huo amelewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 9:00 usiku katika barabara ya Songea- Njombe.

Alisema gari lenye namba za usajiri T. 134 BYH aina ya Scania ikiwa na tela lenye namba za usajiri T. 197 DFX, mali ya kampuni ya Charan Singh and Sons Limited ya Moshi mkoani Kilimanjaro, lilikuwa likiendeshwa na Peam Reginald (28) mkazi wa Moshi liliopakia makaa ya mawe kwenda Kajiado, Kenya.

Kamanda Maigwa alisema gari hilo liliacha njia na kupinduka huku akieleza chanzo kuwa ni ulevi wa dereva.

Baada ya kutokea ajali hiyo, Kamanda Maigwa alisema askari wa usalama barabarani walifika eneo la tukio na kumkuta dereva akiwa na chupa ya K-Vant ndani ya gari na baadaye alipimwa kilevi na kukutwa kiwango cha 534.9 mg/100ml ambacho kilisababisha kushindwa kukata kona kwenye barabara hiyo na kupinduka.

Kamanda Maigwa alisema kutokana na tukio hilo, dereva huyo amefungiwa leseni ya udereva kuanzia jana hadi kesi yake itakapomalizika mahakamani na kwa sasa anashikiliwa na polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

Wakati huo huo, polisi mkoani Ruvuma wanamshikilia Hussein Dumba (27) mfanyakazi wa kampuni ya ujenzi wa barabara ya Chico kwa tuhuma za kumgonga mtembea kwa miguu na gari alilokuwa akiiendesha kwenye barabara ya kutoka Mbinga mjini kwenda Mbamba Bay wilayani Nyasa.

Maigwa alisema dereva huyo alimgonga mtembea kwa miguu huyo Agosti 26, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku katika kijiji cha Mhekela na kumsababishia kifo.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiruka kukwepa takataka na matopo yaliyoachwa bila kuzolewa katika Soko la Buguruni jijini humo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Japan yaimwagia Afrika dola bil. 20

**Na Mwandishi Wetu**

JAPAN imetangaza kutenga Dola za Kimarekani bilioni 20 kwa kipindi cha miaka mitatu kwa nchi za Afrika ili kuziwezesha kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo itakayoleta mageuzi ya kiuchumi.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema wakati Japan ikitangaza hilo, Tanzania imeeleza kuwa fedha zitakazotengwa zitatumika katika utekelezaji wa mkakati wake wa uchumi wa viwanda.

Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi rasmi wa Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD7) unaofanyika jijini Yokohama.

Alisema serikali ya Japan itaendelea kuchangia maendeleo ya Afrika kupitia programu mbalimbali za ushirikiano kwa kuimarisha rasilimali watu, elimu ya awali kwa watoto na kuboresha huduma za afya kwa wote.

Waziri mkuu huyo alisema kupitia mpango wa TICAD, ushirikiano kati ya Japan na Afrika umeimarika na kwamba nchi hiyo itaendelea kuhakikisha inahamasisha kampuni za Japan kuwekeza Afrika na hadi sasa sekta binafsi ya Japan imewekeza Dola za Marekani milioni 20 katika nchi mbalimbali za Afrika.

Kuhusu programu mbalimbali zinazotekelezwa na Japan katika kuchangia maendeleo ya Afrika, ikiwamo ile ya ABE-African Business Education Initiative, alisema tayari zaidi ya vijana 350 kutoka nchi mbalimbali za Afrika wanafanya mafunzo kwa vitendo kwenye kampuni mbalimbali kupitia mpango huo na wengine 3,000 ambao walishapitia mpango huo kama wawezeshaji.

Abe alisema Japan itaendelea kuchangia kwenye sekta ya afya husussan masuala ya dawa, lishe na kutoa mafunzo ya ujuzi kwa nchi mbalimbali za Afrika.

Pia alisisitiza kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na Afrika kwenye ujenzi wa miundombinu kama barabara na bandari pamoja kutoa wataalamu kwa kuwa nchi yake haijawahi kupungukiwa na wataalamu.

Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, ambaye anahudhuria mkutano huo akimwakilisha Rais John Magufuli, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazozalisha malighafi zinazosafirishwa nje kwa ajili ya kuongezewa thamani jambo linaloifanya Afrika, Tanzania ikiwamo, kujikuta ikisafirisha ajira na kutengeneza soko la bidhaa kutoka katika mataifa mengine.

Alisema kwa sasa Tanzania imedhamiria kupitia viwanda kutumia malighafi zake kuzalisha bidhaa mbalimbali, hivyo kutengeneza ajira kwa watu wake lakini kuuza nje ya nchi na kuzalisha fedha za kigeni.


FARM RADIO INTERNATIONAL — REDIO KWA WAKULIMA

## VACANCY ANNOUNCEMENT

| | |
|---|---|
| Position title: | Country Representative |
| Position Location: | Arusha |
| Reports to: | Director of Operations-Africa |
| Application Deadline: | 16th September 2019 |

**Introduction to the Organization**

Farm Radio International (FRI) is a Canadian non-profit organization at the forefront of ICT-enabled extension and communication for scale. FRI's interactive rural radio approach addresses the information, communication and extension needs of millions of small-scale farmers, rural entrepreneurs and citizens.

In Tanzania, FRI currently works in thematic areas of agriculture value chains, livestock, climate information services and conservation agriculture, in collaboration with over 15 radio stations nationally, reaching out to millions of small scale farmers.

**Summary of the Position**

The Country Representative is a key position in Farm Radio International, with overall responsibility for leading and developing the growth of the organization within a specific country. The key expectations of a successful Country Representative are that they: create a strong reputation and profile for FRI; engage with government partners effectively; position FRI to participate in major rural development initiatives; secure new funding opportunities; lead the development of a strong, capable, high-functioning, well-coordinated and motivated staff team and; oversee the sound administration and financial management of FRI operations in the country. The Country Representative will also support team members in working effectively with and fulfilling accountabilities to FRI staff in other teams and offices, including the regional, international, and specialty teams and departments.

**Summary of Responsibilities:**

1. Provide overall leadership and coordination to the Country Team including the development of country strategic planning.
2. Raise the profile and develop/maintain an excellent reputation for impact, reliability and performance of Farm Radio International within the country and region.
3. Develop, build and nurture strong relationships with key stakeholders including the public, private, civil society, media, farmer organizations and funding agencies.
4. Grow the organization both in budget size and portfolio within the country by Identifying and developing prospects for new projects in country working closely with FRI's Program Development Team and systems.
5. Manage the country office and any field-offices or sub-offices including all the assets of the organization and oversee the security, safety and welfare of staff.
6. Manage the Human Resources administration to ensure effective and efficient systems for recruitment and retention of staff.
7. Oversee the financial management of the country office including developing and monitoring country annual budgets, spending plans and related periodical financial reports.

**QUALIFICATIONS**

**Experience and requirements**

- +10 years of experience in program implementation and management, including in the communication for development sector or agricultural development at a senior management level
- University degree in agriculture, communication, international development, environmental studies or a related field, a master's degree (an asset and added advantage)
- Experience in leading teams and multiple, multi layered relationships in an international institution
- Proven skills at managing projects with various donor agencies
- Proficiency in English, with very good written and oral communication skills including development of donor reports
- A mature self-starter, good communicator and team builder with the ability to manage and motivate teams

Knowledge requirements

- Knowledge and experience in project development and implementation, including project cycle management and results-based management
- Knowledge of broadcasting and ICT for development (an asset)
- Knowledge of agriculture and rural development priorities and policies in Tanzania and sub-Saharan Africa
- Knowledge of national or international donors and strategic or implementing partners in East Africa
- Significant knowledge of the principles of gender equality and women's rights and experience in integrating these principles into the project cycle

**Skills and attributes**

- Good team building skills
- Excellent intercultural communication skills
- Good organizational and time management skills; ability to work under pressure to meet deadlines
- Be comfortable working with minimal supervision and limited resources

**Application procedure**

Interested and qualified Tanzanians are invited to send their applications enclosing a covering letter and detailed curriculum vitae with names of three referees, and their contacts to tanzania@farmradio.org and Cc rchapota@farmradio.org

**Please note that Farm Radio International has no recruitment agent, therefore all applications should only be sent to the above mentioned addresses. Only shortlisted candidates will be contacted.**

21539490I

# Katibu Mkuu CCM asema mil. 50/- kila kijiji zimeshatolewa

## Amtaja Sugu akisisitiza ahadi hiyo ya serikali ilitafsiriwa vibaya...

"Kwa hiyo, nadhani watu wanaosubiri mgawo kila kijiji tushushe mafurushi ya pesa, kwa kweli watakuwa wametutafsiri vibaya."



**Na Enock Charles**

KATIKA sehemu ya kwanza ya mahojiano haya jana, Dk. Bashiru Ally, alieleza namna wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi wa serikali za mitaa, watakavyopitia mchujo mkali.

Vilevile, Katibu Mkuu huyo wa CCM alizungumzia kanuni za uchaguzi na mipango ya chama hicho kuelekea uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Leo katika sehemu ya pili ya mahojiano haya, Dk. Bashiru anafafanua kuhusu utekelezaji wa ahadi ya serikali ya kutoa Sh. milioni 50 kila kijiji/mtaa.

Dk. Bashiru aliiambia Nipashe kuwa fedha hizo zimeshatolewa, lakini dhana ya utolewaji wake haijaeleweka kwa umma kutokana na ahadi hiyo kutotafsiriwa vyema.

Alisema CCM haikuahidi kutoa fedha taslimu kwa kila kijiji/mtaa, bali kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutekeleza miradi inayowahusu. Endelea na mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa:-

**SWALI: Kuna wakati CCM inaacha kutekeleza mambo yaliyomo kwenye ilani yake, mfano suala la kutoa Sh. milioni 50 kila kijiji. Kwanini?**

**DK. BASHIRU:** Hebu isome vizuri ile ilani, ile ahadi ipo kwenye dhana ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, umeelewa?

Sasa, wakipeleka Sh. milioni 50 kila kijiji, unazigawaje? Kwa sababu hapa hakuna anayesema kila kijiji hakijafikiwa katika maendeleo, umeelewa?

Wengine walidhani tutaenda na mafurushi na askari wa FFU (Kikosi cha Kutuliza Ghasia cha Jeshi la Polisi) na magari, tunashusha vifurushi vya hela, halafu tunawapa watu Sh. milioni 50 zenu, mafurushi haya hapa, hapana!

**SWALI: Kwa hiyo ahadi yenu hii ilieleweka vibaya?**

**DK. BASHIRU:** Siyo kueleweka vibaya, sisi tunaoahidi ndiyo tunaotafsiri pia utekelezaji, kuna maeneo ambayo yamejengewa barabara za lami, hayako kwenye ahadi kwa kutajwa eneo, lakini tulisema tutapeleka miundombinu wezeshi.

Sasa, unapoangalia eneo limeathiriwa na mafuriko, mahitaji yanapelekwa kule hujayaahidi, kuna mambo ya ajali, kuna mahitaji mapya, kwa mfano tuliahidi kutoa mikopo kwa wanafunzi, tunaongeza idadi.

Ukibanabana, ukakamata madini, unaona ni mapato huku unaongeza jambo. Tuliahidi vitu vinne; kupunguza umaskini, kuongeza mazingira ambayo yatawezesha watu kujipatia riziki kwa njia ya ajira, kupambana na ufisadi na rushwa na kuhakikisha nchi inabaki na usalama, hata hizo Sh. milioni 50 zinaingia kwenye duru hiyo.

Tuliposema tunatoa elimu bure kuanzia elimu ya msingi mpaka kidato cha nne, hatukusema tunaanza lini, tungeweza kuanza hata mwaka 2017, tungeweza kuanza hata 2018, tungeweza kuanza hata 2019.

Si tumetekeleza? Lakini tulianza 'immediately' (mapema) baada ya Rais John Magufuli kuapishwa. Kwa hiyo, kila kijiji kuna pesa imepelekwa kule na miradi tuliyoitekeleza ina akisi kwa kila kijiji, kila kitongoji, kila kata, kila nyumba imefikiwa, hata wewe hapo (mwandishi) angalia kwenye ilani yetu hatukusema tutajaza watu mapesa mfukoni.

Kwa hiyo, nadhani watu wanaosubiri mgawo kila kijiji tushushe mafurushi ya pesa, kwa kweli watakuwa wametutafsiri vibaya.

Najua wako wenzetu watani zetu, Sugu (Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini-Chadema) nilimsikia bungeni, yeye anasema anasubiri Sh. bilioni tisa zipelekwe kwenye jimbo lake kama mgawo wa Sh. milioni 50.

Ukweli ni kwamba kila kijiji tumekifikia, kila kata, kila kitongoji na tutaendelea na utekelezaji wa ilani hii na hata ile ya baada ya 2020 kwa sababu tutashinda kwa kishindo tu, wembe ni uleule.

**SWALI: Wewe ni mtaalamu wa sayansi ya siasa. Unafikiri mfumo wa vyama vingi una tija kwa Tanzania?**

**DK. BASHIRU:** Vyama vingi vinafanya vizuri na mimi naridhika na mchango wa vyama vya upinzani. Kwa mfano, hata kanuni hizi (za uchaguzi wa serikali za mitaa) zimeboreshwa kutokana na ushiriki wao.

Mijadala bungeni inachangamka kwa sababu ya ushiriki wao, maoni yao katika vyombo vya habari, maoni yao katika mitandao ya kijamii. Kwa hiyo, tunao utamaduni sasa umeshakomaa wa vyama vingi na hatuwezi kurudi nyuma na Watanzania hawataki turudi nyuma.

Ni jukumu la vyama vyetu, sote tusibweteke, tufanye kazi ya siasa kwa masharti ya sheria ya vyama vya siasa, tumesajiliwa kwa sheria, tusimamie sheria hizo za usajili wetu, tunafanya siasa kwa mujibu wa katiba yetu, tunafanya kazi kwa mujibu wa utamaduni wetu wa kitaifa ambapo siasa siyo uadui, tukitofautiana tuvumiliane, kila raia ataishi bila hofu yoyote, ana uhuru wa kujieleza.

**SWALI: Ipo hoja kwamba CCM inapata mgawo mkubwa wa ruzuku na hivyo kuwa uwezo mkubwa wa kujenga ofisi nyingi na kuua usawa wa kisiasa nchini. Unasemaje kuhusu hili?**

**DK. BASHIRU:** Kwa sababu sisi pia tuna majukumu makubwa, yaani kuendesha chama kikubwa namna hiyo, kwanza ruzuku haitoshi, huwezi ukaendesha chama hiki kikubwa kwa ruzuku peke yake, lazima michango ya wanachama na ada na miradi ya kiuchumi ihusike.

Chama ni kikubwa, kipo kila wilaya, kila kijiji, kila kata, kila mtaa, kila kitongoji na uongozi upo, ni mtandao mkubwa sana.

Kwa hiyo, ruzuku tunayoipata ni kubwa kweli kwa sababu tuna wingi wa wawakilishi kwenye vyombo vya dola, lakini haitoshi mpaka tutafute vyanzo vingine.

Hata hizo ofisi tunazozijenga zingine za Sh. milioni 200 hadi 300, siyo za ruzuku, hatupeleki hata shilingi moja, mie nimeenda Busega, sikupeleka hata shilingi moja pale, ile ofisi natamani ingekuwa ni makao makuu ya ACT, waulizeni wamejenga ofisi ngapi, mbona hamuwaulizi?

Busega tumejenga bila ruzuku, ni wanachama wamejitolea kwa sababu chama hiki kina wafanyabiashara, kina wakulima, kina machinga, kina bodaboda, kina watumishi wa serikali, kina wavuvi, ukianza kuchangisha kujenga ofisi, watu wanatoa mifukoni mwao wanajenga chama chao, huwezi ukajenga chama kwenye mitandao ya kijamii.

**SWALI: CCM imerithi mali zingine kutoka TANU na ina umri mkubwa kuliko vyama vingine vyote vyenye usajili, huoni hiyo ni sababu nyingine kuwa na ofisi nyingi nchini?**

**DK. BASHIRU:** Mimi nimeingia nina mwaka mmoja tu, lakini nimeshasimamia ujenzi wa zaidi ya ofisi 20 kwenye huo mwaka mmoja, nitakupa orodha ya ofisi tulizojenga ndani ya mwaka mmoja, nao wajenge angalau makao makuu basi.

**SWALI: Kila unapomalizika uchaguzi, vyama vya upinzani vimekuwa vikilalamika CCM kubebwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Malalamiko haya yana ukweli?**

**DK. BASHIRU:** Sasa mimi nisemeje mkurugenzi? Yaani mimi nimeshinda, sawa na mpira bwana, yaani refa anasema goli halafu mashabiki huko wanalalamika ooh wanagongana vichwa huko kwamba labda ni uchawi ama labda tumelogwa, eeh wewe hujawahi kusikia visingizio vya mpira eeh hali ya hewa!

Wakati timu zetu zinaenda Misri, wakati fulani watu wakawa wanasema hali ya hewa ya jangwani, ha ha ha! Sasa wewe ukishakubali kwenda Misri, ujue kuna hali ya hewa ya jangwa, hivyo ujiandae na hali ya hewa ya jangwa, ukienda sehemu ya baridi, ujiandae na hali ya hewa ya baridi, wajiandae kushindana na chama kikubwa.

**SWALI: Kuna ukimya kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti kuhusu waliofuja mali za chama. Kulikoni?**

**DK. BASHIRU:** Hilo nimeshalifafanua sana, litashughulikiwa na kamati iliyoundwa kwa ajili ya kazi hiyo.

**ITAENDELEA KESHO**

## Mfugaji adaiwa kuteka wanafunzi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Kiongozi, Halmashauri ya Babati, mkoani Manyara wanadaiwa kutekwa na mfugaji wa ng'ombe na kwenda kuwafanyisha kazi ya kuchunga mifugo yake kwa ujira wa Sh. 30,000 kwa mwezi.

Tukio hilo limegundulika jana baada ya gazeti hili kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Maisaka, Catherine Koila, aliithibitishia Nipashe kuwapo kwa matukio ya watoto kupotea na kudai kuwa jana alipata taarifa ya mtoto mmoja wa shule hiyo kutishiwa kuuawa kama hatasaidia kupatikana kwa watoto wengine.

Koila alidai alipopata taarifa hizo alimwagiza askari mgambo wafanye msako wa mtu aliyempa kazi mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) ya kuwatafuta wenzake na kumfikisha ofisi za kata ili achukuliwe hatua.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kiongozi, Kanankira Shami, alikiri kuwapo kwa tukio la watoto kupotea katika shule yake, huku akidai mtoto wa kwanza tangu alivyotoweka hajapatikana mpaka sasa ni miezi minne na mwingine ametoweka kwa wiki tatu.

Alisema wanafunzi wote ni wa darasa la sita na walikuwa na uwezo kitaaluma.

Mwalimu Shami alisema baada ya wanafunzi hao kupotea walitoa taarifa polisi na jana limetokea tukio la mtoto mwingine ambaye alimwambia mwalimu huyo kuwa alifuatwa na mtu (jina tunalo) na kumtaka mtoto huyo kuwatafuta wenzake watatu ili awakabidhi kwake.

Alidai kuwa mtoto huyo baada ya kupewa kazi hiyo alikuwa akimkwepa mzee huyo, lakini alimfuata nyumbani kwao akiwa na wenzake wawili na kumtisha kuwa akitoa siri watampoteza na kumuua.

Mwalimu Shami alidai walipomhoji mtoto kama mtu huyo alimwambia nia ya kuwachukua watoto hao, alijibu kuwa mtekaji huyo alimwambia wanapelekwa kwenda kufanya kazi ya kuchunga mifugo na kulipwa Sh. 30,000 kwa mwezi.

"Agosti 20, mzee huyo alimfuata mtoto huyu nyumbani kwao na akamwambia tunaona umeshindwa kazi yetu na ukitoa siri hiyo tunakuua maana hutaki kutoa ushirikiano," alidai Mwalimu Shami.




Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), Mkoa wa kihuduma Kibaha mkoani Pwani, wakibadilisha kipande cha bomba chakavu na kuweka bomba jipya la nchi 30, katika eneo la Maili Moja jana. Ubadilishaji wa mabomba chakavu ni miongoni mwa mikakati ya mamlaka hiyo, ili kuboresha huduma kwa wananchi. **PICHA: FRANK MONYO**

## Uthibitishaji udahili chuo zaidi ya kimoja mwisho leo

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu (TCU), imetangaza kuwa muda wa kuthibitisha udahili kwa waombaji waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya kwanza ya udahili kwa mwaka wa masomo 2019/20 utafungwa leo.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alitangaza hatua hiyo jana na kueleza kuwa katika awamu ya kwanza waombaji ni zaidi ya 16,000 sawa na asilimia 77.

"Tume inapenda kuwatoa hofu waombaji ambao hawajakamilisha uthibitisho kuwa hakuna mtu atakayekosa udahili kwa sababu ya kushindwa kujithibitisha," alisema.

Alisema kwa kuzingatia hilo, kutakuwa na awamu tatu za kuthibitisha udahili kwa waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja.

Alisema awamu ya kwanza waliodahiliwa zaidi ya chuo zaidi ya kimoja ilianza Agosti 22, hivyo itaisha leo.

"Awamu ya pili itaanza Septemba 8 hadi 14 ambayo itahusisha waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja na walioshindwa kujithibitisha katika awamu ya kwanza kutokana na sababu mbalimbali. Awamu ya tatu itaanza Septemba 21 hadi 30, ambayo nayo itahusisha waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja na walioshindwa kujithibitisha katika awamu ya kwanza, ya pili," alisema.

Pia alisema TCU inaendelea kuwasisitiza waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja ambao bado hawajathibitishwa, wathibitishe vyuo wanavyopenda kusoma mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu usiokuwa wa lazima.

Prof. Kihampa alisema kwa wale ambao wana changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

"Waombaji wote watakaoshindwa kujithibitisha wanashauriwa kuwasiliana na vyuo husika, ili wapokee taarifa zao na kuzifanyia kazi," alisema.

Alisema maombi ya udahili na kujithibitisha yanafanyika kupitia akaunti za chuo ambazo waombaji walizitumia wakati wakiomba udahili.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili linawahusu nyie viongozi halmashauri

**KATIKA** gazeti letu la jana, tuliandika habari yenye ujumbe wa Waziri kumpa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, jukumu la kuwacharaza viboko watumishi wenye utendaji wa mwendo wa konokono.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ndiye anayetoa maelekezo hayo, kwenye kutia saini ujenzi na uwekezaji wa vitega uchumi jijini Dodoma.

Waziri anachosema kinamaanisha kuwachagiza watumishi wa halmashauri kufanyakazi kwa wakati, bidii na kwa ufanisi badala ya kutoa visingizio kibao, kuchelewesha kazi na hata wakati mwingine kuzikwamisha.

Waziri anachosema ni kweli kwa sababu miradi mingi katika halmashauri haifanyiki kikamilifu na kwa wakati. Kinachoweza kutumiwa ni kutoa maelezo kama meya hajasaini, madiwani hawajaidhinisha au yanasubiriwa maoni ya mtunza hazina wa halmashauri.

Pamoja na Waziri Jafo kutoa maagizo ya ufuatiliaji huo, ni wakati wa kuwa na mikakati na programu za kuuchunguza utendaji kazi wa viongozi wanafanyaje kazi?

Tunajiuliza hivi inapotokea Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi wa ujenzi hospitali ya wilaya na serikali imetoa fedha, lakini kazi haifanyiki ni nani anayekwamisha? Ni Mkurugenzi wa Halmashauri anayezuia fedha, ni meya na madiwani, mtunza hazina, je, ni mkandarasa asiye na uwezo? Miradi inapokwama ni wazi kuwa wapo maofisa wa halmashauri wasiotimiza wajibu.

Iwapo serikali imeshatoa fedha za ujenzi wa hospitali ya wilaya, ardhi imeandaliwa? Ofisa ardhi amepima kiwanja? Wahandisi wa ujenzi wamekadiria gharama? Wataalamu wa zabuni wameziandaa na kuzitangaza? Kama yote yamefanyika mkwamo uko wapi?

Tunaona kuwa hicho ndicho Waziri Jafo anachotaka kifanyike kila mmoja atimize wajibu wake na kama hatimizi ni nani wa kumbana? Katika utaratibu huo wa Jafo wa kutandika watendaji viboko suala la uwajibikaji ni muhimu.

Tunampongeza Waziri Jafo kwa sababu imekuwa ni mazoea kazi hazifanyiki mpaka wakati wa ziara za Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu au pengine Waziri ndipo hoja zinapoibuliwa kuwa barabara, zahanati na shule hazijakamilika?

Tunajiuliza inakuwaje barabara isimalizike hadi ujio wa Rais kijijini au mkoani hapo? Watu wanapotoa malalamiko kwa kiongozi ndipo kazi inapokamilika? Siku zote hizo watu wanakuwa wapi wasifanye kazi hadi kufokewa na viongozi?

Maelekezo hayo ya Waziri Jafo, yafanyiwe kazi na inapotokea changamoto kama hizo viboko vitembee kwa maana ya ufuatiliaje ifahamike uzembe ulikuwa wapi na mhusika anacharazwa bakora ili ionekane tatizo la uwajibikaji lilianzia wapi na uwajibikaji ulikwamia wapi ili sera na sharia zitumike kwenye uwajibikaji.

Pamoja na kutotekelezwa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo, suala jingine ambalo linahitaji watu kucharazwa viboko ni hili la kazi kwa 'mazoea' mfano bomba zinavuja iwe vyooni, uwanjani au kwenye matangi ya kuhifadhi maji.

Katika mazingira kama hayo hakuna wa kuzikarabati na kila siku maji yanapotea bila viongozi wa halmashauri kuwajibika wala kuwajibishana.

Katika mazingira kama hayo ofisi nyingi za umma taa za umeme zinapoungua hakuna wakiziangalia, vitasa vikivunjika na masinki ya vyoo yakiharibika hakuna anayewajibika moja kushughulikia matatizo hayo.

Tunaona kuwa kupuuza huko mambo wanayoamini kuwa ni madogo kama bomba zinazovuja na viti vilivyovunjika ofisini, kunaendeleza mlolongo wa uzembe kwenye miradi mikubwa kama barabara, ujenzi wa vitega uchumi, ofisi za umma, hospitali na visima au miradi ya maji.

Kwa hiyo utaratibu wa kucharaza viboko kwa maana ya kufuatilia na kubaini viongozi viraka ni muhimu ili kujua nani anayekwamisha maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

N Reubeni Lumbagala, Kongwa.

# Karibu mradi umeme Julius Nyerere utuvushe

**DIRA** ya maendeleo iliyopo ni kwamba Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati, ifikapo mwaka 2025. Katika utekekezaji wa dira hiyo, mkazo uko katika ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, kukuza sekta ya kilimo na uwepo wa nishati ya umeme wa uhakika ili kuwezesha kuendesha shughuli za viwandani.

Nisisitizie umuhimu wa nishati ya umeme katika azma hiyo. Ongezeko la viwanda nchini liko dhahiri limeongeza mahitaji ya nishati umeme.

Safari ya ujenzi wa viwanda inaendelea kwa kasi, wawekezaji wa ndani na wageni wanaendelea kuhamasishwa kuwekeza nchini katika nyanja nyingi mbali na viwanda, kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji, elimu na afya.

Niseme, uwekezaji una faida nyingi zikiwamo kukuza mitaji nchini, ajira, ongezeko la mapato na kukuza uchumi kwa ujumla.

Juhudi za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati haziwezi kufanikiwa, ikiwa nishati ya umeme wa uhakika itakosekana.

Kutokana na ukweli huu, Serikali ya Awamu ya Tano ilipokuja na mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere uliojulikana awali kama 'Stiegler's Gorge' katika eneo la Mto Rufiji, katikati ya mikoa ya Pwani na Morogoro, unalenga kuzalisha megawati 2115 za umeme.

Inatarajiwa, mradi utatoa nafasi ya kukidhi mahitaji ya nishati ya umeme viwandani na majumbani.

Megawati 2115 ni umeme mwingi. Hivyo, kukamilika kwa mradi kutavihakikishia viwanda vyetu umeme wa gharama nafuu.

Viwanda vikipata umeme wa uhakika na gharama nafuu, maana yake utasababisha bidhaa zinazozalishwa kuuzwa kwa bei nafuu na wananchi kumudu kuzinunua. Maana yake maisha yataboreka kila kona.

Kukatika umeme kila mara kumekuwa kikwazo cha uzalishaji nchini. Mradi wa Julius Nyerere, unatarajiwa kuwa tiba ya kukatika ovyo umeme.

Wamiliki na wawekezaji wa viwanda wanapotumia umeme mbadala kama jenereta katika uzalishaji bidhaa, huingia katika hasara kutokana na kutumia fedha nyingi kununua mafuta ya kuendeshea jenereta. Mambo kama hayo yanaongeza bei ya bidhaa zao, kero inayotarajiwa kutibiwa na mradi wa Julius Nyerere.

Wawekezaji wa viwanda waliohofu changamoto ya nishati ya umeme, watakuwa wamejibiwa. Badala yale watavutiwa kuwekeza nchini.

Muda wa uzalidhaji urakiwa ni saa 24. Hakutakuwapo sababu ya viwanda vyetu kufanya kazi nusu siku, huku kukiwapo umeme wa uhakika.

Wamiliki wa viwanda watalazimia kuongeza idadi ya wafanyakazi wakidhi mahitaji yao ya kazi masaa 24. Wakulima wataongeza uzalishaji, ili kulisha mahitaji ya viwanda kwa kutoa malighafi muhimu zinazohitajika katika uzalishaji.

Vilevile, serikali itapata mapato kupitia kodi zitakazolipwa na wamiliki wa viwanda na wafanyakazi wake. Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco), itafikia hatua ya kuuza nishati hata nchi za jirani.

Fedha za kigeni zitapatikana na kutumika katika ujenzi wa viwanda vyingine, zitasaidia kuinua sekta nyingine muhimu kama vile kilimo, miundombinu, elimu, afya, maji, uvuvi na ufugaji ambazo ni sekta muhimu katika kuendeleza maendeleo ya viwanda hapa nchini.

Muhimu ni mkandarasi wa mradi huo, kusimamiwa kikamilifu kuongeza kasi ya ujenzi ili ukamilike kwa wakati na nchi ianze kushuhusdia manufaa, hasa katika sekta ya viwanda. Hakika Mradi wa Umeme Julius Nyerere ni tiba mbadala wa mahitaji ya nishati ya umeme kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii pia. Tafakari.

# Daladala zidhibitiwe usiku

**Mhariri,**

*MARA nyingi katika mizunguko ya maisha ya kila siku, jijini Dar es Salaam na nje ya hapo, huduma za daladala ndio zinazotoa majibu yetu tukasogea kati ya eneo moja na jingine.*

*Kuzunguka huko kuna maana kubwa ya uhai wetu kiuchumi. Katika hilo, msaada kuwezesha mihangaiko hiyo jijini ni kuwapo huduma bora ya usafiri katika pande hizo.*

*Najua hilo si kwetu Dar es Salaam pekee, inaenda mbali hadi hata katika miji mingine mikubwa ya nchi yetu, kama vile Mwanza na Arusha.*

*Jambo linalonigusa ni tabia ninayoishuhudia kwa magari yetu, kila inapofika usiku hasa kuanzia baada ya saa mbili, askari wa usalama barabarani wakianza kutoweka, ndipo tunapoanza kushuhudia vituko barabarani.*

*Daladala zinaanza kubadili njia kinyume na zilikopangiwa, wakifuata watakapopaona kwa wakati huo kama kuna abiria wengi na ndipo wanaamua kufuata. Ni vitiko vitupu.*

*Sijui ndugu zetu wa Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), wanalifahamu hilo? Naomba wafanyie kazi, kwani nyakati za usiku wengi tunateswa sana na shida hiyo.*

*Pia nitumie nafasi hii kuwafahamisha ndugu zetu madereva, makondakta na wahudumu wa magari wabadilike, badala ya kila mara muda mwingi kuwa katika msuguano na mamlaka za usimamizi za kiserikali, kama vile polisi na Sumatra.*

*Naziomba mamlaka hizo kutumia muda huo kutoa ruksa kwa baadhi ya hata magari yanayoenda nje ya mji kutoka Dar es Salam, kama vile Kibiti, Kibaha, Mlandizi na Bagamoyo, ziruhusiwe kutoa huduma muda huo wa usiku.*


**Mantengine Juma,**
**Kibamba CCM, Dar es Salaam.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Sheria inapokuwa mtihani kwa vijana kupima VVU

**Na Joseph Mwendapole**




KWA mujibu wa takwimu za mwaka 2017 takribani watu 81,000 wanapata maambukizi mapya ya VVU kila mwaka.

Hii ina maana kwamba takribani watu 222 huambukizwa maambukizi mapya kila siku. Tabaka la watu wanaotumia dawa za kulevya, watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja, watu wanaojihusisha na biashara ya ngono, vijana na wanawake wakionekana kuelemewa zaidi na maambukizi mapya.

Zaidi ya hayo, vijana wako katika hatari kubwa ya maambukizi, takribani asilimia 43 ya maambukizi mapya ya VVU ya mwaka 2017 yanakadiriwa kuwa katika tabaka la vijana na watu wenye umri mdogo.

Hii inalingana na maambukizi karibu 34,815 mapya ya VVU, kwa hivyo vijana wapatao 96 wanaambukizwa VVU kila siku.

VVU na Ukimwi ni janga ambalo bado linatisha duniani kwa kuendelea kupoteza nguvu kazi. Tanzania si nchi ambayo imetengwa na dunia bali ni miongoni mwa nchi ambazo hupoteza mamilioni ya nguvu kazi kwa sababu ya janga hili la VVU na Ukimwi kila mwaka.

Licha ya jitihada za serikali katika kupunguza maambukizi kwa watu kupima, kujua afya zao na kupata matibabu bado kumekuwa na maambukizi mapya.

Bunge lilipitisha Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU na Ukimwi mwaka 2008, ili kulinda haki za watu wanaoishi na VVU na waathirika.

Katika kifungu cha 15 (2) bado hakimtambui mtu mwenye umri chini ya miaka 18 kama anaweza kupata huduma za kupima na kupata ushauri juu ya VVU na Ukimwi.

Kwa mujibu wa kifungu hicho yeyote ambaye hatokuwa na uwezo wa kuelewa matokeo au mtu mwenye umri chini ya miaka 18 hawezi kupima VVU na Ukimwi kwa hiyari yake mpaka awe na ruhusa ya maandishi kutoka kwa mzazi au mlezi.

Kwa mujibu wa takwimu za sasa zinaonyesha kuwa kusini mwa Jangwa la Sahara watoto na vijana wanaanza kujamiiana wakiwa na wastani wa umri wa miaka 13.

Tanzania ni nchi ambayo takribani theluthi moja ya watu wake ni vijana wenye umri kuanzia miaka 10-24 umri ambao vijana na wototo wengi wanabalehe na kuanza matamanio ya kingono.

Hivyo basi kutokana na sababu hizo sheria hii inaleta kikwazo kwa vijana wengi kupata huduma rafiki za kupima na kupata ushauri juu ya VVU na Ukimwi kwa hiyari yao bila ruhusa ya mzazi au mlezi.

Mpaka mwaka 2016 takribani asilimia 4.7 ya watoto na vijana kati ya umri wa miaka 10-19 walikuwa wanaishi na VVU ni kwa mujibu wa The World's Youth: 2013 Data Sheet.

Hii ni dalili kwamba watoto na vijana wa chini ya umri wa miaka 18 wanajihusisha na ngono. Sheria hii ikiendelea kubaki hivyo ni wazi watoto na vijana wanaotaka kupata huduma juu ya upimaji na ushauri juu ya VVU na Ukimwi watashindwa kufikia huduma hiyo.

Licha ya kuwa na sheria hii tumeona watoto na vijana wakipimwa VVU katika matamasha mbalimbali bila kuwa na ruhusa za maandishi kutoka kwa wazazi au walezi.

Katika dira ya kuwa na taifa bila Ukimwi, serikali imeridhia malengo ya UNAIDS ya 90-90-90 yenye lengo la kusaidia kupunguza maambukizi ya VVU na Ukimwi kwa kuhakikisha kwamba asilimia 90 ya watu wote wanaoishi na VVU kutambua hali zao za VVU.

Asilimia 90 ya watu wenye VVU kuanza kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV), na asilimia 90 ya wote walioanza ARV kupunguza kiwango cha VVU mwilini.

Hivyo basi sheria hiyo ambayo haimruhusu kijana wa umri chini ya miaka 18 kupima VVU na kupata huduma kwa ridhaa yake bado itakuwa ni kikwazo cha kufikia dira ya serikali ya 90-90-90.

Vikwazo vya upatikanaji wa huduma kwa vijana ni changamoto Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zina uhaba wa madaktari hasa katika maeneo ya vijijini ambapo vijana wengi hawana uelewa juu ya masuala ya VVU na Ukimwi.

Na hata hivyo takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 40 ya madaktari wanafanya kazi katika sekta binafsi na si sekta ya umma, hivyo kusababisha vijana wengi kukosa huduma bure za upimaji VVU, ushauri au kuanza matibabu kwa wakati ni kwa mujibu wa Global Aids Response Country Progress Report 2014.

Pia sheria ya kupambana na kudhibiti Ukimwi ya mwaka 2008 ni kikwazo kwa vijana ambao wako chini ya umri wa miaka 18 ambao tayari wanajihusisha na vitendo vya ngono inazuia kupata huduma ya upimaji na kupata ushauri kwa hiyari yao.

**KABWELA NA FADHIL MOHAMMED**



## HABARI KITAIFA

# Ripoti waliotelekeza watoto yaiva

INATOKA UK 2

wazazi wao. Zaidi ya 17,000 walijitokeza.

Katika mkutano wake wa jana na waandishi wa habari, Makonda alisema kupitia malalamiko waliyotoa wajane hao, walibaini kuna upungufu katika Sheria ya Mirathi ya Mwaka 1865 iliyorithiwa kutoka India na Sheria ya Mirathi ya Kimila, Tamko la Kimila la Tangazo la Serikali Na. 436 la Mwaka 1963.

Alisema sheria nyingine ni ya mirathi ya kidini ya Kiislam ambayo pia alidai kuna upungufu kwa kuwa haimtambui mke kama mrithi wa mali za mume, bali sehemu ya mali za mume.

Makonda pia alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kifungu cha 114, inatamka wazi kuwa mume na mke watakapoachana kisheria, watagawana michumo waliyopata kipindi cha ndoa kwa usawa.

"Kifungu hiki kina upungufu kwani kinamlinda na kumpa haki mwanamke pale anapoachana na mwezi wake tu na si pale mwenzi wake anapofariki dunia bila kuacha wosia," Makonda alisema.

Aliongeza kuwa katika sheria hiyo iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, kifungu cha 33 kinaonyesha upungufu kwa kuwa kinatamka kuwa pale tu mwanamume anapofariki, mke anaenda kuomba usimamizi wa mirathi, lakini mwanamume haendi kuomba usimamizi wa mirathi bali maombi ya mirathi, jambo linaloonyesha wazi kuwa mali ni za mume na siyo kwamba zimechumwa na wote wawili wakati wa ndoa.

"Hii inamkandamiza mwanamke anaonekana ni kama sehemu ya mali za mwanaume. Vilevile, kifungu hiki kinaweka mwanya kwa mtu yeyote yule kusimamia mirathi pasipo kutoa kipaumbele kwa mjane aliyeachwa.

"Ni vyema kifungu hiki kikaboreshwa kumpa kipaumbele mjane katika kusimamia mirathi," Makonda alisema.

Alisema upungufu mwingine upo kwenye Sheria ya Mirathi ya Kimila ya Mwaka 1963 ambayo alidai wamebaini ina vifungu vinavyowanyima haki za msingi kina mama wajane kinyume cha katiba ya nchi.

Makonda alisema kifungu cha 36(1) cha sheria hiyo kinatoa tafsiri kwamba anayetakiwa kuwa msimamizi wa mirathi ni mtoto chini ya miaka 18 na mlezi wake anaweza kusimamia mirathi hiyo kwa niaba ya mtoto, lakini wasimamizi hutumia vibaya mali kwa mgongo wa kifungu hicho kujinufaisha.

Alisema mapendekezo yaliyotolewa na jopo la wanasheria walioshiriki mkutano huo, kama yakipitishwa yatasaidia kuondoa mgongano huo na kuwaondolea adha wajane.

Kampeni ya kusaidia wanawake na watoto waliotelekezwa ilianza Aprili mwaka jana, watoto 2,971 wakipatiwa bima za afya kwa ajili ya matibabu mwaka mzima, wanawake 7,000 walisaidiwa kupata msaada wa kisheria na wanaume 2009 walikubali kulea familia zao.

Wanawake 100 walipatiwa msaada wa mawakili kwa ajili ya kusimamia kesi zao mahakamani baada ya kushindikana kumalizika ngazi za chini.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, akizungumza katika mkutano wa tano wa sayansi juu ya mazingira endelevu wenye mada isemayo 'binadamu na utunzaji wa viumbe hai' jijini Arusha jana. Mkutano huo wa siku tatu umeratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamzi wa Mazingira (NEMC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama ya Mafisadi yaelezwa waziri alivyodhamini Dola 500,000

INATOKA UK. 2

Alidai muda wa mkopo huo ulikuwa wa mwaka mmoja na kwamba riba yake ni asilimia 30.

Alidai katika fomu ya kuomba mkopo ya kampuni hiyo iliambatanishwa na ripoti ya tathmini ya nyumba ya Majogo iliyopo Msasani Peninsula, wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, yenye thamani ya Sh. 1,580,000,000.

Shahidi huyo alidai Dola za Marekani 375,750 ziliingizwa kwenye akaunti ya Majogo ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Aliendelea kudai kuwa katika fomu hiyo hakukuonyesha taarifa yoyote kama mkopo huo ulilipwa au la.

Akiendelea kuchambua fomu za mikopo iliyotolewa na kampuni hiyo, shahidi huyo alidai Desemba 11, 2013 Valentine Rutakyamirwa, alikopa Sh. milioni 30 kwa kampuni ya Superior Financing Solution na masharti ya mkopo huo ni kurejesha ndani ya mwezi mmoja na riba ya asilimia 30.

Mwakababu alidai kampuni hiyo ilitoa mkopo kwa Abdul Tuli, Septemba 27, 2012 wa Sh. milioni 17.5 kwa makubaliano ya kulipa kwa siku 45 kwa riba ya asilimia 30.

Alidai fomu hiyo iliambatanishwa na nyaraka zinazohusu kupunguza riba ya Sh. milioni moja na nakala ya Kitambulisho cha Taifa.

Pia alidai Agosti 4, 2014, James Masanja alikopa Sh. milioni 3.3 kwa kampuni hiyo na muda wa mkopo ulikuwa ni miezi miwili na riba ni asilimia 30.

"Katika fomu hii kumeambatanishwa nyaraka ya uthibitisho ya Kampuni ya Superior Financing Solution ya mauzo ya gari aina ya Noah na mnunuzi wa gari hilo ni Moshi Kembo kwa Sh. milioni nane Desemba 12, 2014. Pia kuna nyaraka inayohusu ukaguzi wa gari hilo ambaye mmiliki wake ni James Masanja," alidai Mwakababu.

Shahidi huyo alidai kampuni hiyo ilitoa mkopo kwa Joha Kilabuka wa Sh. milioni 5.5, Julai 5, 2013 kwa riba ya asilimia 30 na kueleza kwamba amepokea dhahabu ambayo aliweka kama dhamana ikiwa salama.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kula njama, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo, kushindwa kulipa kodi na utakatishaji fedha.

Inadaiwa kati ya Machi 2, 2010 na Aprili 26, 2016 katika maeneo tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa hao walikula njama kwa kugushi, kukwepa kulipa kodi na kutakatisha.

Inadaiwa kati ya Machi 4,2011 na Aprili 13,2016 katika maeneo tofauti ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, wakiwa mmiliki na mkurugenzi wa kampuni ya Superior Financing Solution Limited, walijihusisha na muamala wa kiasi cha Sh. 2,967,959,554 wakijua fedha hizo zinatokana na zao la makosa tangulizi.

Pia wanadaiwa kuisababishia serikali hususan Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. 2,967,959,554.

# Wazuiwa kujenga madarasa kwa kuhofiwa Freemason

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Bubale Kata ya Masengwa, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, wamedaiwa kuwakataza wasomi kujenga madarasa ya shule ya msingi kijijini humo, wakidai kuwa ni wafuasi wa Freemason.

Baadhi ya wasomi hao ambao walisoma kwenye shule hiyo na wazawa wa kijiji hicho walijitokeza kujenga madarasa 16 ili kuondoa upungufu wa madarasa, lakini wamegomewa wakidaiwa kuwa ni wafuasi wa kikundi hicho.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Eliakimu Mathew, alieleza hofu hiyo kutoka kwa wananchi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Alisema kwenye shule hiyo kuna upungufu wa madarasa 16 na yaliyopo ni tisa, huku uhitaji ukiwa ni madarasa 25, lakini kuna wasomi walijitokeza kujenga madarasa yote 16 wananchi wakawagomea kuwa ni Freemason.

"Mkuu wa wilaya hapa kwenye shule yetu kuna changamoto ya upungufu wa madarasa na matundu ya vyoo, lakini tunakabiliwa na tatizo la ushirikina na kukwamisha utatuzi wa changamoto hizi," alisema Mathew.

"Hivi karibuni kuna wasomi ambao ni wazawa wa kijiji hiki na walisoma kwenye shule hii, walikuja hapa shuleni kwa ajili ya kutatua upungufu, lakini wananchi walikataa wakidai hao wamejiunga Freemason na wakaondoka," alidai.

Vile vile, alisema mwaka 2014 kuna msomi mwingine alijitokeza kuchangia mifuko 10 ya saruji, wananchi waligoma pia kuwa ni Freemason na hatimaye kuzuia watoto wao kwenda shule kwa madai watachukuliwa kimazingara.

Nao baadhi ya wananchi akiwamo Kulea Kwilasa, walikiri kuwapo na suala la ushirikina kwa madai vijana hao utajiri wao wameupata kwa njia ya Freemason.

# Afrika yataka rasilimali zake zinufaishe watu wake

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI za Afrika ikiwamo Tanzania zimesema wakati umefika kwa nchi zilizoendelea kulisaidia bara hilo kujitegemea kwa kuliwezesha kutumia rasilimali zake yenyewe kwa maendeleo badala ya kulifanya eneo la kupata malighafi ya kuhudumia viwanda za nchi zilizoendelea.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema hayo baada ya kushiriki mkutano wa mawaziri wa maandalizi ya Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD 7), uliofanyika jijini Yokohama, Japan.

Alisema mkutano huo umesisitiza umuhimu wa uwapo wa miundombinu ambayo inaunganisha nchi za kiafrika ili kuliwezesha Bara la Afrika kuwa na miundombinu ya usafirishaji imara yenye kuleta tija.

Vilevile alisema mkutano huo umeazimia nchi zilizoendelea kuongeza fedha zaidi kwa ajili ya kutoa huduma za kijamii hususani katika nyanja za afya kupambana na malaria, kifua kikuu na Ukimwi na Afrika kuwajibika kuchukua hatua zote za kuhakikisha uwapo wa utawala bora, usalama na amani.

Akifungungua mkutano huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Japan, Kono Taro, amezipongeza nchi za Afrika kwa kupiga hatua katika maendeleo kupitia ushirikiano na nchi hiyo na kwamba itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na nchi hizo ili kuziwezesha kufikia malengo ikiwamo mapinduzi ya viwanda.

Alisema ushirikiano kati ya Afrika na Japan kupitia mpango wa TICAD umeendelea kuimarika tangu kuanzishwa kwa mpango huo mwaka 1993 na matarajio yake mkutano wa saba utakuwa wa tija zaidi kwa pande hizo mbili.

"Nawakaribisha mawaziri wenzangu Yokohama na maandalizi ya mkutano wa saba wa kimataifa wa Tokyo kuhusu maendeleo ya Afrika. Jukumu letu ni kupitia na kupitisha rasimu ya Azimio la Yokohama na mpango kazi wake ili hatimaye litunufaishe sote pale litakapopitishwa na wakuu wa nchi," alisema Taro.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri ambaye pia ni Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano huo, Sameh Shoukry, aliipongeza Japan kwa kuendelea kuandaa mikutano hiyo ambayo ina nia ya kuifikisha Afrika katika mapinduzi ya viwanda na kuondokana na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa ajira kwa vijana na nyingine nyingi.

Kwa upande wake, Naibu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ambao ni miongoni mwa waandaaji wenza wa Mkutano wa Saba wa TICAD, Kwesi Quartey, alisema mkutano huo unafanyika wakati Umoja wa Afrika unaendelea kutekeleza agenda 2063 inayolenga kuziwezesha nchi za Afrika kufikia maendeleo ya hali ya juu kwenye sekta mbalimbali zikiwamo afya, elimu, teknolojia na miundombinu.



Ombaomba akiomba pesa kwa abiria waliopo kwenye gari katika Barabara ya Uhuru, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI.**

# Hukumu baba aliyebaka mwanawe Septemba 23

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KESI inayomkabili baba mwenye umri wa miaka 47, anayedaiwa kumbaka mwanawe wa kumzaa, mkaazi wa Wambaa Wilaya ya Mkoani Pemba itatolewa uamuzi Septemba 23, mwaka huu, katika Mahakama ya Mkoa Chakechake.

Uamuzi huo utatolewa baada ya kuwapo mabishano kati ya mwendesha mashtaka wa Jamhuri kutaka apewe muda wa kuwasilisha mashahidi na wakili wa mtuhumiwa anayetaka kesi hiyo ifutwe kutokana na kukaa miezi sita, bila kusikilizwa mashahidi.

Wakili wa mshtakiwa, Saleh Said Mohamed, alidai shauri hilo ni la muda mrefu halijasikilizwa mashahidi na kuiomba mahakama kulifuta.

"Mheshimiwa hakimu, mahakama yako imeshatoa nafasi mara 10 ambazo zinamtaka mwendesha mashtaka awalete mashahidi hapa mahakamani, lakini ameshindwa, hivyo naiomba mahakama yako kuliondosha shauri hili," alidai wakili huyo.

Alidai shauri hilo halijasikilizwa na mashahidi, ingawa upande wa washtaka haujaeleza sababu za msingi za kukosekana kwa mashahidi hao. "Hakuna sababu za msingi walizotoa upande wa mashtaka na wameshapewa nafasi kadhaa za kuwasilisha mashahidi hapa mahakamani, iwapo watapewa nafasi nyingine itakuwa ni kumkandamiza mshtakiwa," alidai wakili huyo.

Mwendesha mashtaka, Seif Mohamed Khamis alidai shauri hilo lipo kwa ajili ya kusikilizwa ingawa hawajapokea mashahidi na kuiomba mahakama kumpa muda zaidi ili kuwapeleka mashahidi.

"Mheshimiwa hakimu, shauri hili lipo kwa ajili ya kusikilizwa, lakini hatujapokea mashahidi, hivyo naiomba mahakama yako tukufu kuipangia tarehe nyingine ili kuleta mashahidi," alidai.

Alidai zaidi kuwa aliyoyasema wakili ni matakwa yake binafsi na sio ya kisheria na kuiomba mahakama kufuata sheria ili kutenda haki.

Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Chakechake, Luciano Makoye Nyengo, baada ya kusikiliza mabishano ya pande mbili hizo, alisema kuwa atatoa uamuzi Septemba 23, mwaka huu.

Alisema tarehe hiyo, ndio ambayo Mahakama itaamua kuwa iendelee na shauri au kuliondoa mahakamani hapo.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Januari 1, mwaka 2019 saa 3:00 usiku, ambapo alimwingilia mwanawe wa kumzaa mwenye miaka 23.

Kufanya hivyo ni kinyume na sheria, kifungu cha 143 (1) (2) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

# NEC yatakiwa nukta nundu kwa wagombea

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mkoani Shinyanga, limeitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuweka alama ya nukta nundu kwenye majina ya wagombea ili wapate fursa ya kuwapigia kura viongozi wanaowataka.

Walisema watu wenye ulemavu hasa wasioona wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa wakati wa kupiga kura kuwachagua viongozi, lakini watu ambao wamekuwa wakienda nao kuwasaidia kwenye upigaji kura, wakati mwingine wamekuwa wakiwapigia kura kwa kuwachagulia viongozi wasiowataka.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Shivyawata, mkoani Shinyanga, Richard Mpongo, wakati akizungumza na Nipashe juu ya changamoto ambazo wanakabiliana nazo watu hao kipindi cha uchaguzi.

Aliipongeza serikali kwa kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu wakati wa kupiga kura, lakini changamoto kubwa ambayo huwa wanakabiliana nayo hasa watu wenye ulemavu wa macho ni kukosa imani na watu ambao huwasindikiza kuwasaidia kupiga kura kwa kuonyeshwa kumchagua mgombea ambaye hamuhitaji.

# Maofisa Uhamiaji wasisitizwa maadili

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Kagera imewataka maofisa 11kutoka wilaya saba za mkoa huo, kuzingatia kanuni, sheria na weledi wa maadili katika kuwatumikia wananchi kwenye maeneo ya kazi waliyopangiwa.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Idara Uhamiaji mkoani Kagera, Christopha Buteng'e, baada ya kuwavua vyeo na kuvisha vipya maofisa na wakaguzi wa Uhamiaji mkoani humo, kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza.

Alisema serikali imelenga kupata matokeo chanya juu ya shughuli zinazohusiana na masuala yanayohusu uhamiaji na kulifanya taifa kusonga mbele.

Hata hivyo alisema ufanikishaji wa suala hilo uliangalia zaidi utendaji wa kazi na weledi pamoja na jitihada katika ofisi kuanzia wilayani hadi vituo vyao kiutendaji.

"Nawasihi tu fanyeni kazi msije mkaona wenzenu leo mpandishwa vyeo pamoja na wengine kubakia palepale, tunaangalia ufanisi wa kazi na weledi kazini," alisisitiza Buteng'e.

Mrakibu wa Uhamiaji Wilaya ya Muleba, Benjamin Mwakasyege, alisema nafasi hiyo itaongeza chachu ya utendaji kazi katika maendeleo ya utambuzi raia wa kigeni wanaongia nchini bila kufuata taratibu.

# Stendi ya kisasa kujengwa kwa bil. 2/-

**Na Hamisi Nasiri,** NANYUMBU

KITUO cha mabasi cha kisasa cha Mangaka wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara kitaanza kujengwa na ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 2.1.

Inaelezwa kuwa kituo hicho kinatarajiwa kuwa sehemu muhimu katika kuongeza mapato ya halmashauri.

Aliyebainisha hayo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Hamisi Dambaya, alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa stendi hiyo mpya ya kisasa.

Alisema serikali imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati, na kwamba kituo hicho ni cha kisasa katika mkoa wa Mtwara.

"Kituo cha mabasi cha Mangaka wilayani Nanyumbu kinatarajiwa kuwa moja ya kituo bora mkoani Mtwara na muhimu katika kuongeza mapato ya halmashauri kwa kweli tunampongeza Rais John Magufuli kwa kupatia fedha hizi Sh. bilioni 2.1 kujenga stendi hii ya mabasi," alisema Dambaya.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kutoka katika hali ya utegemezi wa fedha za Serikali Kuu na kuanza kujitegemea yenyewe kwa vile itakuwa ikipata mapato ya kutosha yanayotokana na kituo hicho.

Dambaya alisema pia fedha zitakazokuwa zikipatikana kutoka kwenye mapato ya stendi hiyo zitasaidia kupunguza ya baadhi ya changamoto ambazo halmashauri inakabiliana nayo kwa sasa.

Aidha, alisema mradi huo wa kimkakati ambao umeanza kutekelezwa hivi karibuni, unatarajia kukamilika Februari 2020, na kwamba ujenzi unaendelea vizuri na ni wazi utakamilika kama serikali ilivyokusudia.

Dambaya alisema katika mradi huo pia kutajengwa na mabanda ya maduka, ambapo wafanyabiashara watapata fursa ya kuendesha biashara zao na kufanya shughuli za usafirishaji katika mazingira bora.

Alisema katika kuifanya stendi hiyo kuwa na mwonekano wa kisasa, pia kutajengwa jengo la hoteli pamoja na jengo la baa ili kuwawezesha wasafiri kupata huduma ya chakula na vinywaji papo hapo wakati wakisubiri kusafiri.

Majengo mengine ambayo yatajengwa katika mradi huo ni jengo la mashine ya kibenki ya kutolea fedha (ATM) pamoja na jengo la duka la kuhifadhia dawa.




Kijiko kikiondoa mchanga uliokuwa umeziba kwenye mitaro ya maji ya mvua katika eneo la Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# SMZ yasaka mashamba yake 400

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya mashamba 1,951 ya Serikali ya Zanzibar yameshafanyiwa uhakiki katika Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba, ambapo mashamba yasiopungua 400 hayajulikani yalipo.

Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Rashid Hadid Rashid, alisema serikali inatafuta mashamba yake ambayo ni ekari tatu ambazo walipewa wananchi baada ya Mapinduzi kwa ajili ya kilimo.

Alisema wilaya hiyo inaendelea kuyatafuta na kuyahakiki mashamba ya serikali ambayo wameshayafanyia uhakiki mashamba 1,915, ingawa mashamba yasiopungua 400 hayajajulikana yalipo.

"Pamoja na kuwa tunaendelea kuyahakiki mashamba yote ya wilaya hii, lakini bado kuna mashamba mengi wananchi wameyaficha, hatuyajui yalipo, ila tunaedelea kuyatafuta," alisema.

Alieleza kumejitokeza baadhi ya watu kuuza mashamba ya serikali kiholela, jambo ambalo ni kosa na kuwataka wananchi wawe makini wanapouziwa maeneo ya ardhi na wafuate utaratibu.

"Ni marufuku kuuza, kurithi ama kuyafanya makazi mashamba ya serikali labda kwa kufuata utaratibu unaotakiwa, mashamba haya walikuwa wamepewa wananchi kwa ajili ya kilimo, lakini sasa wameyabadilisha matumizi kwa kuyajenga makazi, jambo ambalo ni kinyume cha utaratibu," alieleza.

Alieleza serikali haina nia ya kuwanyang'anya wananchi mashamba hayo, bali wanataka kuyatambua, ili kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Aliwashauri wananchi wenye mashamba hayo kuyarudisha ili yatumike kwa shughuli za kilimo na atakayeficha hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Serikali Wilaya ya Chakechake inaendelea na mchakato wa kuyatafuta mashamba hayo na kuyahakiki ili yarejee katika shughuli za kilimo kama ilivyokusudiwa.

# Watumishi watakiwa kumuenzi Magufuli

**Na TIganya Vincent,** TABORA

WATUMISHI wa umma wametakiwa kulipa fadhila kwa Rais John Magufuli kwa kufanyakazi kwa kuzingatia taratibu na sheria wakati wa utekelezaji wa miradi wanayokuwa wamepewa kusimamia.

Kauli hiyo ilitolewa na Kiongozi wa Taifa wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Mzee Mkongea Ali, kwenye Halmashauri ya Mji Nzega mkoani Tabora baada ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi ukiwamo ujenzi wa Hospitali za Wilaya, vituo vya afya, usambazaji wa maji na barabara, hivyo ni vema miradi hiyo ilingane na thamani ya fedha zilizotolewa.

Ali alisema hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki sawa kama yalivyo malengo ya Rais Magufuli kuhakikisha Watanzania wote wanafaidi rasilimali za nchi kwa kupata huduma zote muhimu ikiwamo elimu na afya.

Kiongozi aliweka mawe ya msingi miradi ya maendeleo minne ikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.

# Uwazi wahimizwa katika miradi afya

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Misana Kwangula, amewaagiza watendaji wa halmashauri hiyo, kuhakikisha kunakuwa na uwazi katika kutekeleza miradi ya afya ili kuwapa fursa wananchi kuelewa thamani ya fedha na nia ya serikali katika kuboresha sekta hiyo.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua kikao cha uzinduzi wa mradi wa kuongeza ufahamu kwa wananchi juu ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika sekta ya afya, unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Life change Rukwa Development Organization(LCRDO) utakao tekelezwa katika kata tatu na kufikia vijiji tisa kwa muda wa miezi minane wilayani humo.

Alisema kuwa katika kutekeleza miradi hiyo uwazi ni suala la msingi kitendo kitakachosababisha wananchi kushiriki hatua kwa hatua na kuona miradi hiyo ni mali yao, hivyo aliwasihi kushirikiana na kamati za afya za vitongoji, vijiji, kata na wilaya.

Alisema serikali inatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya hiyo na mara nyingi wananchi wamekuwa wakihitajika kuchangia nguvu kazi katika miradi hiyo, hivyo ni vizuri pia wakawa wanaelewa hata gharama zinazotumika katika ujenzi huo.

# Tasaf yakarabati barabara kilomita 14.5

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) Wilaya ya Longido mkoani Arusha, umekarabati kilomita 14.5 za barabara katika kata za Olmolog na Kamwanga.

Ofisa Ufuatiliaji wa Tasaf Wilaya ya Longido, Majuto Kawambwa, alisema juzi kuwa miradi hiyo iliibuliwa na wananchi, hivyo wahusika wakubwa katika kutengeneza barabara hiyo ni wanufaika wa fedha za kaya duni.

"Wanaofanya kazi hii ya kufyeka na kusafisha barabara hizi ni walengwa na kazi hii wanafanya kwa saa nne kila siku na hulipwa kila mmoja Sh. 2,300, huku mikataba ya kukamilisha kazi hiyo ikiwa ndani ya miezi mitatu," alisema.

Ofisa huyo alisema katika kijiji cha Olmolog, wamekarabati kilomita 10 kwa thamani ya Sh. milioni 74.5 na kijiji cha Kitendeni kilichoko Kata ya Kamwanga kilomita 4.5 kwa Sh. milioni 64.2 ikiwa ni fedha za mradi na ufuatiliaji.

Alisema pamoja na mfuko huo kukarabati miundombinu ya barabara, pia umejenga bweni la wavulana katika Shule ya Sekondari ya Enduiment, lenye uwezo wa kulala watoto wanafunzi 48 kwa gharama ya Sh. milioni 71.7.

"Tutaweka vitanda 24 'dabo deka' katika bweni hili. Mradi huu unaitwa wa nguvu kazi, hivyo jamii ilichangia asilimia 10 kwa kutoa fedha na kwa kufanya kazi na ujenzi huu upo katika hatua za mwisho kukamilika," alisema Kawambwa.

Naishie Simon, mkazi na mlengwa wa Tasaf Kijiji cha Olmolog, alisema kupitia mfuko huo wa kusaidia kaya duni, wamejikwamua katika hali ya umaskini na kwa sasa wengi wao wanafanya biashara ndogo ndogo kupitia fedha za Tasaf.

"Hata huu mradi wa barabara tunaenda kufanya kazi kwa saa chache tunalipwa. Wameona watuwezeshe kwa namna mbalimbali, tunaishukuru serikali kwa kweli," alisema.

Alifafanua kuwa barabara hiyo inawasaidia kukutanisha vitongoji vyote ndani ya kata ya Olmolog pamoja na kufikia huduma za jamii kikiwamo kituo cha afya kilichoko katika kijiji cha Olmot na shule ya awali ya Engatani.

"Hii barabara itaokoa maisha ya mama na mtoto wakati wa kufuata huduma ya afya, kwa sasa kufika kituo cha afya Olmot, unapita njia hii bila usumbufu, ni barabara muhimu sana kwetu," alisema Naishie na kuongeza:

"Mfuko huu (Tasaf) wilayani hapa una walengwa 5,641 na unafanya kazi katika vijiji 27 kati ya 49 vilivyopo, huku kukiwa na kata 18 na tarafa nne zinazoiunda wilaya."



Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zuwena Omary, akizungumza na wadau wa madini wa eneo hilo juzi. **PICHA: GIFT THADEY.**

# Mhandisi aagizwa kuandaa andiko la maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Wizara ya Maji, Jumaa Aweso, amemwagiza Mhandisi wa Mkoa wa Arusha, Joseph Makaidi, kuandaa andiko na kuainisha maeneo yasiyo na maji katika Wilaya ya Arumeru.

Lengo la andiko hilo ni kuiwezesha kampuni ya Fraju Group Ltd inayokamilisha kazi ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya King'ori kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5.

Aweso alisema mkandarasi huyo amekuwa mfano wa kuigwa kwa kutekeleza mradi wake wa usambazaji maji katika kijiji cha King'ori unaotekelezwa chini ya programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

"Makandarasi wengi tunaopata katika wizara hii ni makanjanja kwani badala ya kufanya kazi wanayotakiwa kufanya, wanaleta ujanja ujanja tu na wananchi kuendelea kuteseka kwa kutopata maji. Huyu ameonyesha uzalendo acha ale mema ya nchi, andikeni andiko tumwongezee kazi," alisema.

Alisema mkandarasi huyo ametekeleza mradi huo kwa uaminifu na maji yaliyopo ni mengi mpaka yanapasua mabomba, hivyo lazima kumwongezea eneo la kusambaza maji hayo, badala ya kusambaza kijiji hicho pekee wakati wengine wanakosa maji.

Pia alimtaka Mhandisi Makaidi kuhakikisha anawafuatilia kwa karibu watendaji wake katika mkoa ili wasimwangushe na kumsababishia kupata shida na serikali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alimwomba Aweso ikiwezekana mkandarasi huyo aongezewe kata za kusambaza maji hayo badala ya kata moja ya King'ori kwa sababu maji yanayotoka eneo hilo la mradi ni mengi hadi yanapasua mabomba kutokana na kutumika katika eneo dogo.

"Mheshimiwa Naibu Waziri huyu mkandarasi ameshajenga miundombinu mingi, hivyo akiongezewa eneo la mradi kazi ndogo tu ya kuunganisha mabomba na maji kuanza kutoa sababu tangi la kuhifadhia maji ameshajenga na imara," alisema Alisema katika kata nyingi wilayani hapa kuna upungufu wa maji, hivyo itakuwa busara ya kumwongezea kazi mkandarasi mzalendo aliyetekeleza mradi wake kwa umakini.

# Polepole ataka uhakiki mipaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, ameiagiza ofisi ya maji bonde la kati kufanya uhakiki wa mipaka ya chanzo cha maji Qangded.

Lengo la kufanya uhakiki katika chanzo hicho kilichoko Kata ya Barai wilayani Karatu mkoani Arusha ni kuwekewa ulinzi na kuondoa adha ya maji kwa wananchi wa kata hiyo na ile ya Mang'ola.

Pia amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, kuimarisha ulinzi kwenye vyanzo vyote vya maji katika wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na kusimamia ujenzi wa ukuta katika chanzo cha Qangded kinachohudumia zaidi ya wananchi 36,000 ili kuzuia maji ya mvua yanayojaza mchanga kwenye chanzo hicho na kutishia kutoweka.

Polepole alitoa agizo hilo jana wilayani Karatu wakati wa ziara yake ya kikazi, iliyoenda sambamba na kukagua chanzo hicho cha maji ambacho pia kinatumika kwa ajili ya kilimo cha vitunguu katika kata hizo na kuuzwa nje ya nchi.

Alisema chanzo hicho cha Barai ni uhai wa wananchi wa kata hizo na kwamba uongozi wa bonde la kati unachukua fedha kutoka Juwamaboe, lakini haushiriki kikamilifu kutoa elimu juu na namna bora ya kudhibiti uharibifu wa chanzo hicho.

"Mkuu wa Wilaya wasiliana na ofisi ya bonde la maji la kati, ili wafike hapa kwa ajili ya kushirikiana na wataalamu wa halmashauri kupima na kuweka mipaka kwenye chanzo cha maji cha Qangded ili kisiendelee kuharibiwa na shughuli za binadamu, ikiwamo kukata miti ovyo pamoja na mifugo kwenda kunywa maji kwenye chanzo hicho," alisema.

Aidha, alimwagiza mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Karatu kuanza kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuchimba mtaro wenye urefu wa kilomita saba kutoka kwenye chanzo hicho kwa ajili ya kupeleka maji yote ya mvua kwenye Mto Barai.

Polepole ambaye alionyesha kukerwa na wataalamu wa halmashauri hiyo kushindwa kutimiza wajibu wao na kusababisha migogoro mikubwa ya maji, aliwataka kuanzia sasa waondoke ofisini na kwenda kwa wananchi kwa ajili ya kutoa elimu pamoja na kusimamia sheria.

# Mapya yaibuka kwenye mvutano mradi wa maji

Na Mwandishi Wetu, SIHA

ZIKIWA zimepita siku tatu, tangu wananchi wa Kijiji cha Miti Mirefu, Siha, mkoani Kilimanjaro, walalamikie mazao yao kukauka kwa kukosa maji kutokana na ujenzi wa mradi mpya wa maji kupelekwa Wilaya jirani ya Longido mkoani Arusha, mapya yameibuka baada ya wananchi hao kudai hawakushirikishwa katika mchakato mzima.

Jana, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, lilielezwa kuwa wakati wa mchakato wa kuanzishwa mradi huo hawakushirikishwa na hata halmashauri ya wilaya yao haikuhusishwa.

Diwani wa Miti Mirefu, Simon Shija, alisema ekari zaidi ya 300 za mazao mbalimbali ya biashara na chakula, zimekauka na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima kutokana na kukosa maji ya umwagiliaji.

Wakati Shija akisema hayo, Diwani wa Orkolili, Jonathan Nassari, alitaka waliohusika na uratibu wa mradi huo wakiwamo Bonde la Kati waandikiwe barua ili waweze kufika na kutatua mgogoro huo mapema kabla ya kutokea janga.

"Waje tukae nao kwa pamoja ili tuweke mambo sawa, kama hawatakuja ni bora haya maji kuliko yamwagike porini ni bora yabaki mtoni," alisema Nassari.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Godson Ngumuo, alisema hawakubaliani na utaratibu uliotumika hata kidogo na hawawezi kuacha watu wao wapate hasara zaidi ya hapo au kupata baa la njaa.

"Mkurugenzi nakuagiza, waandikie barua hawa watu (Bonde la Kati), waje tukae pamoja kwa sababu hawawezi kuja kwetu kuchukua maji bila kutushirikisha. Halafu maji hayo hayawafikii yote watu wa Longido, yanamwagika njiani kutokana na miundombinu ya bomba hilo kudaiwa kujengwa chini ya kiwango, na ndiyo maana tunaomba wataalamu wa wilaya hizi mbili wakutane kwa pamoja," alieleza Ngomuo.

Juzi, Kaimu Meneja wa Ofisi ndogo ya Maji ya Bonde la Kati mkoani Arusha, Dandu Joseph, alipoulizwa kuhusiana na malalamiko hayo ya wananchi wa Siha, alisema wanakusudia kwenda wilayani humo kuona na kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo la kupungua kwa maji ya umwagiliaji.

Bonde hilo la Kati, ndilo lenye jukumu la kisheria la kusimamia ugawaji wa maji hayo ya umwagiliaji.

"Ni kweli tumesikia kwamba kuna malalamiko ya wakulima katika Kijiji cha Miti Mirefu na vijiji vya jirani kwamba mashamba yao ya mazao mbalimbali yamekauka baada ya kukosa maji," alisema Dandu.

Baadhi ya wakulima wa Miti Mirefu, wanadai maji hayo yamepungua kutokana na kupelekwa mradi wa majisafi na salama kwa wananchi wa Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

"Kazi ya bonde hili ni kusimamia na kutatua migogoro inayotokea katika matumizi ya maji, kukusanya na kutunza takwimu za mitiririko na hali ya maji kwenye rasilimali za maji pamoja na kusimamia na kuratibu hifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji. Sasa kwa sababu tayari kuna malalamiko, tunaelekea huko kutafuta ufumbuzi wake," alisisitiza Dandu.



Wananchi wakichagua machungwa katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Chungwa moja liliuzwa kwa bei ya 50/- hadi 80/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

## Tarura yakiri changamoto

Na Godfrey Mushi, MOSHI

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, imekiri kuwa bado kuna uhitaji wa matengenezo makubwa ya barabara za majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo ambayo yanaunda halmashauri hiyo, ikilinganishwa na kiasi cha fedha kinachopatikana.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja wa Tarura, Wilaya ya Moshi, Fundi Sanifu Mwandamizi, Loishiye Mollel, halmashauri hiyo imetengewa Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake.

Alisema Wilaya ya Moshi, ina mtandao wa barabara wa zaidi ya kilomita 700 na kwamba hivi sasa baadhi ya barabara zinazotarajiwa kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe ni barabara ya Wami-Gomberi inayotarajiwa kutengenezwa kilomita nne na barabara ya Sangiti-Nganyeni inayofanyiwa matengenezo ya kawaida kwa umbali wa kilomita tatu.

"Tunategemea kuwa changamoto zote zilizotajwa na wananchi na kupigiwa kelele madiwani zitafanyiwa kazi kwa maeneo yote yaliyotengewa bajeti ndani ya mwaka huu wa fedha. Maeneo mengine ambayo bado kuna changamoto na hayamo kwenye bajeti, tutaendelea kushauriana ili kuhakikisha shughuli za kimaendeleo zinaendelea wakati tukiendelea kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya matengenezo yake," alisema Mollel.

Barabara nyingine inayojengwa kwa kiwango cha lami ni ya Getifonga/ Mabogini/ Kahe/ Chekereni ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli ya mwaka 2015. Barabara hiyo tayari imetengewa kiasi cha Sh. bilioni 22.

Kwa mujibu wa Tarura, sehemu ya utekelezwaji wa ahadi hiyo ya Rais Magufuli, ilipangwa kuanza katika bajeti mpya ya mwaka wa fedha ulioanza Julai mosi mwaka huu.

Aidha, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 674.52 ikiwamo ahadi ya Rais John Magufuli ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 20.

Kabla ya kutolewa taarifa hiyo inayoleta faraja zaidi kwa wananchi wa maeneo hayo, Diwani wa Kata ya Mabogini, Emanuel Mnzava, ilieleza kuwa katika sekta ya ujenzi ndani ya kata yake, ahadi ya Rais (Magufuli) ya kujenga barabara hiyo bado haijatekelezwa.

# Shirika Uingereza lafufua matumaini ya serikali

Na Godfrey Mushi, SAME

SHIRIKA la World Expedition Exchange la Uingereza, limefufua matumaini ya serikali katika Wilaya ya Same wa kukuza na kuvitangaza vivutio vyake vya utalii, baada ya kukubali kuja kuwekeza katika sekta hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema wafadhili hao ambao walitembelea Kijiji cha Goma, Kata ya Mshewa, wamekubali kuja kuwekeza katika fursa mbalimbali ikiwamo hoteli za kitalii na kampuni za kitalii.

Alisema kabla ya kuja rasmi, shirika hilo kwa sasa limeanza kugawa vitabu vya masomo ya Sayansi kwa Shule za Msingi na Sekondari za Kata ya Mshewa ili kuunga mkono juhudi za serikali katika utaoji wa elimu bora na yenye ushindani kimataifa.

"Hivyo vitabu vilivyoletwa na Shirika la World Expedition Exchange, ndivyo ambavyo vimewezesha kuanzishwa kwa maktaba hiyo katika kijiji hicho cha Goma. Wametoa maelekezo kwamba vitumiwe na wanafunzi wa Kata ya Mshewa ili kuongeza maarifa.

"Utalii wa asili, ndio ambao umelivutia hilo shirika na kuamua kuja kuwekeza hapa kwetu siku za usoni, lakini kimsingi tayari wamekubali pia kufadhili ujenzi wa maktaba wa kwanza ya utalii, hasa ukizingatia kuwa suala la kukuza utalii wa asili ni moja ya malengo yaliyopo kwenye mpango mkakati wa kukuza utalii wilayani Same."

Mkakati huo, unaelezwa umeanza kuvutia watalii wengi kutoka mataifa ya kigeni kutembelea vivutio vya asili, maporomoko ya maji, mapango, mashamba, mabwawa, misitu, milima na vingine.

Senyamule alitoa wito kwa wananchi kujifunza na kushiriki shughuli za utalii akisema, katika mpango mkakati wa utalii, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Msitu wa Chome wenye kilele cha Shengena, wilaya imepanga kuunganisha vivutio hivyo pamoja na vivutio vya utamaduni ili serikali na wananchi wote wafaidike na kukuza uchumi wa wilaya.

Mmoja wa wafanyabiashara aliyewaleta maofisa hao wa shirika hilo la Uingereza, Elly Kimbwereza, ameeleza mtazamo wake wa namna utalii wa asili unavyoweza kuunganishwa na shughuli za jamii na kuleta maendeleo ya haraka, kwani watalii wengine wameshashiriki kutengeneza barabara katika kijiji hicho.

ama
ALHAMISI AGOSTI 29, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



## Mtaalamu alivyochambua TGNP vs ngono kwa watoto

Ukurasa 17



Ukurasa 14

## Mfumuko wa volkano wagunduliwa



Ukurasa 18

## Kutoelewa afya ya udongo kunavyompa dhiki mkulima



### MASIKINI 'MAPAFU YA DUNIA'...

# Moto usiokwisha ndani ya msitu unaozalisha robo oksijeni duniani

Ukurasa 14

# Mfumuko wa volkano wagunduliwa

**SYDNEY,** Australia

DUNIANI kuna miamba na milima tofauti. Baadhi ni matokeo ya mifumuko ya udongo wa moto kutoka ardhini kutokana na volkano, ambao uliganda katika miaka mingi iliyopita.

Sasa kuna taarifa mpya ya kuibuka mengine, wanasayasi wavuvi kutoka nchini Australia, wameibuka na ushuhuda kuhusu mimba mpya ya volkano chini ya maji katika bahari ya Pacific.

Wanasayansi waliofuatilia wanasema, mwamba huo wenye upana wa kilomita za mraba 150, ikikadiriwa sawa na wastani wa viwanja vya soka 20,000. Huo ni ugunduzi wa mapema mwezi huu.

Kwa mujibu wa wataalamu wakirejea picha za satelaiti, ni kwamba udongo huo wa moto huenda ulifumuka Agosti mwaka huu na wavuvi wametahadharishwa kutopita karibu na eneo hilo, kwani hatari kutokea mfumuko zaidi wa udongo wa hewa ya moto, kupitia matundu yaliyopo.

Wataalamu wanaeleza kuwapo vinzigiti vya vipande vya miamba ya volkano ama vinavyoelea au vilivyoganda majini na kuibuka hasa jirani na kwenye maji ya kina kifupi.



Mvuvi wa Australia, Michael Hoult, akionyesha jiwe aliloliokota. **PICHA: MTANDAO.**

MAZINGIRA

MASIKINI 'MAPAFU YA DUNIA'...

# Moto usiokwisha ndani ya msitu unaozalisha robo oksijeni duniani

• Toka Januari hekta 74,000 zatoweka • Jeshi kazini; ndege zanyunyiza maji • Dunia katika taharuki ya hewa, joto



Moto ukiusambaratisha msitu wa Amazon. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

HADI wiki iliyopita hali haikuwa nzuri hata kidogo. Moto mkubwa ulishasamba katika msitu mkubwa wa Amazon, nchini Brazil, hata ikawa tishio la kidunia.

Lawama za kuungua msitu huo unaojulikana kama 'mapafu ya dunia' sasa anasukumiwa Rais Jair Bolsonaro, akidaiwa kuzembea athari za kimazingira, msitu huo unaosinga kuelekea janga zito litokanalo na moto.

Hilo ni janga la dunia kwa sababu ni msitu wenye mchango mkubwa wa kuilisha dunia na hewa ya oksijeni na kiwango cha sasa kinaelezwa hakijawahi kufikiwa.

Hivi sasa, asasi ya kimazingira inayoitwa; The National Institute for Space Research (INPE), inasema tangu kuanza mwaka huu hadi mwisho wa wiki iliyopita, moto umeathiri eneo la ekari 74,000 ambayo ni ongezeko la wastani asilimia 84 zaidi, kulinganishwa na mwaka jana.

> “Msimu wa nchi kavu unajenga mazingira katika matumizi na kusambaa kwa moto, lakini kuanzishwa moto ni kazi ya mwanadamu.

Pia, inatajwa kuwa rekodi kubwa inayovunja kiwango kama hicho cha juu zaidi mwaka 2016, ikichukua ekari 68,484.

Amazon ina sifa kubwa kwamba ni msitu wenye mchango mkubwa katika kudhibiti joto la dunia na kupumua hewa safi ya oksijeni ikichangia wastani wa asilimia 20 ya hewa duniani.

Nchini Brazil kunaelezwa ndiko kwenye asilimia 60 ya msitu wa Amazon, ambako kuna msitu hekta milioni 670. Wanasayansi wanalalama kuwa moto unaoendelea hivi sasa nchini Brazil, si wa kawaida katika historia ya janga hilo.

Wanamazingira wanamshutumu Rais Bolsonaro, kwamba shida kubwa inaangukia katika sera zake zinazoathiri mazingira, lakini kiongozi huyo amepinga vikali akidai takwimu zinazotolewa kuhusu moto huo ni potofu.

Rais huyo anasema kwamba hivi sasa anasubiri takwimu zijazo ambazo atazitumia kuzungumza ukweli wake. Hadi sasa, dunia imeshatingwa na hofu na mageuzi hayo.

Asasi ya INPE, inafafanua hilo katika mtazamo kwamba wakati ukame unaweza kuelezwa kuwa chanzo cha kuteketea misitu, lakini inasistiza hakuna kilichoenda kombo kuhusu hali ya hewa mwaka huu.

“Msimu wa nchi kavu unajenga mazingira katika matumizi na kusambaa kwa moto, lakini kuanzishwa moto ni kazi ya mwanadamu, ama kwa bahati mbaya au makusudi,” anasema mtafiti wa asasi hiyo, Alberto Setzer.

Wanasayansi wanataja baadhi ya shughuli za kibinadamu kuwa ni kilimo, uchimbaji madini na kuchimba maji, zote zikitajwa kujenga mazingira mabaya ya kuzua moto.

Nchini Brazil, kunaelezwa kumejengeka tabia ya wakulima kuanzisha moto kwa makusudi kufungia mianya na njia za wafugaji, ingawaje ni tendo linalokinzana na sheria katika suala la uhifadhi wa misitu.

Mfuko wa Mifugo Duniani, unakadiria kuwapo hatari ya robo ya msitu wa Amazon kutoweka ifikapo mwaka 2030, kama hakutakuwapo hatua za makusudi kukakabili athari ya kinachoendelea hivi sasa.

Kuna lawama zingine kwa Rais Bolsonaro na sera zake alizoingia nazo ofisini Januari mwaka huu, akinuia kugeuza baadhi ya maeneo ya msitu kuwa mahsusi kwa kilimo na uchimbaji, akidaiwa hajali kelele za kimataifa zinazodai kiwapo hifadhi ya mazingira hayo

**LAWAMA SERIKALINI**

Rais Bolsonaro katika sera zake, anasema katika ahadi zake anahimiza kurejesha uchumi wa nchi kutafuta mbadala wa matumzi ya Msitu Amazon, uwe na manufaa kiuchumi, kuliko kukumbatia mbiu za kimataifa kuhusu hifadhi na ulinzi wa mazingira.

Katika mikakati yake kuhudumia watu wa chini, anajinasibu amekuwa akifanya mageuzi makubwa kisheria kukidhi mahitaji yanayowalenga wakulima na wafugaji kupatiwa vipande vya ardhi ndani ya (msitu) Amazon, huku wanamazingira wakionekana kukerwa na uamuzi huo.

Mtaalamu wa hali ya hewa, Carlos Rittl, ana ufafanuzi: “Kwa kipindi cha miezi sita, (Rais) Bolsonaro na Waziri wa Mazingira wamejitoa kuharibu Usimamizi wa Mazingira ya Brazili na kuzidhoofisha bodi za usimamizi.”

Hivi karibuni, mkuu wa asasi ya utafiti wa mazingira ya INPE, alitoa takwimu kwamba mwezi Juni mwaka huu, msitu wa Amazon uliteketea kwa kiwango asilimia 88 zaidi, ikilinganishwa na kipindi kama hicho, mwaka jana.

MAZINGIRA

# Moto usiokwisha ndani ya msitu unaozalisha robo oksijeni duniani

Lakini Rais Bolsonaro, ambaye kitaaluma ni Kapteni Mstaafu wa Jeshi la nchi hiyo, katika majibu yake alijia juu takwimu za watafiti hao walio chini ya serikali yake akidai; "ni za uongo, zinazolenga kukwamisha biashara za Brazil."

Ni uamuzi uliofuatana na kutimuliwa kwa Mkurugenzi wa asasi hiyo ya INPE, Ricardo Galvao, akimtaja anahujumu hadhi ya taifa la Brazil.

**BRAZIL YASAIDIWA**

Katika kile kinachoonekana kuchukua sura ya kimataifa, baadhi ya nchi kama vile Norway na Ujerumani, sasa zimeanza kuikusanya fedha za kuisaidia Brazil, kukabili janga la misitu.

Pia, asasi ya kimazingira kimataifa iitwayo Greenpeace, inampa mwito rais huyo aitilie maana kwamba, miongoni mwa athari ni kuwapo mzigo mkubwa wa kiuchumi kwa nchi hiyo.

Hata hivyo, kiongozi huyo anaendekeza majibu 'mepesi' pingamizi kuwa moto unaoendelea ni wa kawaida sehemu tu wakulima wanaposafisha mashamba yao

Hivi karibuni, alizinyooshea asasi zisizo za kiserikali kwamba huenda ndio zikawa wahusika wakuu wa moto wanaoiingiza serikali katika lawama kubwa.

Ilipofika Jumamosi iliyopita, mbinu mpya uya kukabili moto ilitumika ambayo ni matumizi ya Jeshi la Ulinzi la Brazil, ambalo lilibebeshwa rasmi jukumu na serikali.

Mbinu kuu iliyotumika katika kazi hiyo ni askari wa nchi kavu wanaukabili moto ardhini, huku wakisaidiwa na wenzao wa vikosi vya anga wakinyunyiza maji.

Inaelezwa kuna jumla ya askari wasiopungua 44,000 wameingia kazini kukabili jukumu hilo la kuuzima moto, huko majimbo sita yakitajwa kuwa hatarini kukumbwa na moto, ambayo ni: Roraima, Rondonia, Tocantins, Para, Acre na Mato Grosso.

Waziri wa Ulinzi wa Brazil, Fernando Azevedo, anasema katika awamu ya kwanza ya operesheni hiyo yenye siku tano sasa inashughulikiwa na vikosi vya askari 700.

Akifafanua anasema, ndege zake anazozitaja aina ya C-130 Hercules ndizo zilizopangiwa kumimina maji msituni wa wastani wa lita 12,000 au sawa na galoni 3,170, katika eneo hilo lililofunikwa na utandu wa moshi.

Inaelezwa ni hatua ya rais kuzima kelele dhidi yake akionekana kuchukua hatua kuu kukabili janga hilo la moto wenu hatari kwa maslahi ya nchi yake.

Waziri Azevedo, anasema tayari Rais wa Marekani Donald Trump, alishawapa ofa ya kuwasaidia katika kupambana na janga hilo na hadi sasa wako katika mawasiliano kukamilisha utekelezaji wake.



Waokoaji wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Lengo ni kuuhifadhi msitu huu, kwakuwa sote tunauhitaji kwa sababu ni hazina ya usalama wa mazingira na hali ya hewa. Tunashukuru oksijeni inayotoa na shukrani kwa hewa ukaa (carbon dioxide) inayounyonya.



Hivi ndivyo yalivyo mapambano ya moto msituni Amazon.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumamosi iliyopita, Rais Bolsonaro, alisema yuko katika matarajio hali itarejea kawaida na hadi mwisho wa wiki alikuwa na mazungumzo na wadau mbalimbali wa dunia kuuomba msaada.

Mbali na Rais Trump, aliwataja Waziri Mkuu Hispania Pedro Sánchez na aliowataja viongozi wengine wengi wa Latin Amerika.

Katika mkutano huo, Rais Bolsonaro kwa mara ya kwanza alikiri 'vijembe' vya wapinzani wake na hasa wanamazingira, kwamba moto huo msituni ni janga kwa maendeleo ya uchumi wa Brazil, ikisambaratisha mimea ya kijani, vyanzo vya hewa na hali ya hewa kubadilika.

Itakumbukwa hata jijini Dar es Sakaam karibuni, katika kikao cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), miongoni mwa ajenda muhimu katika kukuza uchumi wa muungano wa ukanda huo, suala la mazingira na hali ya hewa lilikuwa miongoni mwa ajenda muhimu.

**UGENINI WACHACHAMAA**

Ijumaa iliyopita, mamia ya waandamanaji walikusanyika nje ya ofisi za kibalozi za Brazil hasa za nchi za Ulaya, wakitaka kuwapo hatua thabiti ya kikabili hali hiyo, hasa katika nchi za Ulaya na Latini Amerika

"Mapafu ya dunia yanaungua tunanusuru," yalisomeka baadhi ya maandishi ya waandamanaji, jijini Mexico City, nchini Mexico.

Ni suala lililochukua sura ya kisiasa, pale Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alipotangaza tishio la Umoja wa Ulaya (EU) kuzuia biashara na Brazil, pia baadhi ya nchi za Amerika Kusini.

"Kwanza tunataka kuisaidia Brazil kuuondoa moto huu," alitamka Jumamosi iliyopita na kisha akaongeza: "Lengo ni kuuhifadhi msitu huu, kwakuwa sote tunauhitaji kwa sababu ni hazina ya usalama wa mazingira na hali ya hewa. Tunashukuru oksijeni inayotoa na shukrani kwa hewa ukaa (carbon dioxide) inayounyonya."

Juzi Rais wa Brazil, Rais Bolsonaro, katika kile kinachoonekana kumjibu Rais wa Ufaransa Macron, kupitia mlango wa pili, kwamba nchi yake iko tayari kupekea misaada, lakini isiyo na masharti.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***

AFYA

# Halmashauri, watendaji waingia mkataba aina yake 'operesheni tokomeza utapiamlo'

• Baada ya kuvunja rekodi ya mkoa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UGONJWA wa utapiamlo nchini umekuwa changamoto kubwa, tatizo kubwa ni ukosefu wa lishe bora kwa mtoto.

Kitaalamu inaanishwa, ni ugonjwa unaoanza kwa mtoto anapokuwa tumboni kwa mama hadi siku 1000 za mwanzo, baada ya kuzaliwa.

Utapiamlo unaathiri ukuaji wa mtoto kiakili na kimwili na madhara yake ni vigumu kurekebishwa, kwani tangu mwanzo wa umri wake mtoto anakuwa na afya duni akishindwa kufanya shughuli zake kiuchumi, ukuaji hali inayoathiri nguvu kazi ya Taifa, sasa na siku za usoni

Ni ugonjwa unaotokea muda mwingi unaotokea kwa mjamzito. Ni matokeo, kabla ya kujifungua alikuwa anapata chakula kilichokosa viinilishe sahihi na baada ya kujifungua anaendelea kumpatia mtoto chakula kisichokuwa na lishe, hatua inayomfanya mtoto kuangukia maradhi hayo.

Inaelezwa, hali ya lishe nchini imekuwa hairidhishi, japo wananchi na wakulima kwa jumla, wanalima vyakula vingi, kuwapo kundi kubwa la watoto wenye umri chini ya miaka mitano kiafya wamedumaa, huku wengine wana uzito pungufu na wamekonda.

Vivyo hivyo, wapo kinamama walio katika umri wa kuzaa wamekonda kwa kukosa lishe, wakati zaidi ua nusu ya wajawazito wanatajwa kuwa na asilimia upungufu wa damu, jambo ambalo limekuwa likihatarisha maisha yao wakati au baada ya kujifungua.

Pia, kunaelezwa kuwapo utapiamlo unaoendelea kuongezeka na kuathiri zaidi wananchi vijijini, kwa kuchangia kuibuka magonjwa yasiyoambukiza kama vile moyo, kisukari na saratani.

Nchini, mikoa inayotajwa kuongoza kwa kadhia hiyo ni Kagera, Mbeya, Kigoma, Iringa, Arusha, Lindi, Shinyanga, Tanga, Morogoro, Manyara, Mtwara, Rukwa, Ruvuma, Dodoma, Singida, Mwanza, Pwani, Tabora, Mara, Kaskazini na Kusini Pemba.

### SHINYANGA WAJIPANGA

Kutokana na athari hizo mkoa Shinyanga kuwa na kiwango kikubwa cha utapiamlo, halmashauri zake zimeingia mikataba baina yao kupambana na ugonjwa huo.

Wawajibikaji katika hilo ni watendaji katika ngazi za kata na vijiji, kutokana na asilimia kubwa ya wagonjwa wanatoka katika maeneo yao.

Hadija Nasibu, ni Mratibu wa Lishe katika Halmashauri ya Ushetu, aliyeingia mikataba hiyo hivi karibuni na watendaji wa kata na vijiji, lengo ni kupambana na ugonjwa huo kwa kutoa elimu kuhusu namna ya kuandaa chakula chenye lishe kwa umma.



Watendaji wa kata na vijiji wa Halmashauri ya Ushetu. wilayani Kahama, wakimsikiliza Mratibu wa Lishe kutoka katika halmashauri hiyo, Hadija Nasibu, **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

> “Utapiamlo una madhara ya kuathiri mpaka akili na wakati mwingine ni vigumu kumtambua mtu au mtoto mwenye ugonjwa huo.



Mratibu wa Lishe kutoka Halmashauri ya Ushetu, Hadija Nasibu, akitoa taarifa kwa maofisa watendaji wa kata na vijiji, hali ya utapiamlo katika halmashauri hiyo na namna ya kupambana nao.

Anaueleza utapiamlo una madhara ya kuathiri mpaka akili na wakati mwingine ni vigumu kumtambua mtu au mtoto mwenye ugonjwa huo.

Hata hivyo anadokeza kuwa moja ya dalili zake ni kimo cha mtoto kuwa kidogo, kwani mtoto anapozaliwa anapaswa kuwa na uzito wastani wa kilo mbili hadi tatu na chini ya hapo ni dalili ya hatari, hasa kukosa lishe sahihi.

Hadija anaendelea kusema, udumavu kwa watoto umekuwa janga la Taifa kuanzia ngazi ya familia na unamkosesha mtoto uwezo wa ubongo wake kupevuka kuchanganua jambo.

Ni hali ambayo kitaalamu inarekebishika hadi kufikia umri wa miaka miwili tangu kuzaliwa kwake, baada ya halpo inakuwa vigumu kurekebishika .



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Uyogo, katika Halmashauri ya Ushetu, Edson Mobelo, akitia saini mkataba wa kupambana na ugonjwa wa utapiamlo.

### BAJETI ILIYOPO

Hadija anasema, Halmashauri ya Ushetu katika bajeti ya mwaka wa fedha wa sasa, imetenga fedha kiasi cha Sh. milioni 342.4 kuwahudumia watoto wenye umri chini ya miaka mitano jumla yao 65,315.

Anasema, halmashauri hiyo imekuwa ikitenga bajeti ya lishe kuvuka lengo la Sh.500 kwa kila mtoto aliye na umri chini ya miaka mitano na katika mwaka wa fedha uliopita, halmashauri hiyo ilitenga jumla ya Sh. milioni 276.8 na kiasi cha Sh. 1000 kilitolewa kwa kila mtoto.

Hadija anaeleza kuwa asilimia 28 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Shinyanga, wamedumaa na kiwango cha utapiamolo mkali kwa Halmashauri ya Ushetu, hivi sasa ni asilimia 0.076, na hali hii inaonesha utapiamlo katika halmashauri hiyo ni mkumbwa ukilinganisha na halmashauri nyingine.

Hata hivyo, anasema katika mwaka wa fedha 2015/2016 halmashauri ilitenga Sh. milioni 57,2 kwa idadi ya watoto 73,056 na kila mtoto alitengewa Sh. 784; mwaka wa fedha 2016/2017 walitenga Sh. milioni 70.8 kwa idadi ya watoto 73,056 na kila mtoto alipata Sh. 970.

Anasema, katika mwaka wa fedha 2017/18 walitenga Sh. milioni 140.05 kwa idadi ya watoto 73,056 na kila mtoto alilkuwa na Sh. milioni 2,040; na mwaka wa fedha uliopita walitenga Sh. milioni 276.8 kwa idadi ya watoto 64,550 na kila mtoto alipata Sh. 4,280.

### LISHE & KINGA

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu Nicodemus Lucas, anasema wamefanikiwa katika Kampeni ya Mwezi wa Afya na Lishe ya Mtoto, wamefanikiwa kwenye kata 20 walikotoa matone ya Vitamini A kwa watoto 57,820, ambao ni sawa na matarajio ya asilimia 99.26 ya watoto 58,248.

Anasema, ni hatua iliyoifanya halmashauri kuvuka lengo la kitaifa la asilimia 90, huku waliopata dawa za minyoo, walengwa walikuwa 51,180 na waliopata walikuwa 54,575. Hap ni sawa na asilimia 106.6.

Dk. Lucas anasema katika kundi la waliofanyiwa tathimini ya hali ya lishe walilengwa kuwa 58,248 walipimwa walikuwa 55,734 sawa na asilimia 96.

Sanjali na hilo, anasema kipindi cha Julai 2018 hadi Juni mwaka huu, kinamama wenye watoto chini ya umri wa miezi sita hadi 23 wamepata elimu ya ulishaji chakula cha nyongeza kwa watoto, kupitia watoa huduma katika vituo vya huduma na afya ya jamii.

### MADUKA VYAKULA

Mganga Mkuu huyo, anasema ndani ya kipindi hicho walifanya ukaguzi kwenye maduka ya vyakula 140 na kati ya hayo, maduka 12 yalibainika kuuza vyakula visivyokuwa na ubora, hususani vilivyokwisha muda wa matumizi na biashara katika mazingira machafu.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Atanus Lucas, akimkabidhi Mkataba wa Kupambana na Ugonjwa wa Utapiamlo, Mtendaji wa Kata ya Ukune, Jane Matiko.

> “Katika kundi la waliofanyiwa tathmini ya hali ya lishe walilengwa kuwa 58,248, walipimwa walikuwa 55,734 sawa na asilimia 96.

Hata hivyo, anarejea tatizo la lishe linaanza tangu mtoto anapokuwa tumboni hadi siku 1000 za mwanzo wa maisha yake, utapiamlo ukiathiri ukuaji wake kiakili na kimwili, baadhi ya madhara ni ya kudumu.

### WATENDAJI KATA/VIJIJI

Edson Mobelo, ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Uyogo, asemaye jiografia ya Halmashauri ya Ushetu imetawaliwa na wingi wa wakulima na wamekuwa wakilima chakula kingi, lakini watoto wametekwa na utapiamlo.

Anasema, mikataba waliongia na serikali ni njia mojawapo ya kukumbushana wajibu wa majukumu ya kazi, akidai binafsi atahakikisha kupambana na hilo katika eneo lake la kazi, akianza na elimu kwa umma.

Jane Matiko, kutoka Kata ya Ukune, anasema kampeni yake itaanza kwa kuitisha vikao vya maendeleo ya kata na kutoa elimu kwa wajumbe, watakapokuwa mabalozi kwenye maeneo wanayotoka.

Pia, anaahidi kuhakikisha anashirikiana na watoa huduma ngazi ya jamii, kwa kuitisha mikutano ya hadhara na kutoa elimu ya namna ya kuandaa chakula chenye lishe, ili ifikapo mwaka ujao wa fedha, mwezi Julai 2020, utapiamlo kwenye kata uwe umetoweka.

# Mtaalamu alivyochambua TGNP vs ngono kwa watoto

**Na Yasmine Protace**

NI wito unaotamba katika jamii kwamba ni wajibu na lazima kusimamia ulinzi wa mtoto, hasa dhidi ya ukatili wa kijinsia na kingono, ikielezwa njia sahihi kumuwezesha kufikia ndoto zake. Ndoto za watoto zinafifia baada ya kubainika kufanyiwa ukatili huo.

Inaelezwa kuwapo baadhi ya familia zinashindwa kutoa ushirikiano katika harakati za kuwachukulia hatua wahusika dhidi ya matukio hayo.

Mdau kutoka asasi ya kijinsia ya TGNP Mtandao, Gema Akilimali, anasema hivi sasa wameanzisha kampeni mahsusi kumlinda mtoto, lengo ni kuwasaidia wafikie ndoto zao.

Kwa mujibu wa Gema, ni kampeni iliyopewa jina la 'Mtakuwa' ikiendeshwa kwa kushirikiana na serikali, lengo ni kutokomeza ukatili kwa watoto na wanawake hadi ifikapo mwakani, 2020.

"Mpango huo unasaidia kuwapa ulinzi watoto, ndani na nje ya shule kwa kuwapatia uelewa ulinzi tofauti kwa wasichana na wavulana kwa kuweka bayana taratibu za kutoa taarifa za kingono," anasema.

Anaongeza kwamba takwimu za utafiti za afya ya uzazi na mtoto, zinaonyesha ukatili wa kingono unaongezeka,



Wanahabari walipokuwa mkutanoni kutambulishwa kampeni ya '1_5_5'iliyozindulliwa na TGNP Mtandao, kumlinda mtoto dhidi ya ukatili kingono. **PICHA: YASMINE PROTACE**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ikionyesha mwaka jana, kuna wastani wa watoto 394 kila mwezi walibakwa.

Pia, kuna takwimu za utafiti wa kituo hicho kinachosema, kati ya mwaka 2017 na 2018 hali ni mbaya maradufu katika matukio ya kulawitiwa na kubakwa, Dar es Salaam na Iringa ikiongoza kwa matukio hayo.

Gema anasema kuna mchango wa vyombo vya habari kuwa mstari wa mbele kukabili adha hiyo, ambayo TGNP ndio kinara wa kuikabili

Anarejea uzoefu wa miaka ilivyopita, matukio ya ulawiti na ubakaji hayakuwa mengi, akitoa mfano mabinti na wavulana walipita maporini pasipo kusikika au kushuhudiwa uharamia kama ilivyo sasa, kukishuhudiwa baadhi ni wanandugu.

Rai yake ni watoto kuacha ukimya na wazazi wafuatilie nyendo zao wanapotoka shule na wanapokuwa nyumbani, ikiwamo likizo, huku akiwasisitizia wazazi kwamba kutowasikiliza watoto kunachangia kuedeleza janga la ukatili kwa watoto hao.

Rehema Mwateba, mdau kutoka TGNP Mtandao, anaeleza imani yake kampeni ya sasa itasaidia kupunguza ukatili kupitia ulinzi wa haki za watoto na wakati huo huo, inawapa mbinu sahihi za kujilinda dhidi ya mabaya.

Mwanamama huyo, anawakumbusha wazazi wasiwasahau watoto muda wote, kwani ni jukumu lao kuwahakikishia usalama, kupitia hatua kama kukemea kauli chafu za vijana, kwani wanapojisahau inawagharimu watoto hao.

MAZINGIRA



DARASA KUTOKA ILONGA

# Kutoelewa afya ya udongo kunavyompa dhiki mkulima

**Na Christina Haule,** Morogoro

MTAALUMA Dk. Gillapsy, ambaye wakati fulani alishika chaki katika vyuo vikuu vya Phoenix na Ashford, nchini Marekani, anautafsiri udongo kuwa malighafi za asili na zisizo za asili zinazopatikana juu ya ardhi.

Katika mjumuiko huo, baadhi zina uhai na zingine hazina uhai, kulingana na asili zake.

Pia, udongo huo unaelezwa kutofautiana kati ya eneo moja na jingine, katika namna inavyojumuika.

Kwa mujibu wa Dk. Gillapsy, udongo kwa ujumla wake ni muunganiko wa malighafi tajwa, madini, gesi, maji na viumbe hai.

Mtafiti huyo aliyebobea katika sayansi ya udongo, anasema udongo una kazi kuu nne anazozitaja kuwa ni: Kuwezesha mimea kukua; kuhifadhi na kusafisha maji; kurekebisha hali ya hewa duniani; na makazi ya viumbe hai.

**TAALUMA NCHINI**

Sekta kama za misitu na kilimo nchini, wakiongozwa na magwiji wao Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Morogoro nao hawako nyuma katika kuelimisha, kutoa ushauri wa kitaalamu na kutafiti kuhusu udongo, ambao ndio ngome kuu ya hayo yote.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni katika Maonyesho ya Kuadhimisha Sikukuu ya Wakulima nchini, maarufu 'Nane Nane'kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Morogoro, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ilonga, Meshack Makenge, ana maoni kwa kinachopaswa kufanywa na wakulima.

Mtazamo wake ni kwamba, wajikite kutumia ramani za teknolojia ya afya ya udongo zilizo sambamba na kuweka mbolea kwenye udongo, kwa kuzingatia virutubisho ili wawe na uhakika wa mavuno.

Anafafanua kwamba, TARI imeandaa ramani za mikoa na wadau nchini zinazoonyesha hali ya udongo na ushauri wa matumizi ya virutubisho.

"Katika Nanenane hii, tumekuja na ramani hizo zinazoonyesha kila mkoa ni mbolea ya aina gani iwekwe kwenye udongo na kwa kiasi gani kupata mazao bora na mengi" anasema Makenge.

Anaeleza baadhi ya malalamiko ya wadau shambani, kwa kiasi kikubwa ni dai ardhi zao hazina tija kwa muda mrefu na maeneo mengi bado mavuno yapo chini. Sababu kubwa ni kwamba anaambulia elimu duni ya kutojua afya ya udongo.



Mkulima akiandaa shamba lake. **PICHA: MTANDAO.**

> Kutumia mbegu bora au mbolea hakuwezi kuzaa matunda kama mkulima hatojua hali ya udongo anaoutumia.

Makenge anasema kwamba, wakulima wamekuwa wakijiwekea mbolea pasipo kujua mahitaji ya udongo, hivyo anarejea maelekezo yake ya kitaalamu watumie ramani na elimu kutoka TARI, kuwezesha kujitosheleza kwa mazao nchini na hata mauzo nje ya nchi.

Mbali na Ilonga, TARI ina vituo vya Ukiluguru (Mwanza), Maruku (Kagera), Naliendele (Mtwara) na Uyole (Mbeya).

**KUPELEKA SAMPURI**

Bosi huyo ya TARI, anawaasa wakulima kupeleka sampuli zao za udongo kupimwa kwenye vituo vya utafiti kwa gharama nafuu, jambo litakalowawezesha kuvuna mazao yenye tija.

Pia anasema, kuna magonjwa mengine ya mimea yanaangukia matunda, hayahusu wadudu, bali kujua kama kutojua upungufu wa virutubisho.

Mratibu Mkuu wa Utafiti wa Udongo na Rasilimali Ardhi nchini, Dk. Sibawei Mwango, anawashauri wakulima kupima udongo kabla ya kuwekeza, kwani ndio siri ya mafanikio shambani.

Anasema kutumia mbegu bora au mbolea hakuwezi kuzaa matunda kama mkulima hatojua hali ya udongo anaoutumia.

"Watu wamezoea kwamba, ananunua shamba halafu anatafuta mbegu bora; mbegu bora haiwezi kufanya kazi kama ardhi bado hujaijua, afya ya udongo, lazima upate mazao hafifu," anasisitiza.

Mwango anatoa mfano wa zao la tikitimaji, linalopaswa kuwekewa mbolea maalum kufanikiwa sokoni, kupitia msalahi kama rangi yake, mzizi wa tatizo unanazia katika udongo.

Anasema, afya ya udongo nchini si mbaya, isipokuwa asilimia 16.5 ndio ina tindikali nyingi, hasa katika maeneo anayoyataja kuwa baadhi ya maeneo ya mikoa ya;Iringa, , Songwe, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Katavi, Rukwa, Kigoma, Kagera, Geita na Singida na wilayani Chunya

Anafafanua, udongo unapkuwa na tindikali ya kiwangio cha juu, mazao yanakuwa haba sana na mkulima anaambulia mazao hafifu yaliyedumaa na anapohitaji kutumia mbolea, analazimika kutumia kwa wingi, ili kuishibisha tindikali ardhini kwanza, ndio iweze kutoa mazao stahiki.

Kwa kurejea hali hiyo, anasema wameshawaelekeza wakulima wa maeneo hayo, mbinu ya kuanza kutumia chokaa kwenye udongo wa aina hiyo, kabla ya kuweka mbolea, ili iwe na tija.

Hata hivyo, Makenge, anasema kwa sasa, wamejipanga kutoa elimu pana kwa wananchi, kuhusu masuala ya kilimo bora, zaidi ya masuala ya matumizi ya ramani za udongo,

Katika hilo, Kaimu Mkurugenzi huyo wa TARI Ilonga, anasema watalazimika kupeleka katika maonesho ya wakulima, shamba darasa la kila kata za vijijini mkoani Morogoro.

Anafafanua kwamba, hiyo ni kuanzia mwakani, lengo kuu ni kuwafanya wakulima waboreshe tija na wakati huo huo kufungua fursa ya safari kuelekea kwenye Uchumi wa Kati ifikapo Mwaka 2025.

Anasema, Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, alishawaagiza kwenda hadi vijijini kutoa elimu hiyo, kwani wakulima wanahitaji zaidi elimu, ili waweze kuinuka kiuchumi kupitia sekta ya Kilimo.

Makenge anasema katika maonyesho hayo vijijini, kwenye kila kata kutakuwapo mipando na elimu ya teknolojia mbalimbali ikiwemo ya udongo, itakayotolewa na wakulima watakaoelimishwa, watatumia na kuboresha tija katika maisha yao.

Vivyo hivyo, anaeleza kuwa kila mwaka wameweka utaratibu wa kufanya maonyesho mengine kwenye vituo vyao vya utafiti yajulikanayo kama 'Maonyesho ya Kilimo na Biashara' na kuwafanya wakulima waelimike zaidi na kuongeza fursa mbalimbali za kiuchumi.

Anasema, katika sherehe hizo mwaka huu wameshafundisha wastani wa wakulima 3000 na kwa kutumia vyombo vya habari, kuna wakulima zaidi ya 3000 wameshajifunza teknolojia zilizopo TARI.

Makadirio yaliyopo ni kwamba, hadi kumalizika Nanenane, wameshatoa elimu kwa wadau na wakulima zaidi ya laki mbili na tatu na watakuwa wameshapata teknolojia zinazotolewa, watakazozisambaza kwenda kwa wenzao wengine.

AFYA

# Hivi ndivyo wanawake wanavyotesa 'vichanga' kuendekeza kulinda matiti

- Waziri ang'aka na 'awashukia' mchana kweupe

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

***MWEZI huu kumekuwapo mfululizo wa makala zinazohusiana na Siku ya Unyoyeshaji Duniani. Katika makala ifuatayo, pata undani wa tabia ya kinamama kukwepa kunyoyesha na namna inavyoathiri afya ya watoto na msimamo wa serikali ulipo. Endelea.***

KUANZIA tarehe Mosi ya mwezi Agosti katika mfululizo wa siku saba, ni maadhimisho ya Siku ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama, ambayo katika sayansi ya afya yanajulikana kuwa muhimu zaidi.

Pamoja na nafasi ya lishe hiyo, bado katika sura ya pili kuna changamoto lukuki inayoekezwa kutokana na kushuka kwa hali ya unyonyeshaji duniani, ikiwamo nchini Tanzania.

Takwimu za mwaka 2015/2016 na mwaka jana zinazoonyesha asilimia 43 tu ya watoto wanyonyeshwa hadi kufikia umri wa miaka miwili nchini. Shirika la Watoto Duniani(UNICEF), zinaonyesha kwamba takribani watoto milioni 7.6 duniani hawanyonyeshwi kila mwaka.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha idadi ya watoto wasionyonyeshwa na mama zao ni kubwa zaidi katika mataifa yaliyoendelea, ikilinganishwa na yale maskini.

Inaelezwa kwamba, asilimia nne ya watoto kwenye nchi maskini hawanyonyeshwi kabisa maziwa ya mama, wakati katika nchi zilizoendelea kundi hilo linafikisha asilimia 22.

Miongoni mwa sababu zinazotajwa, ni hofu ya baadhi ya wanawake kuharibu maumbile ya matiti yao kupitia dhana 'kuacha matiti yasimame' na wapo wengine wanashindwa kufanya, hivyo kutokana na kuelemewa na majukumu ya kimaisha

### KAULI YA WAZIRI

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anazungumzia hilo akiunga mkono hoja ya watafiti, kwamba kuna kundi la wanawake hawakunyonyesha watoto kwa madai ya matiti yao kuharibika na wanaishia kuwapa watoto vyakula mbadala.

Ummy analalamika kwamba, ni jambo linaoloathiri makuzi ya watoto na ulinzi wa maumbile ya watoto unakaribisha hatari ya saratani.

"Kuna watu wanaogopa wanadai kuwa wanachakaa hasa visichana vya siku hizi dhana hii si sahihi, matiti yakiharibika kuna 'blazia' sasa kipi bora kuharibika au kupata saratani, kuna watu wananyonyesha watoto 10 lakini matiti ni saa sita,"analalamika, huku akikumbusha hatari mtu anapoyonyesha anajiepusha na saratani, pia mimba za muda mfupi baada ya kujifungua.

Pia, anasistiza umuhimu wa watoto kunyonyeshwa kwa kipindi cha miezi sita ya kwanza bila ya kupewa kingine cha ziada, kwani wapo wazazi wanaokiuka kwa kuwapa maji na uji.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akizindua chumba maalum kwa ajili ya kunyonyeshea katika jengo la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya(NHIF), jijini Dodoma. **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI**

> **"Watoto walionyonyeshwa maziwa pekee bila kupewa maji au vyakula vingine kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58 ukilinganisha na asilimia 59 ya mwaka 2015/2016.**

"Watoto wanaonyonyeshwa bila kupewa chochote ni asilimia 58. Jitihada hazijafanikiwa, lazima tuwasaidie. Watalaamu wanasema miezi sita apewe maziwa ya mama tu. Sasa hawa wamama wanatingwa na majukumu wakiwaachia kina bibi majumbani, unakuta amepewa maji, uji kitu ambacho hakitakiwi," anasema.

Waziri Ummy anasema, idadi ya wanawake wanaonyonyesha watoto ipasavyo imepungua, hivyo kuna haja kutolewa elimu ya jamii kuwawezesha wapatiwe maziwa ya mama.

### ATOA AGIZO

Kupitia tamko hilo, waziri anaziagiza ofisi binafsi na za umma nchini, zitenge vyumba maalum vya kunyonyeshea watoto ana anawataka watumishi wanaonyimwa na waajiri muda huo wa kisheria saa mbili kunyonyesha, watoe taarifa ili hatua zichukuliwe, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004.

"Chumba hicho kitasaidia. Kuna saa maziwa yanatoka mengi, anaweza kwenda kwenye kile chumba akakamua maziwa akaweka katika friji na wataalamu wanasema yanakaa saa sita hadi nane," anaeleza.

Ummya anasistiza: "Hii itasaidia kinamama makazini kupata saa mbili kutoka kwa mwajiri kwa ajili ya kunyonyesha."

### MWAKILISHI UNICEF

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa Linalosghughulikia Watoto nchini (Unicef), James Gitau, anasema Shirika la Afya Duniani(WHO), linasisitiza mtoto anapaswa kunyonyeshwa hasa miezi sita ya mwanzo kabla ya kupatiwa vyakula vingine na itasaidia kuepuka magonjwa.

Anataja changamoto iilyopo ni kwamba, katika uwiano wa kasi ya unyonyeshaji, kwamba kuna mtoto mmoja kati ya wawili hawanyonyeshwi ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa.

Gitau, kwamba ili kuboresha unyonyeshaji, zinahitajika jitihada zinawazoshirikisha wanaume, familia na maeneo ya kazi.

### WANYONYESHAJI

Regina William, anaeleza uzoefu wake kwamba hakupenda kumnyonyesha mwanawe na alitekeleza hilo kipindi cha baada ya mtoto kutimiza umri miezi mitatu, akahamia katika kumpatia vyakula mbadala kama maziwa ya kopo na uji mwepesi.

"Mimi niliacha. Niliona naharibu matiti yatalala wakati nina uwezo wa kumpa mwanangu maziwa mbadala na akakua," anasema.

Mzazi mwingine, Jamila Omari, ana simulizi kwamba alikuwa anabanwa sana na kazi zake hata akalazimika kumuanzishia mtoto maziwa ya kopo na alipofikisha miezi minne alimuachisha kunyonya.

Anasema alipoifikia hatua hiyo ya kumuachisha mwanawe katika umri huo alihakikisha anampatia maziwa hayo na mpaka sasa mtoto huyo amefikisha umri wa miaka mitatu.

Sakina Abdula ni mkazi wa jijini Dodoma, mwenye mtazamo tofauti na kinamama watangulizi wake, akisema binfasi amewanyonyesha ipasavyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili na hakuwahi kufikiria kutowanyonyesha kwa hofu ya kuharibu maumbile.

"Mimi nashangaa wanaacha kunyonyesha eti wanaharibu matiti... wanawanyima watoto haki ya msingi ya kupata maziwa ya mama. Wengine tu ni wavivu kunyonyesha kwa uhalisia wanaleta visingizio ambavyo havina mashiko," anasema.

### VIFO TISHIO

Ofisa Lishe Mwandamizi kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe(TFNC), Neema Joshua, anasema tafiti zinaonyesha taratibu zisizofaa za unyonyeshaji zinaathiri maendeleo ya uhai wa watoto na inachangia kwa kiasi kikubwa.

Anasema vifo vya watoto wachanga vipo juu sana nchini ambapo Vifo 25 hutokea kwa kila vichanga 1000 waliozaliwa hai , huku vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vikiwa ni vifo 43 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai.

Vilevile, anasema katika kundi la watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kuna vifo 67 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai.

Anataja njia mojawapo ya kuepuka kasoro hiyo ni kuboresha huduma za afya, kwa kuwasaidia kinamama wawanyonyeshe ipasavyo watoto wao.

Anaeleza kuwa unyonyeshaji wa muda mrefu (miaka miwili au zaidi) unasaidia kupunguza unene uliozidi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari kwa watoto.

### UNYONYESHAJI ULIVYO

Mratibu wa Lishe ya Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sikitu Simon, anasema takwimu za utafiti wa hali ya lishe nchini mwaka jana, 2018 inaonyesha watoto wanaoanzishwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi ndani ya saa moja mara tu baada ya kuzaliwa ni asilimia 53, ikilinganisha na asilimia 51 wa mwaka 2015/2016.

"Watoto walionyonyeshwa maziwa pekee bila kupewa maji au vyakula vingine kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58 ukilinganisha na asilimia 59 ya mwaka 2015/2016,"anasema.

Hata hivyo, anasema takwimu hizo zinaonyesha asilimia 31 ya watoto chini ya miaka mitano wamedumaa ukilinganisha na asilimia 34 ya mwaka 2015/2016.

### UMUHIMU WAKE

Maziwa ya mwanzo baada ya mama kujifungua huwa ni mazito na yana rangi ya njano, yanayotoka siku chache baada ya mama kujifungua.

Maziwa hayo ni muhimu sana kwa lishe ya mtoto na yana kinga nyingi za mwili kumlinda mtoto na maradhi mbalimbali ya kibinadamu.

Hayo ni maziwa ya mwanzo yenye chembe nyeupe za damu ya mama, zinazotengeneza kinga mwili kwa ajili ya kumlinda mtoto dhidi ya maradhi.

AFYA

# Watumishi wa afya wanolewa kukwepa ebola wawapo kazini

**Na Yasmine Protac**

KIAFYA na kitaalamu, watoa huduma wana kila sababu ya kujikinga ili kuepuka maambukizi ya mgonjwa.

Hapo inamaanisha kwamba, watoa huduma kama vile madaktari, wauguzi na watalamu wa maabara, wanapojikinga kiafya, wanabaki salama katika kipindi chote cha utoaji huduma hizo, hawapati mgonjwa ya kuambukiza.

Mamlaka za afya kiserikali zimekuwa zikiwasisitiza watumishi wa afya, pindi wanapotoa huduma hizo, wahakikishe wanajikinga vilivyo.

Hivi karibuni, timu za uendeshaji wa huduma za afya za halmashauri za mkoa wa Mwanza, zimepata maelekezo hayo, kuhusu namna ya kusimamia miongozo ya kukinga na kudhibiti maambukizi ya magonjwa wakati wanapotoa huduma zao za afya kwa wagonjwa.

Dk. Joseph Hokororo, ni ofisa kutoka Kitengo cha Uhakiki bora wa Huduma, kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, mwenye maelezo ya kina kuhusu namna ya kujikinga dhidi ya maambukizi hayo.

Dk. Hokororo alitoa ufafanzi huo katika mafunzo ya njia bora ya kujikinga na kudhibiti magonjwakwa kufuata kanuni, miiko na taratibu za utoaji huduma kwa mgonjwa, iliyofanyika jijini Mwanza, ikiwa namna mojawapo ya kukabili hatari ya kupata ugonjwa wa ebola.

Pia, anasema mafunzo hayo kwa sura nyingine, yametumika kama njia ya kusambaza mwongozo mpya wa kujikinga na kudhibiti maambukizi, yaliyoandaliwa na wizara inayohusika na afya, ikilenga kuboresha huduma za afya kitaifa.

"Katika mafunzo hayo, inadaiwa Tanzania ipo kwenye hatari ya kupata wagonjwa wa ebola, kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu na ukaribu na nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), ambako mlipuko unaendelea," anasema.

Dk. Hokororo anasema kwamba duniani kunakadiriwa kuwapo watu bilioni 2.5 waliopo hatarini kuambukizwa ebola,

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kati ya wanaoshukiwa, asilimia 60 wanatoka Kusini mwa Jangwa la Sahara, huku nchi za Sudan, Uganda na DRC, ambako maambukizi ya ugonjwa yalianza tangu mwaka 1976. Anasema, kulingana na taarifa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa kuwapo wagonjwa 1,790 wanapoteza maisha tangu mlipuko ulipojitokeza Agosti mwaka jana kutoka kundi la wagonjwa 2577.

Taarifa zinaonyesha katika orodha hiyo, kuna wataalamu wa afya 131 walipata maambukizi na kati yao, 41 wamepoteza maisha.



Wahudumu wa afya wakifuatilia mafunzo ya namna ya kujikinga na magonjwa ya maambukizi, pindi wanapowahudumia wagonjwa. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

> **Katika mafunzo hayo, inadaiwa Tanzania ipo kwenye hatari ya kupata wagonjwa wa ebola, kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu na ukaribu na nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), ambako mlipuko unaendelea.**

**HATUA ZA SERIKALI**

Anasema, hadi sasa serikali nchini imekwishachukua hatua mbalimbali za kujiimarisha kukabiliana na tishio la ugonjwa huo, kuidhibiti isiingie nchini, ikijumuisha elimu kwa umma katika namna ya kujikinga.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wa afya, pia watoa huduma za afya wameimarishwa na mbinu za kumhudumia mtu mwenye dalili za ebola.

Dk. Hokororo kupitia mafunzo hayo, anawataka watoa huduma kuzingatia taratibu za kujikinga na kudhibiti maambukizi kwa kadri miongozo stahiki inavyoelekeza wakati wote, jambo analosisitiza litasaidia kuwaepusha na maambukizi katika namna tofauti, pamoja na mgonjwa.

Dk. Hokororo anasema, anawatahadharisha watoa huduma kuwapo katika hatari kubwa za kupata maambukizi ya ugonjwa huu, endapo hawatofuata miongozo na taratibu za utoaji huduma kwa kadri ya mwongozo huu

"Mara kwa mara ni muhimu kuwa na tahadhari wakati unahudumia wagonjwa, hususan kunawa mikono kabla na baada ya kutoa huduma kwa wagonjwa na wasio wagonjwa," anasema Dk. Joseph Hokororo.

Anasema WHO inakusudia kuzuia ebola kwa kuimarisha huduma za uchunguzi na kusaidia nchi zilizo hatarini kuupata ugonjwa huo, huku akikumbusha kwamba hadi sasa dunia imekumbwa na tatizo la usugu wa vimelea vya magonjwa ambukizi dhidi ya dawa, hali inayotamkwa kitaalamu kuwa 'antimicrobial resistance.'



Ofisa kutoka Kitengo cha Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Joseph Hokororo, akifafanua jambo kwa watumishi afya waliokuwa katika mafunzo ya stadi za kujikinga.

Dk. Hokororo anasisitiza umuhimu wa kufuata taratibu za kutoa huduma, ikiwa ni moja ya njia sahihi za kusaidia kuvitokomeza vimelea hivyo.

Mkufunzi, Dk. Chrisogone German, kutoka wizara hiyo inayohusika na afya, anafafanua mbinu za kujikinga dhidi ya maambukizi wakati wa wazazi kujifungua, anataja umuhimu wa kutumika kinga kwa wote wanaohudumu.

Msisitizo wake ni kwamba, si jambo zuri kwa watoa huduma za afya, kufanya mambo kwa mazoea, hali inayochangia kusambaa maambukizi kutoka kwa mtu anayepokea huduma za afya au mtoa huduma.

# TBL Mbeya yatoa msaada wa vifaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) Tawi la Mbeya, imetoa msaada wa printa 12 kwa shule za sekondari na msingi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya ili kurahisisha uchapaji wa mitihani na nyaraka za serikali shuleni.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Meneja wa TBL Mbeya, Godwin Fabian, alisema utoaji wa vitendea kazi hivyo ni sera ya kampuni na kwamba mikoa mingine ukiwamo Mwanza pia imenufaika.

Alisema printa hizo zitarahisisha utendaji kazi kwenye taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule ili kuhakikisha huduma zinapatikana kwa wakati.

"Mbali na kiwanda chetu kuzalisha vinywaji vya aina mbalimbali, tunafanya kazi kwa karibu na taasisi za umma kwa sababu ni wadau wetu muhimu kwenye masuala ya biashara. Kwa kutambua umuhimu huo, tumeamua kutoa printa 12 kwa shule za msingi na sekondari ili kurahisisha shughuli za uchapishaji," alisema Fabian.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, Ofisa Elimu Msingi jijini hapa, Oscar Kapinga, alisema msaada huo ni chachu kwao katika kuhakikisha shule zote zinakuwa na vitendea kazi kama printa.

Alisema shule nyingi hazina printa hali inayowalazimu kutumia gharama ili kuchapisha mitihani au nyaraka mahali pengine.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga ambayo ni miongoni mwa wanufaika, Edward Mwantimwa, alisema printa hizo zitarahisisha shughuli za utendaji hasa kupindi cha mitihani ya majaribio ya wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya taifa hivi karibuni.

Alisema shule hiyo ambayo ni kongwe, inakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi hasa vya kufundishia licha ya serikali kujitahidi kusaidia.

# Taasisi sasa yageukia viazi mviringo

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

WATAFITI wa viazi mviringo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) - Uyole mkoani Mbeya, wamejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu kupitia teknolojia ya kisasa ili kukidhi mahitaji ya malighafi zinazohitajika kwa ajili ya uchumi wa viwanda.

Akizungumza juzi katika mahojiano maalumu na gazeti hili, Mratibu wa Kitaifa wa Viazi Mviringo, Dk. Juma Kayeke, alisema hatua hiyo inatokana na baadhi ya wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika na kuchakata viazi mviringo, lakini uzalishaji bado ni wa kiwango kidogo.

Dk. Kayeke alisema licha ya asilimia 90 ya viazi mviringo vinatoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Iringa na Njombe, Rukwa na Katavi, bado uzalishaji huo haukidhi viwanda vinavyotarajia kujenga, hivyo Tari-Uyole imeamua kuanza mkakati wa kuzalisha mbegu zaidi kupitia teknolojia za kisasa.

Mratibu huyo alisema zao hilo kwa sasa limekuwa likizalishwa na wakulima wadogo ambao wengi wao wamekuwa wakitumia mbegu za kienyeji na kuvuna kati ya tani saba hadi 10 kwa hekta, kiasi ambacho ni kidogo na kushindwa kutosheleza mahitaji ya viwanda.

Alisema kwa kutumia teknolojia ya kisasa mkulima anaweza kuvuna hadi tani 40 kwa hekta moja na tayari wameshaanza kutoa elimu kwa wakulima kwa kutumia mashamba darasa na maonyesho ya kilimo.

Mtaalamu wa maabara ya kutengeneza mbegu za viazi mviringo kwa kutumia teknolojia ya kisasa, Emanuel Mwampate, alisema endapo wataongeza vifaa vya kisasa, wana uwezo wa kuzalisha mbegu hadi tani 60 kwa mwaka, hivyo kusaidia mahitaji ya mbegu za kisasa kwa wakulima ambao watazalisha malighafi zinazohitajika viwandani.

Alisema mbegu hizo za teknolojia ya kisasa zimekuwa na ukinzani wa magonjwa mbalimbali kama ukungu wa viazi, mnyauko, magonjwa yanayotokana na virusi, magonjwa ya mizizi na bakteria ambayo yamekuwa yakisumbua wakulima wa zao hilo.

Naye mtafiti wa zao hilo, Dora Mende, alisema Tanzania ni nchi ya 15 kwa kuzalisha viazi mviringo, lakini bado wakulima wengi hawatumii mbegu bora hivyo ili kuongeza uzalishaji ni lazima uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora na za kisasa ufanywe kuongeza uzalishaji.

Alisema licha ya watafiti kutoa mbegu bora na kuthibitishwa zikiwamo za Tenguru, Sherekea na Asante na kufanyiwa majaribio katika maeneo mbalimbali, uzalishaji wake umeonekana kuwa mzuri na kuna baadhi kunahitajika mbegu zingine zitakazoendana na mazingira.

Mtafiti huyo aliwataka wakulima wa zao hilo kuchangamkia mbegu za teknolojia ya kisasa ambazo zimeanza kuzalishwa na Tari ili kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija ili kukidhi mahitaji ya viwanda.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Rukia Muwango, akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya Wiki ya Elimu ya Mlipakodi na Tozo za Serikali, katika uwanja wa Naipanga wilayani humo juzi, kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kutambua umuhimu wa kulipa kodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Wachungaji wapinga vitendo vya ukatili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WACHUNGAJI wanawake wa Kanisa la Moravian Tanzania, wamezindua kampeni ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto yenye lengo la kuweka usawa na haki katika makundi hayo.

Wakizungumza na Nipashe jana kwenye kongamano la wachungaji lililofanyika Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (Teku), jijini Mbeya, wachungaji hao walisema walifikia uamuzi huo baada ya kubaini kushamiri kwa vitendo vya ukatili katika jamii licha ya serikali na wadau wengine kupaza sauti kukemea.

Mmoja wa wachungaji hao ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji Teku, Dk. Mary Kategile, alisema lengo la kuanzisha kampeni hiyo ni kuwaweka pamoja wanawake ili washirikiane kutoa elimu juu ya madhara ya vitendo vya ukatili katika jamii.

Alisema kampeni hiyo inakwenda sambamba na kuazimia uvaaji wa nguo nyeusi kila ifikapo siku ya Alhamisi ya juma ikiwa ni alama ya ukimya kupinga vitendo hivyo.

"Ukatili ulioshamiri hivi sasa ni wa kisaikolojia na waathirika wakubwa ni watoto wanaofanya kazi za ndani. Baadhi ya waajiri huwanyanyasa watoto hao kwa kuwatolea kauli mbaya za udhalilishaji," alisema Dk. Kategile.

Alisema kati ya watoto sita wanaofanya kazi za ndani, wawili wanakumbana na kadhia hiyo ya kutolewa kauli za kudhalilisha na mabosi wao hali inayosababisha kutoroka au kuwadhuru watoto wanaowalea.

Aliongeza kuwa ukatili mwingine kuwa ni wa kiuchumi unaofanywa na wanaume na kwamba wanawake wengi, hasa waishio vijijini, ni wazalishaji wakubwa kwenye shughuli za kilimo lakini unapofikia wakati wa mavuno, kinababa huwatenga na kufanya uamuzi peke yao kuhusu mavuno hayo.

Dk. Kategile alisema kitendo hicho kimekuwa kinawaumiza kinamama na kujiona hawana sauti yoyote katika kufanya uamuzi wa familia hasa kupanga na kuamua mambo ya kufanya kutokana na mavuno waliyopata licha ya kuwa wazalishaji wakuu.

Alisema kampeni hiyo ya kupinga ukatili itafanikiwa kwa sababu watafikisha elimu kupitia nyumba za ibada na makongamano mbalimbali watakayokuwa wanaandaa.

Mkuu wa Dawati la Jinsia mkoani Mbeya, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, (ASP) Janeth Masangano, alipongeza hatua ya wachungaji hao kuanzisha kampeni ya kupinga vitendo vya ukatili na kuwakumbusha kupaza sauti kuhusu mimba za utotoni.





## Ushauri kujikinga tetemeko la ardhi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANANCHI jijini Dodoma wametakiwa kujenga majengo yenye ubora ili kukabiliana na matetemeko ya ardhi yanayotokea mara kwa mara.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Majanga ya Asili na Jiolojia, Gabriel Mbogoni, wakati akizungumza na gazeti hili jijini hapa.

Mbogoni alisema Jiji la Dodoma linakabiliwa na matetemeko ya mara kwa mara ambayo mengine hayaonekani kwa macho au kusikika, lakini yanaonekana kupitia vyombo maalum vya kupimia majanga hayo.

Aliwataka kutofanya shughuli zinazoweza kusababisha ongezeko la matetemeko hayo kwa kuwa athari zake zitakuwa ni kubwa zaidi.

Alitaja baadhi ya shughuli hizo kuwa ni pamoja na uchimbaji madini kwa kutumia vilipuzi (baruti) kwa kuwa vyenyewe vina uwezo wa kutikisa ardhi na kusababisha tetemeko.

Uvunaji wa maji kutoka ardhini kwa kiwango kikubwa kwa kuwa hali hiyo husababisha miamba yenye maji iliyojipanga ardhini kutikisika na kusababisha tetemeko pia.

"Kwenye ardhi kuna miamba imejipanga ambayo kawaida mingine huwa na maji ambayo ipo kwenye uwiano (Equillibium) hivyo unapovuna maji kwa wingi kutoka ardhini unaharibu uwiano huo," alisema.

Nyingine ni ulipuaji mabomu ya nyuklia ambayo alisema Tanzania hakuna shughuli kama hizo.

Kufuatia hali hiyo aliwataka wananchi wa Jiji la Dodoma na mikoa yenye matetemeko ya mara kwa mara kuchukua tahadhari kwa kujenga nyumba bora zenye kuhimili na kujifunza mambo yanayotakiwa kuzingatiwa mara tetemeko linapotokea.

Alitaja baadhi ya mambo kuwa ni kukaa sehemu salama yenye uwazi isiyo na majengo marefu, miti, nguzo za umeme  mpaka mitetemo itakapomalizika.

"Endapo utakuwa unaendesha chombo chochote cha moto unashauriwa usimame kwa uangalifu sehemu salama mpaka litakapopita kwakuwa tetemeko linauwezo wa kuvunja madaraja na kuharibu barabara," alisema.

Alisema ukiwa ndani ya nyumba unashauriwa ubaki humo na ukae kwenye makutano ya kuta uvungu wa meza kiti au kitandani hadi tetemeko litakapoisha.

Aliongeza kuwa mtu anashauriwa asitumie muda mrefu kutafuta mahali pa kujihifadhi kwa kuwa tetemeko la ardhi husafiri kwa kasi ya kilomita mbili hadi 13 kwa sekunde moja.

Alibainisha kuwa takwimu zinaonyesha kuwa watu wanaotaharuki na kukimbia ovyo wakati wa tetemeko la ardhi ndiyo wanaopata madhara zaidi.

Aliitaja mikoa mingine ambayo ipo kwenye athari ya kupata matetemeko ya ardhi mara kwa mara kuwa ni Arusha, Manyara, Singida, Iringa, Kagera, Kigoma, Rukwa, Katavi, Mbeya, Njombe na Ruvuma.

# Viongozi S/mitaa kuhamasisha bima ya afya

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia afya, Dk. Doroth Gwajima, amewataka viongozi wa serikali za vijiji nchini kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya ya jamii (CHF) iliyoboreshwa ili waondokane na adha wanapokuwa hawana fedha mkononi.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana wakati alipotembelea zahanati ya kijiji cha Chiboli, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma kushuhudia zahanati hiyo inavyoandikisha idadi kubwa ya kaya katika mfumo huo.

Alisema suala la kuhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa siyo jukumu la wataalamu wa afya kwa kuwa wanaotakiwa kulisimamia ni viongozi wa vijiji ambao ndiyo wenye watu.

Alisema katika maeneo mengi wataalamu wa afya wamekuwa wakikosea kwa kuacha kufanya kazi zao za kutibu na kuingia katika kuhamasisha wananchi kujiunga na bima hiyo.

"Hili suala la watu kujiunga na bima hii ya afya ya jamii ya CHF iliyoboreshwa ni suala la kushirikisha viongozi wa vijiji kama mwenyekiti wa kijiji na ofisa mtendaji wa kijiji ndiyo wenye watu na wenye mikutano ya hadhara ambayo ajenda hii wataifikisha kwa njia rahisi," alisema Dk. Gwajima.

Pia Dk. Gwajima alisema kama viongozi wa serikali za vijiji watakuwa na ushirikiano na wataalamu wa vituo vya afya nchini, wataweza kuibeba ajenga hiyo kwa kuifikisha kwa wananchi na kuziandikisha kaya zote nchini katika mfumo huo wa CHF iliyoboreshwa.

"Hapa Chiboli wameweza na ni kijijini sana ni zaidi ya kilomita 90 kutoka mjini, lakini wameweza kuandikisha zaidi ya kaya 315 toka walipoanza mwaka jana mwezi Novemba," alisema.

Naye muuguzi wa zahanati hiyo, Shija Makeja, alisema  kupata mafanikio ya kuwa na idadi kubwa ya wanachama wa bima ya afya ya jamii CHF iliyoboreshwa kumetokana na kushirikiana kwa karibu na viongozi wa serikali ya kijiji.

"Mwaka jana tulipata mafunzo ya mfumo huu tuliporudi tulishirikisha viongozi wa serikali ya kijiji pamoja na kamati ya uendeshaji wa zahanati na kulipeleka suala hili kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara ndipo watu walipo hamasika na kujiunga kwa idadi kubwa," alisema.

Alisema kutokana na kuhudumia idadi kubwa ya watu wanaotumia bima hiyo, wamepata fedha za kujiendesha na kuondokana na changamoto za ukosefu wa dawa ambao awali ulikuwa kikwazo.

Kwa upande wake, Meneja mradi wa HPSS Tuimarishe Afya, Ally Kebby, alisema azma ya serikali ni kutengeneza mfumo wa bima ambao mwananchi atatambuliwa na pesa anayochangia itarudi kwenye kituo.

Alitoa rai kwa watumishi wa Zahanati ya Chiboli kuhamasisha wananchi wajiunge na bima hiyo kwa kushirikiana na uongozi wa sehemu husika.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (kulia), akimpongeza Meneja wa Kampuni ya Kichina ya ujenzi wa barabara ya Stecol Corporation, tawi la Tanzania, Guo Xin ming (katikati) walipokutana jana jijini Dodoma. Kampuni hiyo ilipongezwa kutokana na kukamilisha barabara kwa wakati. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Wadau mifugo wajadili kanuni za uzalishaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WADAU wa sekta ya mifugo nchini wamekutana jijini Dodoma kwa ajili ya kujadili kanuni za uzalishaji mifugo kwa njia zisizo za asili ili kuwezesha kuzalisha mifugo bora.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia sekta ya mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili uwezekano wa uwepo wa kanuni za uzalishaji mifugo kwa njia zisizo asili ambazo zitasaidia kupata mifugo bora.

Alisema kikao hicho ni muhimu kwa wadau husika hivyo ni vyema kutumia nafasi hiyo kujadili kwa umakini.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwenu wadau utumie vizuri kwa sababu unakwenda kuleta matokeo mazuri katika sekta ya mifugo," alisema Profesa Gabriel.

Alisema wameamua kuwashirikisha wadau katika mkutano huo kwa sababu wao ndio wahusika wakuu na wanahitaji kujadili na kuona umuhimu wa uwepo wa kanuni hizo ikiwamo kwenda kuzitumia.

"Hizi kanuni lazima zipitishwe kisheria ndio maana unaona wanasheria wapo katika majadiliano haya, lengo ni kuweka mambo sawa katika kikao," alisema Profesa Ole Gabriel.

Akielezea faida ya kanuni hizo endapo zitapitishwa kisheria, alisema zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuzalisha mifugo bora, kupunguza magonjwa kwa mifugo ikiwamo kupunguza wingi wa madume na magonjwa kutoka ng'ombe mmoja kwenda kwa mwingine.

Alisema hii ni moja ya kutaka kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano inayosisitiza uchumi wa viwanda hivyo ni lazima kuzalisha mifugo bora ambayo itatoa bidhaa bora kutoka sekta ya mifugo.

"Hiki kikao ni muhimu sana kwa sababu kitakwenda kusaidia kupunguza baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo," alisema Profesa Gabriel.

Aliainisha moja ya changamoto zinazoikabili sekta hiyo kuwa ni pamoja na magonjwa, ubora wa mifugo, gharama ya utunzaji madume kuwa kubwa jambo ambalo kanuni za uzalishaji wa njia zisizo asili zikipitishwa itasaidia kuondoa kero hizo.

Alisema kanuni hizo zitasaidia kupunguza changamoto hizo na kuleta matokeo mazuri kwa mifugo itakayozalishwa kwa njia zisizo za asili.

Alisema njia hiyo ina manufaa makubwa kwa wafugaji kwa sababu wanakwenda kujua ni aina gani ya ng'ombe anakwenda kuzaliwa anapokuwa na mimba.

Alisema njia hiyo pia itasaidia wanaofuga kienyeji kuwa na ng'ombe bora ikiwamo uzalishaji bora kwa sababu watabadilika kimtazamo wa ufugaji.



# Shein: Kiswahili ni kiunganishi cha Rwanda, Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ameeleza kuwa lugha ya Kiswahili itakuwa kiunganishi kizuri katika kukuza ushirikiano na uhusiano kati ya Rwanda na Zanzibar.

Akizungumza na Balozi wa Rwanda nchini Tanzania, Eugene Kayihura, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kuaga, Dk. Shein, alisema azma ya Rwanda na Zanzibar kushirikiana katika sekta ya elimu hasa katika mafunzo ya lugha ya Kiswahili, itajenga uhusiano mwema kati ya pande mbili hizo.

Alieleza kuwa hatua hiyo itakuwa na mafanikio makubwa hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa lugha ya Kiswahili imeteuliwa kutumika rasmi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema amefurahishwa na uhusiano mzuri uliopo kati ya Rwanda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar na kusisitiza uendelezwe.

"Uhusiano na ushirikiano wetu ni lazima uendelezwe kwa kuwa sote ni ndugu na haya ndiyo yanayotupa nguvu na ari ya kuyaimarisha na kuyaendeleza maendeleo yetu tulioyapata sambamba na kufikia malengo tuliyoyakusudia," alisema Dk. Shein.

Rais Dk. Shein alimweleza balozi huyo mafanikio yaliyopatikana Zanzibar kutokana na sekta ya utalii ni pamoja na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watalii ndani ya miaka tisa ya uongozi wake.

Alimweleza balozi huyo kuwa idadi ya watalii wanaokuja kuitembelea Zanzibar imeongezeka kwa kiasi kikubwa ikifananishwa na ya mwaka 2010 na kwa hivi sasa watalii wanakadiriwa kufikia 600,000 walioitembelea Zanzibar.

Katika kuhakikisha sekta ya utalii inaimarika zaidi, Dk. Shein alimweleza balozi huyo mikakati iliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Alisema hatua hiyo ya kuendeleza ujenzi huo ambao ulisita kwa muda, itazidisha na kuongeza idadi ya watalii watakaoingia Zanzibar na kuifanya sekta hiyo izidi kuimarika na kuongeza pato la taifa na fedha za kigeni.

Naye Balozi Kayihura alisema Rwanda inajivunia uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Zanzibar na kusisitiza kuwa miongoni mwa uhusiano huo ni kushirikiana katika sekta ya elimu hasa katika kujifunza lugha ya Kiswahili ambayo Zanzibar ndio kitovu cha lugha hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, itakuwa ni jambo la busara kwa Rwanda kuleta vijana wake kujifunza Kishwahili na kubadilishana uzoefu kati ya vijana hao na wenzao wa Zanzibar hatua ambayo itakuza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano.

Alisema Rwanda ina mambo mengi ya kujifunza na kupanua wigo kutoka Zanzibar kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya utalii na watalii wengi wanaotembelea nchi hiyo pia hufika Zanzibar.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Uongozi wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, wakati wa Mkutano wa Utekelezaji wa Bajeti na Mpango Kazi wa wizara hiyo, kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2019, uliofanyika ukumbi wa Ikulu Zanzibar jana. Kushoto kwake ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi na (kulia kwake) ni Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Waagizwa kuyabaini maeneo yenye uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa Shehia pamoja na watendaji wao wametakiwa kuyatambua na kuyaripoti maeneo yanayotumiwa kufanywa vitendo vya uhalifu ikiwamo dawa za kulevya pamoja na udhalilishaji ili kuondoa kadhia hiyo katika jamii.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, alieleza hayo wakati akizungumza na masheha 31 kutoka shehia zilizomo ndani ya Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema viongozi hao wanalazimika kuzielewa na kuwajibika vyema dhamana zao za uwenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama kwa kufanya vikao kwenye shehia zao, ili kujadili matatizo yanayotendeka kwenye maeneo yao ikiwamo utumiaji wa dawa za kulevya na udhalilishaji ili kuyapatia ufumbuzi wa kudumu.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa masheha kufanya vikao vitakavyoandaa ripoti zenye mapendekezo na hatimaye kuzishauri serikali za mitaa kupitia wakuu wa wilaya, ili kujenga mustakabali mwema kuanzia ngazi ya shehia hadi wilaya.

Alisema sheha ni kiungo muhimu cha kuunganisha serikali na wananchi, hivyo ni vyema wakawajibika kwa karibu kuimarisha ushirikiano baina ya pande mbili hizo ili kutoa tija na kutatua changamoto zilizopo za vitendo vya udhalilishaji.

Akizungumzia suala la masheha kuyatambua maeneo ya uwajibikaji, Katibu Mkuu Shaaban, alisema sheha mzuri ni yule anayeyatambua maeneo yake katika shehia yake wakati wote.

Alisema serikali imeridhika na kuteuliwa kwao kutokana na uwezo mkubwa walionao wa kufanya kazi inayosaidia serikali hasa katika masuala ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi kwenye maeneo yao.

"Kuteuliwa kwenu kumeonyesha imani kubwa kwa serikali katika kutatua changamoto ikiwamo matatizo yanayoibuka hivi sasa ya vitendo vya udhalilishaji na tatizo la vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya," alisema Shaaban.

Viongozi hao walisema wamekuwa wakichukua jitihada kubwa za kuwabainisha wahalifu na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria, lakini changamoto inayojitokeza hakuna hatua inayochukuliwa baada ya kuwakabidhi wahalifu hao na baadaye watu hao huendelea kutamba mitaani.

Walisema jambo hilo kwa kiasi kikubwa linawashushia hadhi na kurudisha nyuma uwajibikaji wao wa kila siku.

Pia wamemwomba Katibu Mkuu kulifikisha serikalini pendekezo lao la kupatiwa usafiri hata wa baiskeli wakati wa kutekeleza majukumu yao ili wapate unafuu.

# Wizara ya Afya yaagizwa kutoa ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Afya kuwa na mpango maalum wa ajira kwa wafanyakazi wa afya katika kipindi cha mwaka mzima, kutegemea na upatikanaji wa fedha kutoka serikalini.

Dk. Shein alitoa agizo hilo Ikulu Mjini Zanzibar, wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi wa Wizara ya Afya kwa mwaka 2018/19.

Alisema ili kufanikisha jambo hilo ni vyema kuwa na ushirikiano wa karibu kati ya wizara hiyo na Wizara ya Fedha ili kuwa na mpangilio mzuri wa ajira utakaowawezesha wanafunzi wanaomaliza masomo ngazi za shahada katika nyanja tofauti kuajiriwa kulingana na mahitaji.

Alisema kuwapo kwa utaratibu huo kutawawezesha wanafunzi wa fani mbalimbali za afya wanaosoma nje ya nchi kuwapo kwenye mpango huo na kuajiriwa baada ya kumaliza masomo yao.

"Ni muhimu kuwa na mpango kuliko kufanyakazi kwa kushtukiza," alisema.

Aidha, aliutaka uongozi huo kuongeza nguvu katika utoaji wa mafunzo ili kuwawezesha wataalamu waliopo kuwa na uwezo zaidi katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali.

Alisema kuna umuhimu kwa viongozi wa wizara hiyo kukaa pamoja na Mshauri wa Rais wa masuala ya afya, ili kuona utaratibu bora utakaokubalika kwa wafanyakazi, na madaktari bingwa wa kufanya kazi katika muda wa ziada na kubainisha umuhimu wa wafanyakazi hao kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria.

# Kanyasu awatangazia vita waharibifu misitu

**Na Lisungu Helela,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wananchi wote wanaopiga mbiu maarufu kwa jina la "mwano" kwa ajili ya kuwashambulia watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao katika Msitu wa Hifadhi ya Kumbulu uliopo Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro.

Hatua hiyo inakuja kufuatia uharibifu mkubwa wa ukataji miti ovyo unaofanywa na baadhi ya wanakijiji cha Kumbulu katika msitu huo, unaosimamiwa na Halmashauri ya Gairo kuwa endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa msitu huo utatoweka kabisa.

Pia, Kanyasu ameiagiza TFS kuwakamata watu wote waliovamia msitu huo walipe gharama zote za miti waliyoikata bila ya kuwa na vibali.

Naibu Waziri Kanyasu alitoa agizo hilo alipotembelea msitu huo na kujionea uharibifu mkubwa uliofanywa na baadhi ya wananchi waliovamia msitu huo licha ya kufahamu kuwa msitu huo ulitengwa kuwa hifadhi na serikali ya kijiji hicho tangu mwaka 2008.

Alisema uharibifu wa msitu huo ni mkubwa hali inayotishia jangwa, hivyo aliitaka TFS ipige kambi ndani ya msitu huo ili kudhibiti hali hiyo isiweze kuendelea.

"TFS ninyi ni jeshi shirikisheni na Jeshi la Polisi kwa ajili ya taratibu za kimahakama kwa wale wananchi wote watakaoendelea kukata miti pamoja na kuchoma mkaa ndani ya msitu huo," alisisitiza Kanyasu.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchemba, alimweleza Naibu Waziri uharibifu huo umedumu kwa muda mrefu na hatua za ufumbuzi kwa ngazi ya wilaya zilielekea kushindikana, kutokana na vitisho kutoka kwa wavamizi wa msitu huo.

Alisema wananchi wa kijiji hicho wamekuwa na tabia ya kupiga mwano ambayo ni wito wa kijadi ukiashiria kuna adui ambapo wananchi hutoka majumbani mwao na kila aina za silaha na kuanza kuwashambulia baadhi ya watendaji wa serikali. Alisema kufuatia hali hiyo baadhi ya watumishi wa TFS katika msitu huo wamenusurika kuuawa zaidi ya mara tatu, hali inayowakatisha tamaa kuendelea kuulinda msitu huo kwa kuhofia kuuawa.

Mchembe alimwomba Kanyasu kama ataridhia msitu huo usimamiwe na TFS badala ya Halmashauri ya Gairo kwa vile imeshindwa kuulinda na kuusimamia.




Ofisa Masoko wa Buchi Herbal Products, Ally Kubuli (kushoto), akizungumza na wateja, wakati wa mkutano wa Taasisi ya Urembo na Vipodozi uliokwenda sambamba na maonyesho ya bidhaa za urembo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA** .

# RC aipa NMB changamoto elimu huduma za kibenki

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ametoa rai kwa Benki ya NMB kutoa elimu ya huduma za kibenki kwa wananchi ili kujenga ufahamu wa huduma hizo hali ambayo itasababisha idadi kubwa ya Watanzania kujiunga na benki.

Mndeme alitoa rai hiyo, jana katika hotuba yake ambayo ilisomwa na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, wakati anafungua kongamano la walimu na NMB lililofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea na kuwashirikisha walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari kutoka katika Wilaya ya Songea.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, takwimu za kibenki zinaonyesha ni chini ya asilimia 40 ya Watanzania ndiyo wenye akaunti benki hali ambayo alisema inaonyesha kuna changamoto kubwa ya uelewa wa masuala ya kibenki kwa Watanzania walio wengi hasa wanaoishi katika maeneo ya vijijini.

"Kuna kila sababu ya vyombo vya fedha kuwa na programu maalum ya kutoa elimu hasa katika maeneo ya vijijini ili waweze kupata elimu sahihi na kufaidika na huduma za kifedha zinazotolewa na benki Tanzania," anasema Mndeme.

Hata hivyo, Mndeme aliipongeza NMB kwa kutoa mikopo mingi kwa wafanyakazi wa serikali kuu na serikali za mitaa, na kwamba asilimia kubwa ya walimu nchini wamefaidika na mikopo ya benki hiyo.

Takwimu za NMB zinaonyesha kuwa hadi sasa imetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni mbili ikiwa ni mikopo kwa wafanyakazi kiwango ambacho amesema ni kikubwa kuwahi kutolewa na taasisi za kifedha nchini.

Mkuu wa Mkoa alitoa rai kwa NMB kuendelea kuandaa programu nyingi kwa watumishi wote wa serikali ili kuwapatia fursa ya kujua huduma zinazotolewa na benki na kuendelea kubuni bidhaa mbalimbali za kibenki ambazo mtumishi wa kawaida anaweza kumudu.

"Endeleeni kupanua wigo wa mikopo, na mikopo yenu iwe na riba nafuu, pia endeleeni kuboresha huduma kwa wateja ili idadi yao iweze kuongezeka na kupata fursa nyingi za kukopa kwa masharti nafuu na kuongeza tija kwenye maeneo yao ya kazi," anasisitiza Mndeme.

Daniel Zake, Meneja wa NMB Tawi la Songea, akitoa shukrani za NMB kwa mgeni rasmi, alieleza kuwa benki hiyo ina matawi 229 nchi nzima, ATM zaidi ya 800 na wakala zaidi ya 7,000.

Zake alimthibitishia Mkuu wa Mkoa kuwa suala la riba litafanyiwa kazi na uongozi wa NMB, na kwamba kwa kanuni za benki kuna vikao mahususi kwa ajili ya kupitisha vitu vya namna hiyo.

## Sababu za Mwenge kukataa miradi bil. 6/-

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MWENGE wa Uhuru umemaliza mbio zake mkoani Singida, ambapo miradi mitano kati ya miradi 46 yenye thamani ya Sh. 6,025,876,427.80 imekataliwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokidhi viwango vya ubora.

Akikabidhi Mwenge huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Agrey Mwanry, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema kati ya miradi iliyokataliwa, mitatu ilikuwa ya kuwekewa mawe ya msingi, mmoja ulikuwa wa kufunguliwa na mmoja ulikuwa wa kutembelewa.

Aidha, Dk.Nchimbi aliitaja miradi hiyo ni wa maji wa Kijiji cha Meli, ujenzi wa maji Nduguti, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mkalama, ujenzi kituo cha mabasi Iguguno na ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Ziginali.

Kwa mujibu wa Dk. Nchimbi, ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Ziginali Halmashauri ya Itigi, utakagharimu Sh. 2,646,234,437, ujenzi wa mradi wa maji Nduguti Sh. 983,913,335, ujenzi Hospitali ya Wilaya ya Mkalama Sh. 1,784,200,000, ujenzi kituo cha mabasi Iguguno Sh. 125,758,600 na mradi wa maji Kijiji cha Meli Sh. 476,570,055.80.

## Ajivunia fedha za mfuko wa jimbo

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MBUNGE wa Masasi, Rashidi Chuachua (CCM), amesema hadi sasa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye jimbo hilo imegharimu Sh. milioni 34 za mfuko wa jimbo.

Chuachua aliyasema hayo mjini Masasi alipokuwa kwenye ziara yake maalumu ya ukaguzi wa baadhi ya miradi inayotekelezwa kupitia fedha za mfuko wa jimbo hilo.

Alisema fedha za mfuko wa jimbo la Masasi zina malengo ya kuhakikisha wananchi wanatekelezewa huduma mbalimbali za kijamii ambazo zinakosekana kwenye maeneo yao zikiwamo afya, maji na miundombinu.

Alisema jumla ya Sh. milioni 34 za mfuko wa jimbo zimeshatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye vijiji na kata zilizopo katika jimbo hilo na wananchi wameanza kunufaika na miradi hiyo.

Alisema baadhi ya miradi ambayo imeshatekelezwa na kukamilika kupitia mfuko huo ni miradi ya ujenzi wa matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa.

HABARI KIMATAIFA

# Fayulu aibuka adai maslahi, matokeo

**KINSHASA,** Congo

MGOMBEA aliyeshindwa kwenye uchaguzi wa rais katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Martin Fayulu, ameunda vuguvugu jipya la upinzani kwa ajili ya kile anachoita kuwa ni kudai maslahi ya wananchi na matokeo sahihi ya uchaguzi.

Vuguvugu hilo ambalo linajumuisha baadhi ya wapinzani akiwamo mshauri wa zamani wa Etienne Tshisekedi, linaelezea kwamba Joseph Kabila bado anaushawishi mkubwa katika uongozi wa Congo.

**Ni Kabila ndiye ana miliki bunge, ni Kabila ndiye anamiliki magavana na mabunge za majimbo.**

Fayulu alisema kwamba serikali mpya ilioundwa ni aibu kubwa kwa raia wa Congo waliotarajia mageuzi. Huku akisema kwamba raia hawana haja ya serikali hiyo bali kukamilisha mahitaji yake, huku akimnyooshea kidole cha lawama Rais mstaafu, Joseph kabila.

"Ni Kabila ndiye ana miliki bunge, ni Kabila ndiye anamiliki magavana na mabunge za majimbo.Ni Kabila ndiye aliteuwa Waziri Mkuu, ni kabila ambaye ana asilimia 65 ya mawaziri kwenye serikali hii mpya. Hiyo ni kuwakejeli raia ambao walipiga kura kwa ajili ya mabadiliko."

Kiongozi huyo wa upinzani aliyasema hayo wakati alipotangaza kuundwa kwa vuguvugu jipya liitwalo Dynamique pour la Verite des Urnes (DVU).

Fayulu alisema kwenye vuguvugu hilo wanatarajia kuendesha upinzani mkali kwa ajili ya mageuzi nchini DRC.

Miongoni mwa wapinzani walioijiunga na vuguvugu hilo jipya ni pamoja na Waziri Mkuu wa zamani, Adolphe Muzito, Jeanbaptiste Sonji Waziri wa zamani wa afya chini ya utawala wa Laurent Desire Kabila, na Valentin Mubake, moja wapo ya vigogo wa zamani wa UDPS na mtu wa karibu wa hayati Etienne Tshisekedi.

Mubake ambaye alimpinga Rais wa sasa Felix Tshisekedi alisema kwamba uchaguzi uliopita haukuleta mageuzi.

Mwanzoni mwa wiki hii, Rais Tshisekedi alitangaza baraza lake la mawaziri ambalo lina mawaziri 66 wengi wao hawajawahi kufanya kazi katika serikali. **DW**



Rais wa Uturuki, Tayyip Erdogan (kushoto) na mwenyeji wake, Vladimir Putin wa Urusi, wakijadiliana kuhusu mzozo wa kisiasa unaoendelea baina ya mataifa hayo mawili. **PICHA: REUTERS**

## Alilaumu shirika la ndege kwa kumtelekeza

**NAIROBI,** Kenya

RAIA wa Kenya ambaye ni mlemavu, Harun Hassan, amelilaumu Shirika la Ndege la Ethiopia, baada ya kuachwa na wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege wa Jomo Kenyatta (JKIA) ambao walikataa kumsaidia kupanda ndege kwenda Marekani.

Hassan ambaye pia ni mwandishi na mwanaharakati wa haki za walemavu katika ukurusa wake wa mitandao ya twitter na Facebook, alisema alidhalilishwa bila kujali, huku mmoja wa wafanyakazi akimwambia: "Tafadhali, hatuna msaada kwa mtu mwenye mlemavu anayesafiri peke yake."

Hassan alisema kuwa tiketi yake inaonyesha wazi kuwa yeye ni mtumiaji wa kiti cha magurudumu ambaye alikuwa akisafiri peke yake.

Hassan aliandika: "Waliniacha peke yangu na kunitekeleza, Kwa kweli hii inakwenda kinyume na sera na miongozo ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wa Kenya na sheria zingine za kusafiri za walemavu za kimataifa ambazo ndege hii inatakiwa kuzifuata"

Baada ya kuposti muda wa saa 10 kupita ndege ya Ethiopian Airlines ilimfikia, ikaomba msamaha na kumuomba aendelee na safari yake katika daraja la economy class. **BBC**

# Wageuka 'mbogo' wenzao kufukuzwa

**HONGKONG,** China

WANACHAMA wa Chama cha Wafanyakazi Hong Kong jana waliandamana dhidi ya Shirika la Ndege la mji huo, Cathay Pacific baada ya kuwafukuza kazi wafanyakazi wake kwa madai kuwa wanahusika na maandamano yanayoshinikiza kuwapo demokrasia yanayoendelea kipindi hiki cha joto.

Shirika la Habari la AP limeripoti kuwa bango nyuma ya jukwaa katika bustani ya umma iliyoko katikati ya mji lilisomeka kuwa "Sitisheni ufukuzaji kazi na acheni kuwatishia wafanyakazi wa CX," wakikusudia shirika hilo la ndege.

Muungano wa vyama vya wafanyakazi Hong Kong wamesema kuwa wafanyakazi 20 wamefukuzwa kazi wengine wamelazimishwa kujiuzulu, wakiwamo marubani, wahudumu wa ndege na mameneja.

Shirika la hiyo la Ndege lilieleza kuwa Mkurugenzi Mtendaji, Rupert Hogg, alijiuzulu mwamzoni mwa Agosti akiwajibika baada ya matukio hayo.

Cathay alithibitisha kufukuzwa kwa wafanyakazi kadhaa katika kipindi cha wiki mbili.

Alisema wafanyakazi hao walifukuzwa kutokana na sababu mbalimbali, kama vile rubani mmoja aliyetumia vibaya taarifa za kampuni au mwengine anayekabiliwa na kesi, bila ya kutaja maandamano.

Cathay ambaye ni rubani alishtakiwa kwa kufanya vurugu wakati wa maandamano. Muungano wa vyama vya wafanyakazi wameita maandamano kwa jina la Cathay Dragon, kundi la Cathay la Shirika la Ndege, aliyemfukuza mkuu wa chama cha wafanyakazi wahudumu wa ndege.

Mamlaka ya usafiri wa anga China wamemshinikiza Cathay kuwapiga marufuku wafanyakazi wanaofanya kazi katika ndege iwapo wataunga mkono.

Serikali ya China imekuwa ikipinga maandamano yanayofanyika katika mji wa Hong Kong ambao ina utawala wake unaojitegemea. **VOA**

## Waziri ahojiwa 'kutafuna' fedha za ebola

**KINSHASA,** Congo

WAZIRI wa zamani wa afya aliyejiuzulu mwezi uliopita katika Jamhuri ya kidemokrasi ya Congo (DRC), Oly Ilunga amehojiwa jana na Mwanasheria Mkuu wa serikali kujibu masuala kuhusu namna fedha za umma zilizolengwa kwa ajili ya kupambana na maradhi ya ebola zilivyotumika.

Wakili wake, Guy Kabeya, aliliambia Shirika la habari la Ufaransa AFP kuwa Dk. Ilunga alitoa ushahidi na kwamba ana imani na mfumo wa sheria wa nchi yake.

Taarifa kutoka mahakamani zilieleza kuwa Dk.Ilunga aliachiwa baada ya mahojiano kumalizika. Washauri wake watatu wa zamani, akiwamo tabibu mmoja bado wanashikiliwa rumande.

Dk. Ilunga alijiuzulu julai 22 baada ya kuondolewa wadhifa wa kuongoza juhudi za kupambana na ebola. Ugonjwa wa ebola umeua watu zaidi ya 2,000 DRC **DW**

# Serikali yatangaza bei elekezi ya mbolea

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imetangaza bei elekezi za mbolea ya kupandia (DAP) katika soko la ndani ya nchi, ambayo inatakiwa kushuka kwa Sh.8,000 hadi Sh.10,000 ambayo ni sawa na asilimia 13-17.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya na ushindani wa zabuni za BPS iliyofunguliwa Juni 21, 2019.

Alisema tayari mbolea tani elfu 29 imeshawasili nchini na imeanza kupelekwa kwenye maeneo husika, bei za mbolea ya DAP katika chanzo ilipungua kwa asilimia 12 ikilinganishwa na bei za zabuni ya Julai, 2018.

"Wizara yangu pia ilifanya marejeo ya kikokotoo cha bei elekezi ambacho kimetumika kwa misimu ya kilimo 2017/2018 na 2018/2019," alisema.

Alisema hatua hiyo imetokana na ushindani wa zabuni za BPS pamoja na marejeo ya kikokotoo umefanya bei ya mbolea kwa mkulima kupungua kwa wastani kimkoa wa Sh. 8,000 hadi Sh. 10,000 ambayo ni sawa na asilimia 13 - 17 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ainaya DAP.

Aidha, punguzo la Sh. 5,000 6,000 sawa na asilimia 14-19 kwa wastani wa kimkoa kwa mfuko wa kilo 25,wakati kwa mfuko wa kilo 5, bei imepungua kwa Sh. 1,300 hadi Sh. 1,500 sawa na asilimia 15 - 20.

Alisema bei elekezi ya mbolea ya DAP kwa mikoa ya Kanda ya Mashariki, Kati, Kusini na Kaskazini zitakuwa kati ya Sh. 51,900 na Sh. 60,300.

"Kwa mikoa ya Kanda ya Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa, bei elekezi itakuwa kati ya Sh. 57,000 na Sh. 63, 200, hizi zitaanza kutumika rasmi tarehe 1 Septemba, 2019 na zitaendelea kutumika hadi pale itakapotangazwa bei nyingine," alisema.

Waziri Hasunga alisema bei hizi ni kikomo cha juu kwa mkulima katika eneo husika, hivyo wafanyabiashara wanaweza kuuza chini ya bei elekezi bila kuathiri ubora wa mbolea.

"Kwa kuzingatia hilo, Wizara imetoa bei elekezi ya jumla na rejareja za mbolea kwa uzani wa kilo 50, 25, 10 na 5, izingatiwe kuwa ni kosa kisheria kuuza mbolea kwa bei ya juu ya bei kikomo kwa nia ya kujiongezea kipato," alisema.

"Naagiza kwa wakuu wa mikoa na wilaya kukaa na kamati za pembejeo na kurekebisha bei hizi ili ziendane na hali halisi ili kurahisisha usambazaji na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima," alisema.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (kulia), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe (kushoto), wakiwa ndani ya kibanda ambacho kimejengwa ndani ya Msitu wa Hifadhi ya Kumbulu uliopo wilayani Gairo mkoani Morogoro, juzi. Msitu huo unaosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ambao umevamiwa na baadhi ya wananchi na kuuharibu kwa kiasi kikubwa. **PICHA: WMU**

# Kesi ya kina Tenga yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI ya kutakatisha fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms akiwamo wakili wa kujitegemea, Dk. Ringo Tenga na wenzake, imepigwa kalenda mpaka Septemba 10, mwaka huu.

Kesi hiyo imetajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri unaandaa nyaraka muhimu kwa ajili ya kukamilisha kesi hiyo kuhamishiwa Mahakama Kuu, Divisheni ya Uhujumu Uchumi maarufu kama ya mafisadi.

Alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 10, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mapema Aprili 5, mwaka huu, upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

"Mheshimiwa hakimu kesi hii imepangwa kwa ajili ya kutajwa na Jamhuri tunaifahamisha mahakama kwamba upelelezi wake umekamilika na tunaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza mchakato wa kusikilizwa," ulidai upande wa Jamhuri.

Mbali na Dk. Tenga washtakiwa wengine ni Mhandisi na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Hafidhi Shamte, maarufu Rashidi Shamte, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha wa kampuni hiyo, Noel Chacha na kampuni ya Six Telecoms Limited, wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni nane.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, hivyo kuwafanya wasote mahabusu kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

# Bibi alipwa nusu bilioni fidia ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemaliza mgogoro uliodumu miaka 43 kati ya mmiliki wa eneo lenye ukubwa wa ekari 6. 8 lililoko Makao Mapya jijini Arusha, Naasi Murio na wavamizi 110 kwa kuamuru alipwe Sh. 519,380, 000 na watu hao.

Lukuvi alihitimisha mgogoro huo jana alipozungumza na wavamizi hao katika mkutano uliofanyika katika uwanja wa Shule ya Sekondari Sinon na kwamba bibi huyo atatakiwa kulipwa fedha hizo ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa.

Alisema uamuzi uliofanywa na serikali kuwataka watu hao aliowaita wavamizi kumlipa bibi Muruo kiasi hicho cha fedha ni huruma kwa kuwa mahakama ilishatoa uamuzi kwa kumpa haki mmiliki na kilichotakiwa ni utekelezaji wa amri ya Mahakama ya watu hao kuondolewa katika eneo hilo.

Aidha, Lukuvi alisema thamani ya kiwanja katika eneo hilo kwa sasa ni Sh. 50,000 kwa mita za mraba, lakini kwa huruma ya serikali, watatakiwa kulipa Sh. 20,000 kwa mita hiyo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wananchi waliovamia eneo hilo lenye nyumba za makazi, biashara na kanisa, wanatakiwa kumlipa bibi Murio fedha hizo kulingana na ukubwa wa kila kiwanja cha mtu aliyevamia.

Hata hivyo, Waziri Lukuvi alisema mbali na watu hao kiasi hicho cha pesa, watatakiwa kulipa pia gharama zingine za umilikishwaji kama vile fomu ya maombi ya kiwanja na gharama ya kutengenezewa hati.

Aliagiza ramani ya eneo lililovamiwa ibandikwe katika eneo la wazi ili watu hao wahakiki maeneo yao pamoja na majina na yule atakayeridhika alipe kiasi cha pesa anachotakiwa kulipa na kupatiwa hati ya umiliki katika muda mfupi.

Mmoja wa wavamizi wa eneo hilo, Alhaji Omar Mgaza, aliiomba serikali kufikiria uwezekano wa kuongeza muda wa kulipa fedha hizo kwa kuwa baadhi yao uwezo wao ni mdogo.

Hata hivyo, Lukuvi aliwaeleza kuwa muda huo hauwezi kupunguzwa na mvamizi atakayeshindwa kukamilisha malipo kwa wakati atoe sababu kwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha.

Naye Katibu wa Kanisa la EAGT, Dk. Leonard Mwizarubi, aliimwomba waziri kulifikiria kanisa hilo kupunguza gharama za kumlipa bibi huyo kwa kuwa wanatoa huduma na hawafanyi biashara.

Kwa muda mrefu eneo hilo limekuwa na mgogoro mkubwa uliloanzia ngazi ya familia na kusababisha baadhi ya maeneo kuuzwa kwa wavamizi na bibi kuondolewa katika eneo alilokuwa akiishi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**

Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470 Dodoma

**28/08/2019.**

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **30/08/2019 Kampuni ya Mussa holdings** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Moshi kupitia **Bomangombe -Kia. Gari lenye namba za usajili T277ALQ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0
3. Njia itakayotumika ni Moshi, Bomangombe - Kia

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470 Dodoma

**28/08/2019.**

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe **01/09/2019 Kampuni ya Mussa holdings** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Kia kupitia **Bomangombe -Moshi.** Gari lenye namba za usajili **T277ALQ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   Urefu - 9.7
   Upana - 3.0
   Kimo - 3.0
3. Njia itakayotumika ni Kia, Bomangombe - Moshi

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

### KADI YA GARI IMEPOTEA

BONIFACE JOSEPH ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO T227 BVG ENGINE NO 1ZZ0963353 CHASSES S NO ZZT240011119

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**ARU/ARU/RB/244236/2019**

215394702

### KUPOTEA KWA KADI

Honester Benedict Ndunguru anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji aina ya TVS KING yenye namba ya usajili MC 119 AAE, engine namba OK4BE4063521.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa :
**CHA/RB/405/2019**

215393902

### KUPOTEA KWA KADI


Agatha Benedict Ndunguru anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji aina ya TVS KING yenye namba ya usajili MC 653 AVR, engine namba OK4FD1139051.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa :
CHA/RB/405/2019

215394002

### KUPOTEA KWA CHETI



**Diones Majogo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0140-0025** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1993 katika shule ya Sekondari Mzumbe.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/OST/RB/2483310/2019

215393602

### KUPOTEA KWA CHETI



**Derick Mathew** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0387-0069 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Karagwe.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: KAR/RB/3303/019

215393002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 91 YA 2018**
**BAINA YA**
**GODFREY MASSAMA MAKEY..............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ALLY SHARIF AIDAN**
**JABIR HAMIS JABIR .............WADAIWA**

KWA:-JABIR HAMIS JABIR
POPOTE ULIPO

**YAH:KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa /mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 25.09.2019 saa 3.00 asubuhi.Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO:-Kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya Mwezi wa Agosti,2019.

R. S. S. Mandari,
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ,
DODOMA.

215394502

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ARISTIDES MUTUNGI KENIZIO. anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SAN LG Yenye namba za usajili MC 820 BUY. Chassis Na.LBRSPKB51H9005834..

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/-DOD/RB/249507/2019.

215394602

### TANGAZO LA WIZI



**Hamisi Malashi Abdallah** mwenye picha hapo juu ambaye ni dereva wa magari makubwa anatafutwa kwa tuhumu za wizi kwa muibia muajiri wake Vanilla Enterprises Company Ltd. Kwa yeyote atakaye mwona atoe taarifa kituo cha polisi na zawadi nono itatolewa Tsh. 1,000,000.

Taarifa ya polisi
DOM/RB/8932/2019

215393402

### KUPOTEA KWA KADI

Maria Ansgar Komba anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA-IST yenye namba ya usajili T273 DJU. Yenye chasis namba NCP 60-0228713.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/KIJ/RB/247358/2019

215393502


**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako la Nipashe kila

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MALIPO KWA MAFUNGU YAMCHELEWESHA NEYMAR

**BARCELONA,** Hispania

KLABU za Paris Saint-Germain na Barcelona zimepanga bei ya kumuuza na kumnunua Neymar kuwa euro milioni 170, lakini utaratibu wa malipo ndio unachelewesha dili hilo, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, wanataka fedha zote hizo zilipwe kwa pamoja, lakini miamba hao wa Catalunya wanafikiria utaratibu wa malipo tofauti hasa baada ya kufanya usajili mkubwa kipindi hiki cha majira ya joto kwa kuwanunua Antoine Griezmann, Frenkie De Jong, Neto na Junior Firpo ambao jumla yao ni euro milioni 239.

Wakati wa mazunguzmo ya pande hizo mbili Jumanne, Barcelona ilitoa ofa ya kuilipa kwanza PSG euro milioni 40 kwa mwaka huu 2019, na malipo mengine ya euro milioni 65 yalipwe mwaka 2020 na 2021.

Lakini mabingwa hao wa Ligue 1 walikataa wazo hilo na walisisitiza kwamba wanataka ada yote ilipwe kwa pamoja.

Barca inajaribu kumuongeza Ousmane Dembele ili kukamilisha dili hilo, lakini mpango huo unaweza kushindikana kwa sababu wakala wa Mfaransa huyo alisisitiza hivi karibuni kwamba mteja wake anataka kubakia hapo Camp Nou.

Vyanzo zaidi vimeitonya ESPN kuwa Neymar mwenyewe amekuwa katikati ya majadiliano hayo kwani anataka kurudi Barcelona alikoondoka mwaka 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 222.

Klabu hizo mbili zinaendelea na mazungumzo kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili Septemba 2, mwaka huu.

# Bury yaondolewa kwenye Ligi, Bolton yapewa siku 14

**LONDON,** England

BURY, moja ya klabu kongwe zaidi katika soka la Uingereza iliondolewa kushiriki ligi ya soka Jumanne baada ya kushindwa kumaliza matatizo yao ya kifedha au kupata mnunuzi mpya, huku Bolton ikipewa siku 14 kumaliza matazito yao.

Kampuni ya C&N Sporting Risk iliachana na mpango wake wa kuinunua klabu hiyo ya Ligi Daraja la Kwanza dakika chache kabla muda uliopangwa kufika.

Bury ilijiunga na ligi ya soka mwaka 1894, miaka tisa baada ya kuanzishwa, na ikashinda Kombe la FA mwaka 1900 na 1903.

Hiyo ni timu ya kwanza kuondolewa kwenye kushiriki ligi yoyote ya soka tangu Maidstone mwaka 1992.

Wakati Bury ikiondolewa kushiriki ligi ya soka, wao Bolton wamepewa siku 14 kumaliza matatizo yao ya kifedha au kupata mnunuzi mpya.






# Dele Alli kuiwahi Arsenal Jumapili

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham imepata habari nje ya kuimarika kwa kikosi chake, baada ya Dele Alli kurudi kwenye mazoezi ya kikosi cha kwanza Jumanne.

Spurs watakutana na wapizani wao wa jiji moja la London, Arsenal Jumapili hii na itakuwa ikihitaji pointi tatu baada ya kupata pointi nne kwenye mechi zake tatu za mwanzo.

Alli anarudi uwanjani kutoka kwenye majeraha ya misuli ya paja na kocha wake, Mauricio Pochettino amesema hatakuwa na haraka kumtumia mchezaji huyo hadi awe fiti kabisa.

Spurs haitaki kujiweka kwenye hatari kwa kuharakisha kumchezesha mchezaji ambaye amekuwa na matatizo ya maumivu ya misuli mara kwa mara.

Pochettino alisema: "Ni zama zile zile. Ndio, bila shaka tuna hofia.

"Bado ni kijana. Ndio kwanza ana umri wa miaka 23, wengine wamekuwa wakikumbwa na matatizo ya kuumia misuli ndani ya miaka hii michache.

Spurs ilifungwa nyumbani bao 1-0 na Newcastle Jumapili iliyopita na ilishindwa kutengeneza nafasi za kufunga huku nyota wao Christian Eriksen akianzia benchi.

## HABARI MICHEZO

# SHAW KUKAA NJE WIKI SITA




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inahofu Luke Shaw anaweza kuwa nje ya uwanja kwa zaidi ya mwezi mmoja baada ya kuumia misuli, kwa mujibu wa ESPN FC.

Beki huyo wa kushoto alilazimika kuondolewa uwanjani kipindi cha pili wakati wakiwa wamefungwa mabao 2-1 na Crystal Palace Jumamosi baada ya kupata maumivu hayo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ataukosa mchezo dhidi ya timu yake ya zamani ya Southampton Jumamosi, ukiwa ni mchezo wa mwisho wa United kabla mapumziko ya mechi za kimataifa.

Pia huenda asiwapo kwenye kikosi cha kocha wa timu ya Taifa ya England chini ya kocha, Gareth Southgate dhidi ya Bulgaria na Kosovo na anaweza kuikosa mechi dhidi ya Leicester pale Old Trafford Septemba 14, mwaka huu.

Shaw anatarajiwa kufanyiwa uchunguzi zaidi wiki hii, lakini inaonyesha wazi kwamba anaweza kukaa nje ya dimba kwa zaidi ya wiki sita, pia ataukosa mchezo wa nyumbani dhidi ya Arsenal Septemba 30.

Ashley Young anatarajia kuanza mchezo wake wa kwanza dhidi ya Southampton baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kuchukua nafasi ya Shaw dhidi ya Palace.

Marcos Rojo, ambaye alikuwa anatakiwa na Marseille, AC Milan na Monaco, anaweza pia kuanza.

Hata hivyo, kocha Ole Gunnar Solskjaer hataweza kumtumia Diogo Dalot.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye anacheza nafasi zote za beki ya pembeni atakuwa nje ya uwanja hadi baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa kwa sababu aliumia kwenye mazoezi.

# Robben afikiria kurudi dimbani



**AMSTERDAM,** Uholanzi

WINGA Mholanzi, Arjen Robben, amekataa kufuta uwezekano wa kurudi kwenye soka, licha ya kustaafu mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye hivi karibuni alitangaza kwamba ataachana na kucheza soka baada ya kutimiza miaka 19 dimbani, amebainisha kwamba anaweza kufikiria kurudi tena kama ataweza kuwa fiti.

Robben ambaye alishinda mataji manne makubwa katika nchi nne tofauti, anahofia kwamba anaweza 'akawa anakikosa kitu anachokipenda' kwa miezi inayokuja.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kurudi, Robben aliiambia Redio NPO: "Mara zote nasema kamwe usiseme kamwe."

"Pengine mwezi mmoja au miwili nitakuwa na hisia za ajabu kwamba nimekikosa kitu nilichokuwa nakipenda na nitaamua kurudi tena.

"Lakini bila shaka haiwezi kuwa rahisi hivyo kwa sababu umri unakufanya uchoke. Lakini siwezi kusema kwamba, sitakuwa na uwezekano wa kurudi uwanjani."

Nyota huyo alishinda taji la Ligi Kuu ya England mara mbili katika misimu yake miwili pale Chelsea na alifunga bao la ushindi kwa Bayern Munich wakati ikitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013, lakini siku zake za mwisho kwenye mchezo huo zilitawaliwa na kuwa majeruhi.

# Ozil hana mpango kuondoka



**LONDON,** England

LICHA ya kutopata nafasi ya kuichezea Arsenal mchezo hata mmoja msimu huu, wakala wa Mesut Ozil, Dkt. Erkut Sogut amesisitiza mteja wake atasalia kwa 'Washika Bunduki' hao wa jijini London.

Ozil ambaye amerhusiwa na watu wa usalama England kuendelea na majukumu yake baada ya uchunguzi wa tukio la kuvamiwa kwake akiwa na Sead Kolasinac kumalizika, hakuwa sehemu ya kikosi cha Arsenal kilichocheza dhidi ya Liverpool.

Erkut alisema mteja wake hawezi kwenda popote majira haya ya kiangazi pamoja na kuwindwa na Fenerbahce ya Uturuki.


Ozil anakabiliwa na changamoto ya kuingia kwenye mfumo wa soka la kasi na pasi za kwenda mbele la Unai Emery.

Mchezaji huyo ambaye analipwa mshahara mkubwa zaidi katika kikosi hicho, amekuwa akionekana kutokuwa kwenye mipango ya kocha Emery na kwamba mara kadhaa wamejaribu kumuuza bila mafanikio.

Ozil ambaye alitua hapo Arsenal akitokea Real Madrid ya Hispania, mara kadhaa amekuwa akisisitiza kuwa hana mpango wa kuondoka kwenye klabu hiyo.

Arsenal ambao walipoteza wiki iliyopita mbele ya Liverpool kwa mabao 3-1, watakuwa na kibarua kizito nyumbani Jumapili Septemba Mosi kucheza na Tottenham ambao ndio mahasimu wao wakubwa.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SANCHEZ AMFUATA LUKAKU INTER MILAN

### ●●● United kuendelea kuingia hasara kwa kumlipa sehemu ya mshahara huku ikibaki na...

**MILAN,** Italia

INTER Milan imekubali kuinasa saini ya mshambuliaji wa Manchester United, Alexis Sanchez kwa mkataba wa mkopo wa miezi 10, Sky Sports News inalitambua hilo.

**Mkataba huo wa miezi 10, utaigharimu Manchester United takriban pauni milioni sita na Inter haijakubali mbadala wa kumnunua jumla Sanchez mwishoni mwa msimu wakati huu ikiwa tayari imeshamnasa straika Mbelgiji Romelu Lukaku kutoka hapo Old Trafford.**

Sanchez ambaye alikuwa akilipwa mshahara mkubwa zaidi hapo United, inadhaniwa atakuwa akivuta pauni 400,000 kwa wiki, akiwa Inter.

Na ilidaiwa United itachangia kiasi cha mshahara na wiki iliyopita Inter ilitoa ofa ya kumlipa pauni 150,000 kwa wiki lakini United ilitaka zaidi.

Lakini sasa miamba hiyo ya Serie A inatarajia kuchangia takriban pauni milioni 4.5 katika mshahara wa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Chile kwa kipindi hicho cha miezi 10, kwa mujibu wa Sky in Italy, na Sanchez alitarajiwa kutua Milan jana tayari kwa kufanyiwa vipimo vya afya.

Sanchez alivutia kwa kiwango bora wakati akiitumikia Chile kwenye michuano ya Copa America majira haya ya joto, lakini bado hajapata nafasi ya kuichezea United msimu huu baada ya kusumbuliwa na majeraha wakati akicheza mechi ya kusaka mshindi wa tatu.

Alicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Sheffield United karibia na dirisha la usajili England kufungwa wakati akiendelea kujizatiti.

Inter tayari ilishamsajili Lukaku kutoka United kwa ada takriban pauni milioni 73 mapema mwezi huu.

Kuondoka kwa Sanchez kutaiacha United ikiwa na Anthony Martial, Marcus Rashford na kinda mwenye umri wa miaka 17, Mason Greenwood katika safu ya ushambuliaji ya kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer.

United itakuwa bila Martial kwa muda kutoka na kukumbwa na majeraha ya paja wakati wakikubali kipigo cha mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Crystal Palace Jumamosi.

## ZISIKUPITE

### IBRAHIMOVIC AIITA UNITED

MSHAMBULIAJI wa LA Galaxy, Zlatan Ibrahimovic, 37, amesema atakaribisha kurudi Manchester United, sehemu aliyofunga mabao 29 kwenye mechi 53 kabla ya kuelekea Marekani. ***(Daily Star)***

### SPURS YANAWA KWA ERIKSEN

TOTTENHAM haina uhakika na malengo ya Christian Eriksen baada ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mwenyekiti Daniel Levy na wakala wa kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark mwenye umri wa miaka 27. ***(Guardian)***

### REDKNAPP AIPA SOMO SPURS

KOCHA wa zamani wa Tottenham Harry Redknapp anaamini Christian Eriksen anapaswa kuanza Spurs licha ya kutoeleweka kwa mustakabali wake wa baadaye. ***(Talksport)***

### LOVREN AIRUDISHA UPYA ROMA

ROMA inajiandaa kutoa ofa mpya kwa beki wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren, 30. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### NAPOLI YAMSIKILIZIA ICARDI

NAPOLI bado inashikilia kutoa mkataba wa miaka miwili kwa Fernando Llorente, 34, ambaye ni mchezaji huru wakati huu ikiendelea kusubiri kujua mazungumzo yatakavyokwenda kati ya Mauro Icardi, 26, na Inter Milan. ***(Corriere dello Sport via Football Italia)***

### VELA CHUPUCHUPU ATUE BARCA

STRAIKA wa zamani wa Arsenal, Carlos Vela, 30, amefunguka kuwa alikaribia kujiunga na Barcelona kwa mkopo akitokea klabu yake ya sasa, LAFC. ***(BS Podcast via Goal)***

### NACHO AKARIBIA SOCIEDAD

REAL Sociedad inataka kuharakisha mchakato wa kumnasa beki wa Arsenal, Nacho Monreal hivyo anaweza kujifua na klabu hiyo na kuichezea kwa mara ya kwanza Ijumaa usiku. Beki huyo mwenye umri wa miaka 33, amepewa ofa ya miaka miwili huku kukiwa na kipengele cha kuuongeza kwa miezi 12. ***(Express)***

### LEICESTER KUMUUZA GHEZZAL

LEICESTER ipo katika mazungumzo na Olympiakos kuhusu dili la kuwauzia winga Rachid Ghezzal, 27. ***(Sky Sports)***

### LANZINI, WEST KUMALIZANA

WEST Ham inakaribia kukubaliana suala la mkataba mpya na kiungo Muargentina Manuel Lanzini, 26. ***(Sky Sports)***

### MARTINEZ AMFUNGUKIA LUKAKU

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku, 26, alitaka kuondoka Manchester United kwa sababu alichoka Old Trafford, kwa mujibu wa kocha wake wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez. ***(Mirror)***

### TOSUN AING'ANG'ANIA EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Everton na Uturuki, Cenk Tosun, 28, anataka kuendelea kubaki katika klabu hiyo licha ya tetesi zinazomhusisha na kujiunga na Eintracht Frankfurt. ***(Turkish Football)***

## Nkamia awashukia wanaoiponda Simba SC

**Na Shufaa Lyimo**

KATIBU Mwenezi wa zamani wa Klabu ya Simba, Juma Nkamia, ametoa ya moyoni baada ya kushindwa kuvumilia kauli za kejeli kutoka kwa baadhi ya Watanzania wanaodharau klabu hiyo kutokana na kuwahi kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Jumapili iliyopita ikicheza katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Simba ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, hivyo kutolewa katika raundi ya awali kwa faida ya bao la ugenini kufuatia mchezo wa kwanza ugenini kutoka suluhu.

Akizungumza kwa uchungu juzi, Nkamia alisema amesikitishwa na Watanzania kwa kitendo hicho badala ya kutafuta kilichosababisha Simba itolewe.

"Hili ni janga la Taifa, si la Simba kwa sababu Simba ilikuwa inaiwakilisha Tanzania ni wakati wa kuwa kitu kimoja kutafuta sababu iliyoifanya itolewe mapema tuache u-timu," alisema Nkamia.

Aidha, aliongeza licha ya kutolewa Simba ilijitahidi kucheza mpira mzuri japokuwa kulikuwa na mapungufu machache ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi na kocha na si vinginevyo.

"Wachezaji walijitahidi kucheza mpira tukubali walikutana na timu nzuri tuache tabia ya 'kujaji' (kuhukumu) kwa nini kocha hakuchezesha wachezaji fulani yeye ndiye mwenye maamuzi," alisema.

## Ndayiragije: Lugha tatizo kikosi Azam

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kuifunga timu ya KMC FC kwa bao 1-0 katika mchezo wao wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya Vodacom juzi, Kocha Mkuu wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, amesema haikuwa rahisi kupata ushindi huo kutokana na timu zilivyokuwa zimekamiana.

Akizungumza na Nipashe jana, Ndayiragije alisema amefurahishwa na viwango na umakini ulionyeshwa na wachezaji wake ingawa bado kuna tatizo la kushindwa kuelewana lugha kati ya wazawa na nyota wa kigeni.

"Mchezo ulikuwa mgumu nashukuru wachezaji wangu wamefanya nilichowaelekeza kitu ambacho kimenipa matumaini, ila bado kuna shida ya mawasiliano," alisema.

Alisema ataendeleza ushindani katika mechi zote za Ligi Kuu, lengo likiwa ni kuiweka mahali pazuri timu yake.

Aliongeza kuwa timu yake itapata mapumziko mafupi kupisha majukumu ya timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa kucheza na timu ya Taifa ya Burundi ugenini katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar 2022.

# LIPULI YAANZA TAMBO

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

BAADA ya kuanza msimu wa Ligi Kuu ya Vodacom kwa ushindi mnono wa mabao 3-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Lipuli, Heremana Haruna, ametamba kikosi chake kuendelea kuvuna pointi zaidi katika mechi zijazo kutokana na uimara wa kikosi chake na kusakata kandanda la kuvutia.

Ikiwa katika uwanja wao wa Samora mjini Iringa Jumapili iliyopita, Lipuli ilianza ligi hiyo kwa kishindo, shukrani zikiwaendea wapachika mabao hayo, Paul Materezi, Daruweshi Saliboko na Seif Abdallah.

**Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Lipuli, Haruna, alisema licha ya uimara wa kikosi chake na kucheza kandanda la kuvuti, pia matumaini zaidi kwake ya kuendelea kutesa Ligi Kuu ni kutokana na ukweli kwamba katika mchezo huo hakutumia nyota wake wote.**

Alisema wachezaji wengine wa kutoka nje hawakucheza kutokana na kutokamilisha vibali, jambo ambalo ana matumaini mechi ijayo kila kitu kitakuwa tayari kwao na kuanza kuitumikia timu hiyo ambayo msimu uliopita ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu iliyojumuisha timu 20 kama ilivyo kwa msimu huu wa 2019/20.

Hata hivyo, Kocha wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, naye alikiri Lipuli kucheza vizuri zaidi, lakini akiweka wazi kuwa kupoteza kwao kulitokana na uzembe wa makosa waliyoyafanya na kukosa umakini kwa baadhi ya wachezaji.




Kutoka kushoto ni mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sadick Mangesho, Mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Magabe Marwa akifuatiwa na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, mshindi wa Jackpot Kingsley Pascal. **PICHA: SPORTPESA**

# Marwa, Pascal na milioni 825/- Jackpot SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

Baada ya Jackpot ya SportPesa kuvunjwa kwa mara ya kwanza ikiwa imefikia jumla ya Sh. 825,913,640 na washindi wawili kupatikana, jana wamekabidhiwa rasmi mkwanja wao kila mmoja akichomoka na kitita cha Sh. 412,956,820 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13 wiki iliyopita.

Kingsley Pascal mwenye umri wa miaka 26, akitokea Biharamulo ameshinda Jackpot hiyo pamoja na Magabe Marwa mwenye miaka 31 kutoka wilayani Serengeti wote wakigawana kwa usawa kitita hicho cha Jackpot.

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas akizungumza wakati wa kukabidhi hundi kwa washindi hao wa kihistoria, alisema: "Nafurahia kuwakabidhi washindi wetu wa shilingi 825,913,640 za Jackpot yetu ambayo ndiyo kubwa zaidi nchini, na hii ikiwa ni mara ya kwanza kwenye historia ya 'betting Tanzania' kwa kiasi kama hichi kutolewa kwa washindi wa michezo ya kubahatisha.

"Naomba mtambua kila wiki watu wanacheza michezo mbalimbali na SportPesa ila kwenye hii 'segment' (sehemu) ya Jackpot, tangu tumeanza tumetoa zaidi ya bilioni 4.4 kwa washindi na kati ya pesa hizi kodi ni Sh. milioni 864 na hutujawahi kupata malalamiko kutoka kwa washindi wetu na wamekuwa wakituamini na kuwa na uhakika wa kushinda."

Kwa upande wa washindi kila mmoja akionyesha furaha ya kipekee wakifurahia ushindi wao, na wote wakikiri kuwa pesa zote hizo ni za kwao, Marwa ambaye pia akiwa na mkewe, Elizabeth Wambura, alionekana kuwa na furaha isiyo ya kawaida kabisa.

"Leo ndio nimeamini rasmi baada ya kukabidhiwa fedha hizi na kuamini kwa macho yangu kama nimeshinda, naomba Watanzania waamini kuwa mimi nimeshinda kweli na si vinginevyo.

"Watanzania waamini mimi sifahamiani na mtu yeyote SportPesa na kuibuka mshindi niliweka mkeka mmoja wa shilingi 2,000 tu."

Pascal alipoulizwa kuhusu watu wasioamini kama wanaweza kushinda, alisema: "Huwezi kupata kitu usipojaribu na mimi ni mtu wa kujaribu vitu vingi na sasa ni mshindi wa Jackpot ninachoweza kusema kila mtu anaweza kushinda akijiamini na kuweka nia bila kukata tamaa.

"Tangu nianze 'kubeti' Jackpot mwezi wa tatu mwaka huu hii ni mara ya 17 kama si 16 na nimebahatika kuibuka mshindi wa Sh. milioni 412."

Michezo

Alhamisi Agosti 29, 2019

Nipashe



Sanchez amfuata Lukaku Inter Milan

UKURASA 30



Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga, akipiga mpira wa faulo ambayo hata hivyo ilishia mikononi mwa kipa wa Ruvu Shooting, Bidii Hussein, katika mechi ya Ligi Kuu ya Vodacom iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jana na Ruvu kushinda bao 1-0. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Yanga 'yapapaswa' Uwanja wa Uhuru

## ●●● Straika wa Zahera bado shida, Ruvu Shooting yalia na mwamuzi kuwanyima la pili...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza tangu ipande Ligi Kuu, timu ya Ruvu Shooting inayotamba na msemo wao wa "papaso squared", imefanikiwa kuichapa Yanga bao 1-0 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana.

**Ni mara ya 18 timu hizo kukutana tangu Ligi Kuu ya 2007/08, Yanga ikishinda mara 15, zikitoka sare mara tatu na Ruvu Shooting imeweka rekodi ya kushinda kwa mara ya kwanza jana.**

Yanga inayonolewa na Mwinyi Zahera, iliuanza mchezo kwa kasi na dakika ya tano tu Papy Tshishimbi aliunganisha mpira wa krosi kutoka winga ya kushoto, lakini golikipa Bidii Hussein aliupangua na kuwa kona tasa.

Dakika moja baadaye, Said Dilunga akiwa anatazamana na kipa Farouk Shikalo wa Yanga alipiga shuti kali lililopaa juu ya lango.

Ruvu Shooting iliandika bao dakika ya 21, baada ya mpira mrefu ambao Sadat Mohamed aliwazidi mbio mabeki wa Yanga na kuudokoa uliomshinda kipa Shikalo aliyekuwa ametoka golini na kujaa wavuni.

Baada ya bao hilo Ruvu ilionekana kurudi nyuma kulinda lango, hivyo kuiachia Yanga kufanya mashambulizi mfululizo.

Tshishimbi kwa mara nyingine tena alikosa bao dakika ya 27 baada ya mpira alioupiga kwa kichwa kuokolewa na kipa Bidii, huku David Molinga akiikosesha Yanga mabao mawili dakika za nyongeza za kipindi cha kwanza.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, na kuingia kwa Mrisho Ngassa na Mapinduzi Balama kulileta uhai kwa Yanga, lakini mabeki wa Ruvu, wakiongozwa na kipa wao Bidii ambaye alionyesha bidii kubwa kuokoa michomo ya mastraika wa Yanga wakiongozwa na David Molinga, Sadney Urikhob na Juma Balinya ambaye alitolewa kipindi cha pili.

Mfungaji wa goli hilo, Sadat alisema kuwa anajisikia furaha sana kuifunga timu kubwa kama Yanga na kuongeza kuwa alipopewa pasi, alitulia kwa sababu alijua kabisa kuwa atafunga.

Kwa upande wa nahodha wa Yanga, Tshishimbi alisema walitengeneza nafasi nyingi, lakini mastraika wao hawakuwa makini ndiyo sababu ya kupoteza mechi hiyo.

"Mashabiki wetu watulie na wasivunjike moyo kwa sababu makosa tuliyoyafanya tunakwenda kurekebisha na mechi ijayo huenda tutafanya vizuri."

Msemaji wa Ruvu Masau Bwire, pamoja na kutamba kuwa 'wamewapapasa' Yanga, alilaumu bao lao lililokataliwa ambalo alidai lilipaswa kuwa la pili na kuitaka Kamati ya Waamuzi kuwachukulia hatua waamuzi waliochezesha mechi hiyo.

"Tumewapasa na niliahidi tangu mwanzo, lakini Kamati ya Waamuzi ichunguze bao la pili ambalo mwamuzi alidai ni la kuotea na ikiwezekana adhabu kali ichukuliwe," alisema.

# Simba: Maisha lazima yasonge

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba leo ikishuka Uwanja wa Uhuru kuwakabili JKT Tanzania kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Vodacom msimu huu, mashabiki wa timu hiyo na wachezaji wametakiwa wasiumie sana na wavumilie kejeli zinazoelekezwa kwao kwa kuwa "maisha lazima yasonge mbele".

Simba inaugulia maumivu ya kutolewa kwenye raundi ya awali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na UD Songo ya Msumbiji kwa faida ya bao la ugenini kufuatia sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa ikiwa ni baada ya mchezo wa awali ugenini kutoka suluhu.

Kutokana na matokeo hayo, watani zao, mashabiki wa Yanga, wamekuwa wakiwarushia vijembe na maneno ya kejeli baada ya kutolewa huku wao wakisonga raundi ya kwanza ya michuano hiyo kufuatia kuitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1.

Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, kupitia mtandao wake wa Instagram jana alisema: "Najua wachezaji wetu mmefadhaika, najua Wanasimba wote mmeumia, mimi nakejeliwa na kutukanwa kila mahali, lakini niwasihi watu wangu, msiumie sana na maisha lazima yasonge mbele.

"Zinafungwa klabu kubwa duniani nini Simba? Hiki ni kipindi kigumu lakini lazima tukivuke kwa kila hali na ni wajibu wetu kuwa wamoja 'now' (sasa), na niwahakikishie tena na tena, tutarudi kwa nguvu kubwa sana, tumejifunza na tushajuana klabuni 'which is which'! Na kwa wale wawachekao leo vuteni subira nao."

Msimu uliopita Simba ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, jambo ambalo wengi walitarajia inaweza kufikia hapo ama hata kutinga nusu fainali, lakini mambo yamekuwa sivyo.

Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems baada ya kutolewa, yeye ameahidi nguvu zote kugeuzia kwenye ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho (FA Cup) pamoja na mataji mengine.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002